

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 25 Aprili, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani :-

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:-

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report and Accounts of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) for the year ended 30th June, 2007*).

MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:-

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa Mwaka 2007/2008.

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE (k.n.y MHE. GIDEON A. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:-

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Kilimo na Ardhi kwa Mwaka 2007/2008.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 173

Ukosefu wa Mahali pa Kulaza Wagonjwa

MHE. JANETH M. MASSABURI aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na malalamiko mengi ya wagonjwa kwenye Hospitali za Amana, Temeke na Mwanyamala; na zahanati nyingine nchini juu ya

wagonjwa kulazwa wawili, watatu au wanne kwenye kitanda kimoja; na kwa kuwa, hali hiyo husababisha wagonjwa na wauguzaji kuambukizwa maradhi mengine kutokana na mlundikano huo usiozingatia kanuni za afya:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga wodi kwenye hospitali hizo kwa kuzingatia takwimu halisi za wagonjwa na kwa kutofautisha maradhi mbalimbali?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha zahanati zilizoko kwenye maeneo ya pembezoni kama Msongola, Pugu na Pembe Mnazi kwa kuzipandisha hadhi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuwa kumekuwepo na msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Amana, Mwanyamala, Temeke na hospitali nyingine kutokana na ufinyu wa nafasi. Hali hii inatokea baada ya hospitali ya Rufaa ya Taifa Muhimbili kupokea wagonjwa wa Rufaa tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hali hiyo, Serikali kuititia Halmashauri za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni imefanya jitihada za kukabili tatizo hili.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala upanuzi wa wodi ya wazazi katika Hospitali ya Amana umefanyika katika kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2007/2008 kwa kuongeza wodi yenyе vitanda 60 ambavyo inalenga kupunguza msongamano katika wodi ya wazazi, ukamilikaji wa wodi hii utaongeza vitanda kutoka 60 hadi vitanda 120 na hivyo kupunguza msongamano katika wodi ya wazazi. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala inaandaa mapendekezo ili kutafuta fedha shilingi bilioni 1.6 za kujengea ghorofa na kubomoa baadhi ya wodi zilizopo ili kukabiliana na ufinyu wa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa mwaka 2006 ilifanya ukarabati katika Hospitali ya Temeke kwa kuongeza wodi ya wazazi yenyе vitanda 24, kujenga wodi ya muda na kuweka vitanda 20, hadi kufikia Desemba, 2007 hospitali ya Temeke ilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 3. Jengo hili lina wodi mbili, moja ya wanawake na nyingine ya wanaume na kila moja ina vitanda 25. Pia kuna wodi ya akinamama wajawazito yenyе vitanda 50 iliyojengwa kwa msaada wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Katika hospitali ya Mwanyamala katika Manispaa ya Kinondoni inapokea wagonjwa wengi kuliko uwezo wake. Tatizo lililopo katika hospitali ya Mwanyamala ni ufinyu wa eneo la ujenzi kwa ajili ya upanuzi wa hospitalil hiyo.

(b) Serikali imeweka mikakati ya kuboresha zahanati zilizo pembezoni na kuzipandisha hadhi ili kukidhi ongezeko la wagonjwa. Kwa mfano, Manispaa ya Ilala imekarabati kliniki ya mama na mtoto ya Makangarawe, pamoja na kujenga wodi ya wazazi katika zahanati ya Mbande na Yombo Vituka. Manispaa inatarajia kujenga Hospitali ya Wilaya maeneo ya Kivule Kata ya Kitunda kwa lengo la kuhudumia jamii iliyopo pembezoni na nje ya mji na hivyo kupunguza msongamano katika hospitali ya Amana. Katika Manispaa ya Temeke imejenga majengo kwa ajili ya Mama wajawazito katika zahanati za pembezoni za Tambuka Reli, Mji Mwema, Rangi Tatu, Tuangoma, Chamazi, Mbande Gonvu, Kimbiji na Chekeni na Mwasonga. Zahanati hizi zimepunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, zahanati za Kata za Pemba Mnazi ambako ni zahanati ya Tumbwi, Songani, Buyuni na ile ya Yaleyale Puna pamoja na zile za Kata ya Pugu hazitapandishwa hadhi kwa sababu bado hazijafikia sifa ya kupandishwa hadhi kuwa Vituo vya Afya. (*Makofit*)

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza. Kutokana na jiografia kuwa mbaya katika maeneo aliyoyataja. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda kukagua zahanati hizo za Mkoa wa Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli jiografia ya Dar es Salaam ni ngumu na ndio maana tumejenga zahanati karibuni kila pembe ya Kata au sehemu nyingi za Dar es Salaam. Kuhusu kuzitembelea zahanati za Mkoa wa Dar es Salaam tutawasiliana mimi na yeye tuone kama mimi au Waziri wangu ni nani ambaye anawenza kufanya ziara katika zahanati hizo za Mkoa wa Dar es Salaam.

Na. 174

Muda Unaohitajika Kupata Uamuzi wa Kesi

MHE. ABUBAKAR K. BAKARY aliuliza:-

(a) Je, ni muda gani kisheria unaohitajika kuwa mtu kupata uamuzi “*Ruling*” ya kesi yake kuanzia pale ambapo Hakimu au Jaji ameshapata “*Submission*” za pande zote mbili na Jaji au Hakimu huyo kutoa kauli kwamba, atatoa maamuzi kwa taarifa?

(b) Je, muda huo unatofautiana baina ya kesi za jinai na zile za hukikia (*civil*)?

(c) Ikiwa muda huo utapita. Je, mwananchi anatakiwa afanye nini ikiwa kesi yake iko Mahakama ya Wilaya, Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa fungu la 28 la Sheria ya Mwenendo wa Madai (*Civil Procedure Code, Cap.33*) na fungu 311(1) la Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai (*Criminal Procedure Act, Cap. 20*) kama yalivyorekebishwa na mafungu 45 na 46 ya Sheria ya Utumishi wa Mahakama (*Judicial Service Act Na.2/2005*), Hakimu au Jaji anapaswa kutoa uamuzi katika kipindi kisichozidi siku sitini tangu siku ya mwisho ya kuhitimisha kesi baada ya kupokea hoja za mwisho za wadaiwa.

(b) Muda huo wa siku sitini ni kwa kesi zote za jinai na za madai.

(c) Ikiwa Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa atashindwa kutoa hukumu katika muda huo wa siku tisini, mwananchi anaweza kulalamika kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu ambaye ndiye chini ya fungu la 6 la Sheria ya Utumishi wa Mahakama 2005. Ana mamlaka ya kusimamia umalizwaji (*disposal*) wa kesi katika Mahakama. Chini ya fungu hilo, Mheshimiwa Jaji Mkuu ana mamlaka ya kumtaka Jaji ye yeyote kumpa takwimu ya kesi alizohukumu katika kipindi fulani. Pia anaweza kuchunguza malalamiko ya kutokuhukumiwa kwa kesi yoyote na kuchukua hatua anayoona inafaa au anaweza kupendekeza kuwa malalamiko ya mwananchi husika yafikishwe kwenye Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa uamuzi.

Aidha, iwapo Hakimu wa Wilaya au Mkoa akichelewa kutoa hukumu mwananchi anaweza kupeleka malalamiko yake kwa Jaji Mfawidhi wa Kanda ambaye ndiye kisheria anasimamia umalizwaji (*disposal*) wa kesi katika Mahakama za Wilaya na Mkoa.

MHE. ABUBAKAR K. BAKARY: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mwanasheria Mkuu wa Serikali swali moja la nyongeza. Pale ambapo Hakimu au Jaji anazidisha siku tisini kwa makusudi hatuoni kwamba haki za mwananchi zinakataliwa kwa makusudi?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Spika, kama Jaji au Hakimu anapitisha zile siku tisini inategemea, inawezekana kabisa ni kwa sababu ya uzito wa kesi ambayo ilikuwa mbele yake au kesi iliyokuwa imepelekwa ilikuwa *complicated* kidogo. Ndiyo sababu tunasema kwamba chini ya Sheria *Judicial Service Act Na.2/2005* mwananchi ambaye anaona kwamba hukumu yake imecheleweshwa anaweza kwenda kwa Jaji Mkuu kwenda kutoa malalamiko yake, na kule Mikoani anaweza kwenda kwa *Judge in-charge* ili kutoa malalamiko yake ili aweze kuyachunguza na kujua ni kwa sababu gani huyo Mheshimiwa Jaji au Hakimu ameshindwa kutoa hukumu katika muda ule ambao umepangwa.

MHE. HAMAD R. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ikiwa Jaji amechelewa kutoa hukumu kwa muda wa mwaka moja na nusu, kwa mfano, kesi ya kwetu sisi watu kumi na nane(18), Jaji huyo anahitaji kupewa hukumu gani?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kwamba Jaji ambaye anakaa muda mrefu kama huyo hajatoa hukumu, basi mwananchi yejote ambaye anaathirika na kitendo hicho anapaswa kwenda kulalamika kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu na yeje anaweza kujua ni kitu gani cha kufanya kwa huyo Jaji ambaye amechelewa hukumu hiyo kwa muda wote huo.

Na. 175

Ujenzi wa Chuo cha VETA Longido

MHE. MICHAEL L. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Longido ni moja kati ya Wilaya zilizo nyuma kielimu; na kwa kuwa, vijana wengi wanaomaliza darasa la saba na sekondari na kukosa kazi hukimbilia Mijini kufanya kazi za ulinzi kwenye nyumba za watu; na kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga Chuo cha VETA kwenye kila Wilaya:-

Je, Serikali itakuwa tayari lini kujenga Chuo hicho huko Longido ili vijana waweze kuijiendeleza kimasomo na kujiajiri na kupunguza wimbi la vijana hao hukimbilia Mijini kufanya kazi za ulinzi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO NA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza Mpango wa Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya kwa awamu baada ya kukamilisha tathmini ya stadi zinazotakiwa katika kila Wilaya. Katika mpango huu, ujenzi umepangwa kufanywa kwa awamu kutokana na ufinyu wa bajeti.

Kwa kuanzia kipaumbele kimewekwa katika Wilaya ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi vya aina yejote ikiwemo Wilaya ya Longido. Fedha kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya kwanza zimeombwa katika mwaka wa fedha 2008/2009 na ujenzi unatarajiwa kuanza Desemba, 2008 baada ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kupata maeneo ya ujenzi katika Wilaya husika, mwezi Agosti, 2008;

- (ii) Kutafuta na kukamilisha taratibu za kuwapata wataalam elekezi (*consultants*) wa ujenzi, Septemba, 2008;
- (iii) Kuandaa michoro na kutafuta makandarasi wa ujenzi Oktoba hadi Novemba 2008; na
- (iv) Kuanza ujenzi Desemba, 2008.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kuuliza swali moja la nyongeza baada ya kusikia majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Kwa kuwa katika maeneo ya wafugaji wimbi kubwa la vijana wanakimbilia Mijini kwa sababu hawana ajira ya aina nyongeza yoyote wanayojua. Je, isingekuwa jambo la dharura kwa maeneo ya wafugaji kujenga Vyuo vya Ufundu Stadi ili nao wapate kazi mbadala kuliko kwenda kufanya kazi ya ulinzi kwa watu, na Serikali itakuwa na shughuli muhimu sana kujenga Vyuo vya VETA katika maeneo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO NA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, hicho ndiyo tumesema kwamba moja ya Wilaya ambazo tunatarajia kujenga Vyuo hivyo ambavyo tumeahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2005 ni katika Wilaya ya Longido. Tumesema tunaanza mwezi Desemba, 2008, na kabla ya kuanza ilikuwa kwanza tuangalie ni stadi zipi zinahitajika kila Wilaya kulingana na mazingira na fursa zilizopo za uchumi kwa Wilaya hiyo.

Kwa mfano, siyo rahisi kuweka stadi ambazo zinahusiana na ushonaji katika Wilaya ya Longido. Kwa hiyo, tutaweka stadi ambazo zitawafaa vijana. Kwa hiyo, kwa kifupi Chuo hicho kitajengwa katika Wilaya ya Longido. (*Makofii*)

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Vyuo vingi vya VETA vilivyopo hapa nchini hivi sasa kikiwemo Chuo cha VETA cha Mbeya vinakabiliwa na matatizo mkubwa sana ya uhaba wa vifaa na walimu. Je, Wizara ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kwa wakati huu wanapoendelea na juhudzi za kujenga Vyuo vipyaa vya VETA kutatua tatizo hili la uhaba wa walimu na vifaa vya kufundishia na vilevile vifaa vya wanafunzi? Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO NA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, katika ujenzi huo tunaoenda kwa awamu. Katika awamu hiyo ya kwanza pamoja na ujenzi pia kuna kupanua na kuongeza vifaa kwa kutumia wafadhili na fedha zetu za ndani katika baadhi ya Vyuo ambavyo tayari viro. Kwa mfano, kuna Vyuo katika Wilaya ya Korogwe, Karagwe pamoja na Mwanga ambavyo vinaendeshwa vizuri, kwa hiyo hivi vyuo tunataka tuvipanue zaidi. Lakini pia kuna Vyuo katika Wilaya mbalimbali zikiwemo Wilaya za Mkoa wa Mbeya

vyote hivyo tuna mpango wa kuvipanua, na kuvipatia vifaa pamoja na kuwa na wakufuzi wa kutosheleza katika stadi ambavyo zinahitajika katika maeneo husika.

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO NA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kutoa ufanuzi wa nyongeza kwa swali alilouliza Mheshimiwa Cynthia Ngoye kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mbeya na katika Mikoa mingi vipo Vyuo vya VETA vya Kanda na Vyuo hivi vina vifaa vizuri sana na katika maeneo mengine vifaa hivi bado vipo kwenye mabox kwa sababu hakuna wataalam wa kuvitumia. Kwa hiyo, Wizara inachukua hatua mbili muhimu.

Kwanza, ni kubadilisha ule mtaala uliopo unaotoa dhana kwamba VETA ni mahali ambapo wanakwenda watu ambao wameshindwa masomo, na kufanya mtaala ule uwe unamwezesha mtu kutoka VETA kwenda *Technical College* na kwenda Chuo Kikuu.

Pili, tunafundisha walimu na wataalam ili waweze kuvitumia vifaa hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa ufanuzi wa ziada. Sasa swali linalofuata linaulizwa na Hassan Chande Kigwalilo wa Liwale.

Na. 176

Upungufu wa Walimu wa Sekondari Nchini

MHE. HASSAN C. KIGWALILO aliuliza:-

Kwa kuwa, shule nyingi za Sekondari hapa nchini zikiwemo za Wilaya ya Liwale zina upungufu mkubwa wa walimu na hivyo kuathiri malengo yaliyotarajiwa ya kuboresha elimu nchini:-

(a)Je, Serikali inaweza kutoa takwimu za upungufu wa walimu Kitaifa na kwa Wilaya ya Liwale ambazo ni mionganini mwa Wilaya zilizo nyuma kielimu?

(b)Je, nini kifanyike ili kukabili tatizo hilo?

(c)Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa motisha maalum kwa walimu wanaopelekwa kwenye Wilaya zenye mazingira magumu na zilizo nyuma kielimu ikiwemo ile ya Liwale?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA) aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kumjibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kikamilifu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya zoezi la kuainisha upungufu wa walimu kimasomo katika shule za sekondari za kawaida (*O-level*) na za juu (*A-level*) mwezi Desemba, 2007. Katika zoezi hilo ilibainika kuwa Shule za Sekondari za kawaida zilikuwa zinakabiliwa na upungufu wa jumla ya walimu 29,789 wakiwemo walimu 21,273 wa masomo ya Sanaa, Lugha na Biashara na walimu 8,516 wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Shule za Sekondari za juu yaani *A-level* zilikuwa na upungufu wa jumla ya walimu 1,104 wakiwemo walimu 710 wa masomo ya Sanaa, Lugha na Biashara na walimu 394 wa masomo ya Hisabati na Sayansi. Wilaya ya Liwale ilikuwa na upungufu wa jumla ya walimu 91 wakiwemo 40 wa Sanaa na Lugha na 51 wa Hisabati na Sayansi.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu, Wizara yangu hivi sasa inao Mpango Kabambe wa upatikanaji wa walimu wa kutosha ifikapo mwaka 2010. Mpango unaainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa za muda mfupi na za muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa:-

(i)Kuajiri kwa mkataba walimu wastaa fu kufundisha katika shule zilizopo kwenye maeneo yao;

(ii)Kuajiri Wataalam wenyе Shahada zisizo za Ualimu kwa kuwapatia Leseni za kufundisha;

(iii)Kuajiri walimu wote wenyе sifa ambao hawajaajiriwa; na

(iv)Kuongeza nafasi katika Vyuo vilivyopo ili viweze kuongeza idadi ya wanachuo kutoka 4,000 sasa hadi 9,000.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la kutoa motisha maalum kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu linagusa wafanyakazi katika Sekta mbalimbali, hivyo inahitaji kushirikisha Wizara nyingi zaidi. Wizara yanguinaweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za walimu na kuboresha mazingira ya shule zilizopo ili kupunguza ugumu wa mazingira ya kazi kwa walimu.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza, kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna upungufu wa walimu wapatao 91; na kwa hivi sasa kiasi gani kwa *percentage* walimu ambao wamekuwa *assigned* kwenda katika shule zile za Liwale ambazo tunahitaji sana walimu kutokana na upungufu wa walimu katika Wilaya yetu?

Pili, mpaka hivi sasa walimu waliopo katika Wilaya ya Liwale wapatao 45 walikuwa na madai yao ambayo yanahu uhamisho, matibabu na gharama zingine. Wiki moja iliyopita walimu waliolipwa ni 11 tu na walimu 34 hawajalipwa kwa sababu ambazo kusema kweli siyo za msingi. Walimu hao 34 waliobaki watalipwa lini haki zao, na kwa nini tunaendelea kuwanyanya wa walimu kwa kiasi hicho? **NAIBU**

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, suala la *percentage* ya walimu nafikiri linaweza likapatikana katika kukokotoa kulingana na hiyo idadi niliyotoa. Kwa hiyo, tunaweza baadaye tukakokotoa na Mheshimiwa Mbunge pale nje.

Mheshimiwa Spika, swal la pili, kuhusu walimu ambao hawajalipwa aliowazungumza idadi yake siikumbuki. Lakini hili suala la malipo linategemea mwalimu mmoja mmoja husika kulingana na matatizo yake mwenyewe. Kwa sababu inawezekana hao ambao hawajalipwa hawana viambatanisho vinavyothibitisha kwamba wana madai yanayohusika. Lakini Wizara kwa wale ambao wameleta viambatanisho na wameleta madai halali wameanza kulipwa na wanaendelea kulipwa na fedha zimeishatumwa kunakohusika. Kwa hiyo, naomba kwa wale ambao hawajalipwa matatizo yao wayalete Wizarani, na kwa kupitia Wakuu wao wa shule tujue matatizo yanayowasibu na ambayo yamesababisha hawajalipwa hadi sasa. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri swal moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule zetu zina tofauti kubwa sana katika nchi yetu, tofauti katika idadi ya walimu, ikama na tofauti katika vitabu, majengo na huduma mbalimbali na bahati mbaya sana mtihani kwa Kidato cha Nne unaotungwa na Kidato cha Sita ni mmoja tu kuweza kupimwa uelewa sawa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba huo mtihani ni batili kwa sababu hauwatendei haki watu wengine?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ni mwalimu na anajua kwamba hakuna mtihani batili. Utungaji wa mtihani mchakato wake ni wa kidemokrasia unatumia *panel*. Kwa hiyo, hakuna mtihani ambao ni batili.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye hata hivyo, kwamba mazingira ya shule zetu ni tofauti. Lakini tunafikiri kwamba popote pale shule ilipo kwa kuwa mtaala wetu ni mmoja kinachotakiwa ni kuhimiza walimu wale wafundishe ule mtaala ipasavyo, walimu wahudhurie vipindi vyote na itakapokuwa imefanyika hivyo kwa kweli mtihani utakaotungwa utakuwa unalingana na silabasi na wanafunzi wote wana haki sawa ya kufaulu mtihani huo. (*Makofi*)

Na. 177

Hitaji la Kutumia Jeshi la Ulinzi

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Kwa kuwa, hali ya Usalama wa Raia na mali zao inazidi kutia mashaka kutokana na wimbi la ujambazi unaotokea mara kwa mara katika maeneo ya Itigi na Mgandu; na

kwa kuwa, Jeshi la Polisi limekiri kuwa linakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi na nyenzo za kazi:-

Je, kwa nini Serikali isitumie Jeshi la Ulinzi (*TPDF*) kukabiliana na majambazi hao hadi hapo Jeshi la Polisi litakapotatua matatizo ya upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi badala ya watu kuendelea kuishi kwa kuhofia maisha yao na mali zao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Tanzania limeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi sura ya 322 R.E. 2002. Majukumu ya msingi ya Jeshi la Polisi yameainishwa katika kifungu cha 5 cha Sheria hiyo kuwa ni kulinda amani, kusimamia sheria na utulivu nchini, kuzuia na kupeleleza makosa ya jinai na kulinda maisha na mali za wananchi. Majukumu yote hayo yanaweza kujumuishwa kwa maneno kuzuia na kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu wa vitendea kazi na uchache wa askari, Jeshi la Polisi bado lina uwezo mkubwa wa kukabiliana na uhalifu wa aina zote hapa nchini na lipo kisheria kwa kazi hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza uwezo wa Jeshi la Polisi katika kupambana na uhalifu wa aina zote.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uhalifu hapa nchini, Jeshi la Polisi pia limeanzisha mpango wa Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi ili kuwashirikisha wananchi na wadau wengine katika shughuli za ulinzi na usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, matukio ya uhalifu yanayotokea katika maeneo ya Itigi na Mgandu na maeneo mengine ya nchi yetu yamekuwa yanadhibitiwa ipasavyo na Jeshi la Polisi. Mafanikio ya Operesheni za hivi karibuni Wilayani Manyoni ni ushahidi wa maelezo yangu juu ya uwezo wa Jeshi letu la Polisi kupambana na uhalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wote wa Wilaya ya Manyoni, akiwemo na Mbunge wao na Mkoa wa Singida kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Jeshi la Polisi katika kukabiliana na uhalifu.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wananchi wa Mgandu walijitolea wakajenga Kituo cha Polisi pale Mitungi na kwa kuwa mpaka sasa kituo hicho hakijafunguliwa kwa sababu ya ukosefu wa *armoury*. Je, ni lini Serikali itatimiza ngwe yake kwa upande huu?

(b) Mapema mwaka huu kikosi maalum cha askari 6 ilifanya operesheni kali kwenye mapori kati ya Kitalaka na Mgandu na kufanikiwa kuliua jambazi kiranja sugu sana. Je, Serikali imewatunuku nini hawa askari 6?

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi katika eneo la Mitungi ni kweli tuna taarifa na ujenzi huo na ni jambo ambalo tunalifanyia kazi katika mpangilio wa Bajeti yetu.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine ni kwamba tuna maombi mengi kutoka kote nchini na kila Mbunge anatoka katika kila sehemu pawe kuna kituo cha Polisi. Kwa kweli jitihada inafanyika lakini kutokana na ufinyu wa hali ya fedha ambayo tunakabiliana nayo siwezi nikatoa hadi kusema lini tutafanya.

Lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kwamba suala lake tunalizingatia kama mengine na Serikali itajitahidi kadri Bajeti itakavyoruhusu kuhakikisha kwamba wananchi wa eneo la Mitungi wanatengenezewa kituo chao cha Polisi.

Kuhusu operesheni iliyofanyika katika maeneo kati ya Kitalaka na Mgandu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli operesheni ilifana sana kutokana na Aaskari wenyewe. Lakini pia kutokana na ushirikiano mkubwa ambao tuliuopata kutoka kwa wenyeji. Sasa kuhusu ni zawadi gani ambao wamepewa hawa Askari kwa kweli tunazo taratibu ambazo tunazifanya ambazo ni za ndani na nadhani kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wangweza wakaelewa kwamba zipo taratibu ambazo zinafanyika ambazo ni za ndani ya utaratibu kufuatana na ile *discipline* ya chombo chenyewe. Lakini kwa kweli heshima wanapata na tunu wanapata kutokana na kazi zao ambazo wamezifanya. Ningependa nijibu hivyo tu Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza.

Kabla sijaauliza swali langu la nyongeza, naomba kutoa shukrani zangu. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunteua kuwa Mbunge. Pia, namshukuru sana Mheshimiwa Spika na Wabunge wote mliomo ndani ya Bunge hili kwa kunipa ushirikiano mkubwa tangu nimefika hapa Bungeni. (*Makofi*)

Bado kidogo nina shukrani zingine naomba niongeze shukrani na pia bila ya kusahau Chama changu cha Mapinduzi. Mwisho kabisa namshukuru mpPENDWA mume wangu kwa kunipa moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye swali langu la nyongeza. Kwa kuwa siku hizi tunalo tatizo kubwa la maalbino, hili tatizo lenyewe ni la kishirikina, tatizo kubwa limejitokeza hivi sasa. Swali lina sehemu mbili.

SPIKA: Moja tu.

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR: Siruhuswi sehemu mbili. Naiomba Serikali ieleze Bunge hili hatua gani inachukua kuzuia kitendo hiki kiovu cha maalbino kuuawa, kuchinjwa, kutolewa utumbo na mambo mengine maovu yanatendeka kwa maalbino. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze. (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama mnnavyofahamu Serikali imekwisha chukua hatua na imetamka kwa nguvu sana ikilaani vitendo hivyo.

Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania amelizungumzia hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu amelizungumzia kwa nguvu zote, Inspeksa Jenerali wa Polisi pia na ye ye amelizungumzia kwa nguvu zote.

Kwa hiyo unaona kabisa kwamba uongozi mzima katika Taifa letu kwa kweli umechukua *position* kubwa sana na ya nguvu katika ku-*condemn* mambo kama haya ambayo yanafanyika kwa ndugu zetu wa maalbino.

Hatua ambazo zimechukuliwa mpaka sasa na bado hatua zinachukuliwa mtahafamu kwamba kuna Tume Maalum ambayo imewekwa ambayo inatizama juu ya undani wa suala hili. Lakini pia kuna elimu ambayo inatolewa kwa wananchi wetu na kwa watu wetu na kuwaeleza na kujaribu kuwafundisha na kujaribu kuona kwamba hawa ni wenzetu, hawa ni ndugu zetu na hawa ni watu kama sisi. Kwa hiyo, hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naweza kusema katika kujibu swali hili ni kwamba hili si jambo zuri katika Taifa letu na bila ya kujirudia ni kwamba Serikali imechukua msimamo na kuna Kamati Maalum ambayo imewekwa ambayo inatizama suala hili na tukishamaliza katika kulitizama na kutazama njia gani ambazo tutafanya. Lakini pia hatua za mpito zinachukuliwa kuhakikisha kwamba matendo kama haya yanadhibitiwa na hayaendelei katika nchi. Lakini ningependa nichukue nafasi hii niseme kwamba hivi ni vitendo ambavyo Serikali inavishutumu kwa nguvu zote kabisa. Ahsante sana.

MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza linalohusiana na wasiwasi wa wananchi kukabiliwa na ujambazi.

Kwa kuwa wavuvi wa Wilaya ya Ukerewe na visiwa vilivyomo katika Ziwa Victoria wamekuwa na mapambano makali na majambazi yanayodhoofisha shughuli za uvuvi ambazo zinaleta pesa za kigeni katika nchi hii.

Kwa kuwa inaelekea kwamba juhudzi za Polisi zimezidiwa hasa kwa kutokuwa na vifaa vya kukabiliana na majambazi majini. Je, Waziri atahakikishaje kwamba wavuvi hawa wanalindwa na mbinu maalum zinatumika katika kuhakikisha usalama wao wanapokuwa kazini katika uvuvi?

NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli tunazo taarifa kuhusu matatizo ambayo yanawakabili wavuvi katika maeneo ya Ukerewe. Lakini ningependa niliambie Bunge lako Tukufu kwamba hili ni tatizo ambalo linakabili maeneo mengi katika nchi yetu. Lakini hii sio kwa sababu tuseme kwamba Jeshi la Askari limezidiwa. Jeshi la Askari ni kwamba linakabiliana na mbinu mpya, linakabiliana na wahalifu wapya ni kwa sababu ambazo ziko na nje ya uwezo wakati mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano lakini napenda nilieleze hili tuweze kuelewana vizuri ni kwamba yako matatizo ambayo yanatokea nchi jirani na unapata watu wengi wanakimbia kutoka nchi zao wanakuja kwa wingi kutokana na matatizo ambayo wanakuwa nayo katika nchi zao jirani.

Kusema kwamba Jeshi la Polisi limezidiwa kwa kweli si kweli. Jitihada zinafanyika ni kwa sababu matendo ya uhalifu yamezidi kutokana kama nilivyosema na matatizo ambayo yanatokana na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba ilitokea si muda mrefu kulikuwa kuna wimbi la kuvunja Mabenki, wizi katika *Mabureau de change* na kadhalika. Waliopambana na wahalifu hao na wengi walikuwa wanatoka nje ya nchi lilikuwa ni Jeshi letu la Polisi na sasa ukitazama katika eneo hilo limekuwa ni shwari.

Kwa hiyo, napenda nichukue fursa hii kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe Mheshimiwa Balozi Dr. Mongella kwamba jitihada zinafanyika na Serikali inalifahamu hilo na tutajitahidi kadri ya uwezo wetu na kadri Bajeti itakavyoruhusu kuhakikisha kwamba tunapambana na hali ya uhalifu.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi awali kwamba jukumu kubwa la Jeshi la Polisi ni ulinzi na usalama wa nchi yetu, raia wetu na mali zao. Ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana kabisa kwamba Jeshi la Polisi halijashindwa kushughulikia masuala mbalimbali yanayotokea yanayohusu uvuvi katika sehemu mbalimbali kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Lakini pia ningependa niongezee kwamba kwa mujibu wa Sheria Na. 22 ya Mwaka 2003, fungu Na. 18 linahamasisha wavuvi waliomo katika Ziwa Victoria na Maziwa mengine mbalimbali kuunda vikundi vinavyoitwa *Beach Management Unit* na kwa bahati nzuri katika Ziwa Victoria zaidi ya *Beach Management Unit* 507 zimeshaundwa zikiwepo zingine katika Visiwa vya Ukerewe na Ukara. Ningombaa hizi *Beach Management Unit* vitumike vizuri katika kushirikiana na Polisi na Serikali kwa ujumla katika kuzungumzia ujambazi unaofanyika katika Maziwa yetu. (*Makofî*)

SPIKA: Nashukuru sana kwa jibu hilo la ziada limetupa mwanga zaidi kuhusu ulinzi katika maeneo ya maji. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Magufuli.

Na. 178

Onyesho la “Big Brother Africa”

MHE. ALI AMEIR MOHAMED aliuliza:-

Kwa kuwa onyesho la shindano linaloitwa “*The Big Brother Africa*” limekuwa maarufu sana baada ya kijana wa Kitanzania kuwa mshindi wa kwanza mwaka 2007:-

- (a) Je, zaidi ya zawadi ya fedha nini hasa lengo la onyesho au shindano hilo?
- (b) Je, Serikali imeridhika na lengo hilo hasa katika kuudumisha utamaduni na heshima ya vijana wa Afrika?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zaidi ya zawadi fedha zilizotolewa katika onyesho au shindano la “*The Big Brother Africa*” lengo lake kuu ni kuonyesha jinsi watu wanavyoweza kuishi pamoja bila kujali tofauti walizo nazo hasa kwa kuzingatia utamaduni wa Kiafrika.

Aidha, mbunifu wa Shindano hilo alikusudia kubaini kama vijana kutoka Mataifa mbalimbali wanaweza kuishi pamoja kwa kuunganisha tamaduni zao.

Mheshimiwa Spika, kila mshiriki katika shindano hilo alilazimika kubuni mtindo wa maisha atakaoweza kuishi katika jumba hilo kwa siku 98 walilokuwa wamekaa. Mtindo huo wa maisha ultakiwa ukubalike na jamii zote duniani. Wale wote waliokuwa wanaangalia kwenye luninga jinsi washiriki walivyokuwa wanaishi ndani ya jumba hilo, waliwapigia kura wale ambaa mtindo wao wa maisha waliyokuwa wanaishi unakubalika na jamii nyingine duniani. Washiriki ambaa mtindo wao wa maisha waliokuwa wanaishi ndani ya jumba hilo haukukubalika na jamii nyingine hawakupigiwa kura za kuendelea kuwepo na hivyo kutolewa katika mashindano.

Mheshimiwa Spika, kuishi katika jumba hilo ambalo washiriki waliwekwa ulihitaji uvumilivu wa hali ya juu, upendo, uelewano, ushirikiano na kukubali hali ya wengine. Katika mazingira kama hayo mshiriki wetu wa Tanzania Richard aliweza kuonyesha hayo yote na kupigiwa kura nyingi zilizomfanya aibuke kuwa mshindi. Aidha, mshiriki wetu alikiri kwamba katika kipindi chote alichoishi katika jumba hilo

amejifunza mengi yatakayomwezesha kuishi na watu wenye mtazamo tofauti. Hivyo basi kufuatia ushindi alioupata kijana wa Kitanzania nchi yetu imepata sifa kubwa kwa kuzingatia madhumuni ya shindano hilo. Serikali imeridhika na lengo la shindano hilo hasa katika kuudumisha utamaduni wetu na heshima ya vijana wa Afrika kwa ujumla kwa kuonyesha uvumilivu, upendo, uelewano, ushirikiano na pia kukubali hali ya wengine. (*Makofî*)

MHE. ALI AMEIR MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na kweli lazima nieleze mshtuko wangu kwa majibu ya Naibu Waziri. Sina hakika kama Naibu Waziri alikuwa analiangalia onyesho hili. Hivi kweli Serikali yetu inawahimiza vijana wetu kushiriki katika hali ile ya maisha na ikiamini kwamba wanaendeleza utamaduni wa Tanzania. Je, Waziri anajua kwamba hata mshiriki wetu alikaribia kuvunja ndoa yake kutokana na shindano lile?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nilitaka niwe muwazi kabisa kwamba katika dunia ya leo ni utandawazi, hakuna ambacho kinafichika Mheshimiwa Spika.

Lile shindano ni shindano kama nilivyoeleza unatakiwa uwe uvumilivu, uwe na upendo, uwe na ushirikiano ni ujasiri. Iko michezo mingi ule ni mmoja wa mchezo katika dunia na duniani humu kuna michezo mingi kweli. Kwa hiyo, ninachotaka kusema kwamba kuwa na utamaduni uliovunjwa ni Shindano la Kimataifa la Dunia nzima lengo linajulikana. Lakini yako masuala leo ukifungua *internet* unaweza kuona zaidi ya yale.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba tunaishi katika dunia ya utandawazi ambayo hakuna kificho katika dunia ya leo, dunia ni kijiji. (*Makofî*)

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa sababu Tanzania tumejapata kijana kama huyu mvumilivu kwa nini sasa tusimtumie tukamwekea kipindi cha nusu saa kupita katika Vyuo Vikuu kuwaelimisha vijana wenzake pale sasa hivi?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Hawa washindi wa mashindano kama haya mshindi wa *Big Brother Africa*, *Miss Tanzania*, *Miss Utalii* tunawatumia katika shughuli mbalimbali. Shughuli za kijamii kama vile unavyoona leo hii mshindi wa tatu wa *Big Brother* yupo hapa Tanzania Tatiana yupo Arusha ni *model* anaonyesha mavazi. Kwa hiyo, wazo la Mheshimiwa Nyawazwa nalikubali kwamba *Big Brother* wa kwetu sisi ambao ameshinda Richard yeye ameamua kuendelea na masomo *University* lakini ame-plan baada ya kumaliza tuweze tukamtumia na yeye akafanya kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Huduma za Mirathi Kusogezwa Mikoani

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Kwa kuwa, imeonekana kuwa kuna ugumu wa taratibu zilizopo za Pensheni na mirathi kwa familia za watumishi waliofariki wakiwa kazini, hasa wale wanaotoka vijijini na kwenye Wilaya za pembezoni kama ya Namtumbo:-

Je, Serikali haioni kuwa, ni vyema kutengeneza utaratibu wa kusogezwa huduma hiyo Mikoani kupitia “*Sub-Treasury*”?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Vita Kawawa kwa kuhakikisha kwamba matatizo ya wananchi wa jimbo lake la Namtumbo anayowakilisha katika Bunge hili. Pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni vyema kwa Serikali kutengeneza utaratibu wa kusogezwa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma hii ya pensheni na mirathi karibu na wananchi, kwa manufaa ya watu wetu.

Aidha, wakati nikijibu suala Na. 134 la Mheshimiwa Ussi Ame Pandu mnamo tarehe 22/4/2008 katika Bunge lako Tukufu, nilieleza utaratibu utakaotumika wa kuwalipa wastaafu pensheni zao kupitia akaunti zao kuanzia Julai, 2008. Utaratibu huo umeandaliwa ili kuwaondoshea wastaafu usumbufu unaowapata pamoja na kuwasogezea karibu wastaafu huduma hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mirathi, kuanzia Julai, 2000 malipo yote yanayoambatana na mirathi hulipwa kupitia Mahakama iliyofunguliwa kesi ya Mirathi kwa kushirikiana na Mahakama ilikofunguliwa mirathi. Wizara ya Fedha huandaa malipo ya mirathi na baadaye Mahakama ukabidhiwa hundi za malipo kupitia Hazina Ndogo ilioko Mkoani kwa ajili ya kuwakabidhi wahusika. Kwa utaratibu huu, ni dhahiri kwamba huduma hizi sasa ziko karibu na wananchi, kwani ndugu wa marehemu hufungua kesi za mirathi karibu na Mahakama iliyo karibu na wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni haki ya mtumishi kupata haki zake baada ya utumishi wake, Serikali itaendelea na juhudzi za kusogezwa huduma mbalimbali karibu na wananchi na kila itakapoonekana kuwa utaratibu uliopo hauridhishi basi tutawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuandaa utaratibu mwengine utakaokuwa mzuri zaidi. (*Makofi*)

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niseme kwamba kwa kuwa zoezi hili la mpaka kupata mirathi na pensheni ni *process* ambayo ina urasimu wake tena ni mrefu.

Je, katika zoezi hili la kupata hiyo mirathi Serikali iko tayari kuwa na Ofisa mmoja kati ya walio katika Ofisi ya DC kuwa *coordinator* wa madai ya mirathi na *responsible* wa kuhakikisha wadai wanapata haki yao haraka na inavyostahili kuliko ilivyo hivi sasa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Kawawa ni zuri lakini kwa hivi sasa utaratibu ambao umewekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ni kwamba wanafamilia wanapaswa kufungua kesi ya mirathi katika Mahakama iliyoko karibu na baadaye kabla ya kufungua kesi ya mirathi wanapaswa kuandaa kikao cha wanafamilia ambacho kinateua msimamizi wa mirathi na baadae kufungua kupitia katika Mahakama.

Sasa ukianzisha utaratibu mwingine kwamba Wilayani kuwe kuna Ofisa atakayefuatilia nadhani tutakuwa tunakiuka utaratibu ambao umewekwa kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Spika, namwomba astahimili kwanza ili tuweze kuona utaratibu huu unavyokwenda. La msingi ni kwamba wanafamilia wanapaswa kuwa na vielezo vyao karibu zaidi ili waweze kuharakisha huu ufunguzi wa kesi na kuweza kupata hayo mafao yao kwa haraka zaidi.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili ni zaidi ya tatizo la habari (*information*). Na kwa kuwa Serikali siku hizi inajivunia kwamba imefungua utaratibu wa *E-Government*, Serikali ambayo unaweza kuipata kwenye tovuti.

Kwa nini Serikali isianzishe utaratibu angalau wa kuweka habari juu ya watu wanaodai mirathi yao katika tovuti au mahali ambapo watu wanaweza kupata hiyo habari wajue tu wamefikia wapi halafu ikifika Mahakamani watakwenda Mahakamani.

Sasa watu wanasafiri kutoka kijijini kuja Dar es Salaam, kwa hiyo naomba majibu juu ya hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, wazo lake ni zuri la kuweka taarifa katika mtandao. Lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Cheyo huko vijijini hii mitandao bado haijafika. Hata ukiweka wananchi wa vijijini si rahisi kuweza kupata hizo taarifa.

Nadhani la msingi ni kujaribu kutumia vyombo vyetu vya habari ambavyo vinasikika vijijini kama redio na magazeti ili wananchi wetu wakawenza kuona na kusikia kwa wale ambao mirathi yao iko tayari. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini kama kumbukumbu yangu iko sahihi wakati Waziri Mkuu akiahirisha Bunge la mwaka la bajeti alituomba Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli ni wajibu wetu kuwasaidia hawa watu wanaodai pensheni huko vijijini katika kuwashughulikia.

Lakini utaratibu ule ni mrefu na ni mtindo wa kizamani kwa sababu mafaili na mambo yote hayako katika kompyuta, kwa hiyo ni mafaili yanayotembea. Lakini bado Wabunge tunapokwenda pale hakuna *special care* kwamba sisi ni Wabunge na ni viongozi tunastahili heshima katika kushughulikia masuala yale. Kwa hiyo, unafika pale utaratibu si mzuri unakaa kwenye foleni.

Je, hawaoni kwamba kuna haja basi ili tuweze kusaidiana katika jambo hili watuwekee utaratibu mzuri pale Pensheni, Hazina ili Wabunge tukifika tukae au tusubiri kwa utaratibu unaoelewaka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE): Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wake na tutakaporejea baada ya kumaliza kwa Bunge hili tutaandaa utaratibu mzuri ili Waheshimiwa Wabunge watakapokuja pale Hazina waweze kuelewa nini cha kufanya na wasipoteze muda ili tumalizane nao waweze kuendelea na kufanya shughuli zao.

Na. 180

Mkataba wa Uuzaji wa Kiwanda cha Baiskeli

MHE MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. BAKAR SHAMIS FAKI) aliuliza:-

Kwa kuwa, baiskeli ni nyenzo muhimu kwa wananchi hususan wale wa kipato cha chini; na kwa kuwa, Kiwanda cha Baiskeli kimeuzwa na sasa kinatengeneza na kuza vigae vyta sakafu na kuta badala ya baiskeli:-

(a) Je, mkataba wa kuza kiwanda hicho uliridhia biashara ya vigae badala ya baiskeli?

(b) Kama mkataba haukuelekeza hivyo. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kazi za kiwanda hicho kwa sasa?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mkataba wa kuuza kiwanda cha baiskeli cha *NABICO* 1997, kwa Kampuni ya *Ivon Cycles* ya India haukuridhia kiwanda hicho kiuze vigae bali kiendelee na uzalishaji wa baiskeli isipokuwa pale itakapothibitika kibiashara kwamba haiwezekani. Kutokana na hasara kubwa iliyokikumba kiwanda hicho, mnunuzi wa awali yaani kampuni ya *Ivon Cycles* aliamua kukiiza kwa *Mohamed Enterprises (T) Ltd.* mwaka 2003 kwa masharti hayo hayo waendelee kutengeneza baiskeli. Baadaye *Mohamed Enterprises (T) Ltd.* iliamua kukihamishia kiwanda hicho Kiwalani na kuuza jengo lililokuwa la kiwanda cha *NABICO* pale Mwenge.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kiwanda cha baiskeli kinaendelea na jukumu la kuzalisha baiskeli katika eneo la Kiwalani ambako kiwanda kimehamishiwa na kampuni ya *Mohamed Enterprises (T) Ltd.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, kwa nia yake njema ya kupenda kuona kuwa wananchi wote hawa wa vipato wa kawaida wanapata nyenzo za usafiri ikiwemo baiskeli.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa uzalishaji katika kiwanda tajwa umepungua mno na katika kukabiliana na upungufu huo baadhi ya wananchi wanaagizia baiskeli *used* na kuingiza nchini ambazo zinapendwa sana na ni madhubuti lakini wanakwanzwa na ushuru mkubwa. Je, Serikali ipo tayari kupunguza ushuru huo ili kufanya baiskeli hizo ziuzwe kwa bei nafuu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, baada ya kampuni ya *Ivon Cycles* pamoja na kampuni ya *Mohamed Enterprises* kuanza kazi ya kutengeneza baiskeli serikali iliweka ushuru ili kuzuia uingizaji mkubwa wa baiskeli kutoka nje kuwezesha viwanda hivi viweze kuuza hapa nchini. Lakini tulipoingia katika Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki ushuru huu umeondolewa likiwa ni azimio lililokubaliwa chini ya itifaki ya Umoja wa Ushuru wa Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, hivi sasa huo ushuru ambao Mheshimiwa Mbunge anasema ni kwamba umeondolewa ili kuwafanya wananchi wa Afrika Mashariki pamoja na Tanzania waweze kupata baiskeli kwa bei ambayo ni nzuri. Lakini vilevile Serikali yetu inaongea na Wizara ya Fedha na uchumi kwa kuona kama kuna uwezekano wa kumwondolea *Mohamed Enterprises* tozo la VAT ili aweze kuuza baiskeli hizo vilevile kwa bei ambayo kila mwananchi anaweza akaipata. Kwa hiyo, sasa hivi tunangojea majibu kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi na endepo Wizara hiyo itakubali pendekezo la Wizara yangu, basi baiskeli zitapatikana kwa bei ambayo ni nzuri.

Na. 181

Chombo cha Kusimamia Biashara ya Ndani

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kuunda Baraza la Mawaziri mwezi Februari, 2008 Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa, kutakuwepo na chombo kitakachosimamia masuala ya biashara ya ndani:-

- (a) Je, chombo hicho kimeshaundwa?
- (b) Kama kimeundwa. Je, kina muundo gani?
- (c)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiunda Baraza jipya la Mawaziri mwezi Februari, 2008, Wizara imeandaa mapendekezo ya muundo wa Idara zake ili kujipanga vema katika kushughulikia kwa karibu masuala yanayohusu biashara ya ndani. Mapendekezo hayo yamewasilishwa katika ngazi za Serikali zinazojadili Miundo ya Wizara na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ipo katika mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria Na. 5 ya 1978 ilioanzisha Halmashauri ya Biashara ya Nje (*Board of External Trade – BET*) na pia kuifuta Sheria aya Bodi ya Biashara ya Ndani Na. 15 ya mwaka 1973 ili kuunda Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*Tanzania Trade Development Authority – TANTRADE*). Lengo ni kuwa Mamlaka hii itakayoundwa iwe na jukumu la kusimamia na kukuza biashara katika soko la ndani na nje kulingana na sera za uchumi-jumla na za kisekta kwa kuzingatia mabadiliko yaliyopo katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mhagama kwani hii si mara yake ya kwanza kuuliza maswali yanayohisiana na biashara ya ndani na hasa masuala ya bei kwa wananchi wa Jimbo lake la Peramiho. Hata hivyo napenda kumwomba Mheshimiwa Mhagama pamoja na Wabunge wote wavute subira ili tufikie azma ya kuuda chombo hicho.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa azma ya Mheshimiwa Rais alipotamka uundwaji wa chombo hicho ilikuwa hasa ni kusimamia suala zima la biashara ya ndani ya nchi yetu ya Tanzania ambalo limekuwa sasa hivi likienda kwa namna fulani holela holela.

Je, Mheshimiwa Waziri kwa Mamlaka yake ya kumshauri Mheshimiwa Rais, yupo tayari kuhusisha chombo hicho pia na usimamizi wa bei ambazo zimekuwa zikipanda na kushuka bila kuwa na mpangilio na hasa kwa kutumia mfumo huo wa soko huria?

Swali la pili, kwa kuwa imekuwa sasa ni desturi ya wafanyabiashara kujichukulia mamlaka ya uzalishaji wa bidhaa na upangaji wa bei na hivyo basi wananchi wengi na wanyonge wanaoishi kule vijijiini wamekuwa wakiathirika sana na mfumo huo katika nchi yetu ya Tanzania. Je, Mheshimiwa Waziri anaelewa sasa ni wakati muafaka haya yote yakashughulikiwa katika mchakato huo mzima wa kutunga sheria mpya na kuwa na chombo kama *EWURA* katika masuala hayo ya biashara?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuyajibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Jenista Mhagama ambayo yanaulizia kuhusu suala la usimamizi wa bei pamoja na uundaji wa chombo hicho cha kusimamia biashara ya ndani hapa nchini. Kama nilivyosema mchakato wa kuunda *TANTRADE* ambacho ni chombo kitakachoangalia masuala yote ya biashara ya nje na ndani bado unaendelea. Kwa hiyo, mchakato huo tutakavyoona umuhimu wake Mheshimiwa Waziri wangu nafikiri atapata nafasi nzuri ya kumshauri Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba chombo hicho kitakapoundwa basi matatizo yote ambayo yanatokana na wafanyabiashara kuongeza bei kiholela yanashughulikia.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kukubaliana naye kwamba tatizo la wafanyabiashara kuongeza bei kiholela kuzalisha bidhaa wanavyotaka ni tatizo ambalo linamgusa kila Mtanzania na ni tatizo ambalo Wizara yangu italiangalia kwa makini kabisa ili chombo hiki kitakapoundwa tuhakikishe kwamba hakuna mfanyabiashara ambaye atakuwa juu ya Sheria.

Na. 182

Kuitangaza Mbuga ya Selous

MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA aliuliza:-

Kwa kuwa Mbuga ya Hifadhi ya Selous ni hazina kubwa ya dunia na kwa sababu hiyo watalii wengi sana wanakwenda kufanya utalii kwenye mbuga hiyo.

(a) Je, ni lini Serikali itaipa Mbuga hiyo hadhi ya juu kwa kuitangaza ndani na nje ya nchi?

(b) Je, ni lini Serikali itaamua kujenga miundombinu bora ndani ya hifadhi hiyo ya barabara za kuifikia mbuga hiyo kama ilivyo kwa mbuga za Kaskazini ya Tanzania ili wawezeshaji waweze kujenga hoteli bora na kuinua biashara ya utalii kwenye maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Pori la akiba la Selous lilitangazwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) mwezi Machi, 1982 kuwa urithi wa dunia (*World Heritage Site*). Hatua hii ilikuwa muhimu na imelifanya eneo hilo liwe katika hadhi ya juu na kuiweka Tanzania kuwa mojawapo ya nchi zenyenye maeneo maarufu na yenye umuhimu wa kipekee duniani.

Mheshimiwa Spika mikakati ya kukuza na kutangaza vivutio kwenye pori la Akiba *Selous* ndani na nje ya nchi ni kwa kuwaruhusu wanafunzi kutembelea pamoja na ushiriki wa Wizara katika maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) yanayofanyika kila mwaka katika viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere. Pia Bodi ya Utalii Tanzania hutangaza vivutio vya pori la *Selous* kuititia majarida ya *Tantravel, Selling Tanzania* na *Tanzania the Land of Kilimanjaro and Zanzibar* ambalo linatolewa kwa lugha saba (7) ambazo ni Kichina, Kiingereza, Kijapan, Kifaransa, Kitaliano, Kijerumani na Kispanishi. Aidha, maelezo ya vivutio vya *Selous* na maeneo mengine hupatikana kwenye mtandao wa Bodi ya Utalii Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, Wazira imetengeneza barabara zenyenye urefu wa kilomita 1,000 pamoja na kununua mitambo ya ujenzi wa barabara. Uimarishaji wa barabara zinazoingia kwenye Pori la *Selous*, ni jukumu la Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROAD*) na Halmashauri za Wilaya husika. Hata hivyo kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hizi kwa shughuli za utalii Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Miundimbinu na Halmashauri za Wilaya husika katika kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, *Selous* ni kubwa sana zaidi ya nchi ya Switzerland. Pori hilo kuna upoteaji wa mali, njia za panya ni nyingi sana, watu hubeba meno ya tembo katika balskeli kichwani na unaweza kuiba meno ya tembo Malinyi ukakamatwa Songea. Je, Serikali ina mpango gani madhubuti ya kulinda upotevu huu wa mali asili katika pori la *Selous*.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli pori hili ni kubwa sana lakini Wizara yangu imekuwa ikiimarisha miundombinu iliyoko katika Hifadhi yenyewe katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kwa mfano tumeongeza idadi ya wafanyakazi kwenye pori hilo kufikia 300 pamoja na kwamba haifiki kiwango ambacho kinakidhi mahitaji na pia kujenga nyumba za wafanyakazi kwenye pori lenyewe kwa sasa tumejenga nyumba mia moja za kisasa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kwa hivyo wafanyakazi wananyumba nzuri za kuishi lakini pia maeneo ambayo yanazunguka pori hili tumekuwa tukishirikiana nayo kwa kutumia huu ulinzi wa mipango Shirikishi tunaposhirikiana na wananchi wa maeneo hayo.

Lakini pia tumekuwa tukiimarisha barabara kama nilivyosema zinazoingia na kutoka kwenye eneo hili ili iwe rahisi kwa askari wetu pamoja na vyombo vingine vya dora kuweza kufanya doria kwa hivi uimarishaji wa ulinzi. Kwa hiyo, uimarishaji wa doria utaendelea kufanyika. (*Makofit*)

Mpango wa Kuunganisha Umeme Vibaoni - Chanika

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa kuunganisha umeme kati ya Kijiji cha Vibaoni – Chanika hadi Kwachaga – Turiani tayari uko mikononi mwa Serikali toka mwaka 2005.

Je, ni lini utekelezaji wa mradi huu utaanza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADIN I alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Mradi wa kuunganisha umeme kati ya kijiji cha Vibaoni – Chanika na Kwachanga – Turiani umeorodheshwa na Wizara yangu kwa lengo la kuutafutia fedha kutoka katika vyanzo vya ndani na nje ya nchi ili uweze kutekelezwa. Shughuli za awali za utekelezaji wa mradi huo zilizokwishafanyika ni upembuzi yakinifu uliofanywa na *TANESCO* ambaao ulibaini kuwa kazi zinazohitajika kufanyika ni pamoja na ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 25; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 0.4 umbali wa kilomita 6 pamoja na ujenzi wa vituo 3 vya kupozwa umeme. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 zitahitajika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ukamishaji wa ujenzi huo. Mara baada ya fedha kupatikana utekelezaji wa mradi huo utaendelea. Tunawashauri wananchi wa maeneo ya Kwachanga Turiani kuwa na subira wakati Serikali ikifanya jitihada za kupatikana fedha za kutekeleza mradi wa kuunganishia umeme kutoka Vibaoni – Chanika hadi Turiani.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja dogo la nyongeza. Je, mradi huu unawenza kutekelezwa kwa awamu kwa kuanzia Chanika – Vibaoni mpaka Magamba na baadaye mkatafuta hela mkamalizia kipande kilichobaki?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Tayari tulishaanza kuzingatia kwamba shilingi bilioni 1.1 kwa mradi wa moja kwa moja ni kiasi kikubwa na hivyo tuliwasiliana na namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge alifika ofisini na tayari tumeanza kufanya tathimini ya kuugawa huu mradi kwa awamu mbili. Yaani kuanzia Vibaoni hadi Magamba na awamu ya pili Magamba hadi Kwachaga. Lakini kwa kuwa tathmini hii hajakamilika naomba tuendelee kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tutakapopata makisio kamili ya mradi huu tuangalie kama tunaweza tukaupatia utekelezaji kwa awamu gani na kwa muda gani.

MHE. RAMADHAN A. MANENO aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mpango wa kuitengeneza barabara ya kutuka Bagamoyo – Kiwanga –Msata kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa mradi wa kuvuta maji kutoka Mto Wami –Chalinze unatarajiwa pia kufikishwa Kiwangwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Kiwangwa ili uweze kuwasaidia wajasiriamali katika usindikaji wa matunda kama mananasi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme hadi kijiji cha Kiwangwa kama ilivyo kwa vijiji vingine nchini, utatekelezwa chini ya Wakala wa Nishati Vijijini ambayo imepewa majukumu ya kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi na za umma kutoa huduma za nishati bora kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini. Mfuko wa Nishati Vijiji utatumika kutoa ruzuku kwa wawekezaji wenyewe sifa watakaowekeza kwenye miradi ya Nishati Vijiji kiushindani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya jitihada za kutafuta fedha kutoka katika vyanzo vya ndani na nje ya nchi ili kuweza kuutunisha mfuko huo uweze kutoa ruzuku kwa wawekezaji wengi kwa lengo la kufikisha umeme katika maeneo mengi ya vijijini. Tunawashauri wananchi wa Kiwanga kuwa na subira wakati Serikali ikitekeleza mipango yake hiyo.

MHE. RAMADHAN A. MANENO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa suala la umeme ni kichocheo cha wananchi hata wale wa Kiwangwa ambao ni walimaji wakubwa wa zao la mananasi. Je, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba wataalam wake hawakumpa majibu sahihi ya swali langu?

Swali la pili. Je, Naibu Waziri upo tayari kwenda Kiwangwa kuniwekea sawa jambo hili kwani naona Serikali inasababu ya kunipunguzia kura zangu?

SPIKA: Mheshimiwa Maneno Uchaguzi bado. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa barabara ya Msata, Kiwangwa hadi Bagamoyo kunahitaji kubadilisha kwa kiasi kikubwa hali ya uchumi na kijamii ya maisha ya wananchi watakaopitiwa na barabara hii haswa kwa wenyewe magari yenye uzito stahili na itapunguza umbali wa safari baina ya Dar es Salaam na Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha kwa kupitia Bagamoyo na Kiwangwa badala ya Mlandizi na Chalinze.

Mheshimiwa Spika, tumeshawasiliana na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Pwani kwamba tunatambua hasara kubwa inayosababishwa na ukosefu wa masoko au viwanda vya usindikaji ambao kusema kweli unazuia kupanuka au kuongeza uzalishaji wa matunda Kiwangwa na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani na Mikoa ya jirani. Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amezungumzia lengo la wajasiliamali wadogo

tumeshawasiliana na wana nia ya kuwekeza kwenye mashine lakini wanashindwa kufanya hivyo kwa sababu ya kukosekana kwa umeme ndiyo maana nimemwomba kwamba tuipe jukumu hili Wizara yangu kwa kuwasiliana na wakala wa nishati vijijini ili tuangalie namna ya kufanya ili miradi ambayo inalengwa kuwekezwa kwa kuwapatia ujira na kuongeza maslahi mapana ya kiuchumi kijijini hapo yasipotee. Naomba tuendelee kuwasiliala na namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatalia suala hili kwa makini.

Na. 185

Uanzishwaji wa SACCOS – Muleba Kaskazini

MHE. RUTH B. MSAFIRI aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini ni mionganoni mwa wananchi walioitikia wito wa kuanzisha *SACCOS*:-

- (a) Je, ni *SACCOS* ngapi zimepata mkopo wa Benki kutokana na shilingi bilioni moja kila Mkoa zilizotolewa na Mheshimiwa Rais?
- (b) Je, Serikali inashirikiana na wananchi kwa kiasi gani katika kuanzisha na kuboresha *SACCOS* hizo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika awamu ya kwanza ya utoaji wa mikopo kutoka Mfuko wa Uwezeshaji ulioanzishwa na Mheshimiwa Rais, Mkoa wa Kagera ulipata mikopo yenye thamani ya shilingi shilingi 429 milioni. Mikopo hii iliwanufaisha wajasiliamali 492 hadi kipindi kilichoishia Februari, 2008 kuititia *SACCOS* 6 zifuatazo: *Karagwe Women SACCOS*, *Nkwerwa SACCOS* ya Karagwe, *Chikanya SACCOS* ya Karagwe, *Biharamulo Women SACCOS*, *Bukoba Women SACCOS*, *Mviwaru SACCOS* ya Bukoba Mjini.

Aidha katika Wilaya ya Muleba *SACCOS* 5 zilizoomba mikopo kuititia Benki ya CRDB lakini hazikuweza kupatiwa mikopo hiyo kutokana na kutotimiza vigezo vilivyowekwa. *SACCOS* hizo ni Muleba Women *SACCOS*, *Nshamba SACCOS*, *Umoja SACCOS*, Tegeka na *Tujipaki SACCOS*.

(b) Mheshimiwa Spika, uanzishaji na uboreshaji wa *SACCOS* nchini umezingatia mpango shirikishi ndani ya Programu kabambe ya mageuzi na modenaizesheni ya Ushirika. Chini ya utaratibu huu, wananchi kuititia Asasi mbalimbali za kijamii,

mashirika yasiyo ya kiserikali, wanasiasa wakiwemo Wabunge na Idara za Serikali, zimeshiriki sana kuwahamasisha wananchi kuunda, kujiunga na kumiliki *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikiwa kama msimamizi wa Sera na Sheria ya Vyama vya Ushirika nchini, inathamini sana mchango mkubwa wa wadau hawa. Napenda kutoa rai kwa wadau wote kwamba juhudhi hizo ziendelee ndiyo njia sahihi na endelevu ya kumkomboa mwananchi.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza katika jibu la swali langu amekiri kwamba *SACCOS* tano toka Wilaya ya Muleba ikiwemo *SACCOS* maarufu ya Tujipaki ambayo ni ya Jimbo la Muleba Kaskazini hazikupata mikopo kwa sababu hazikukidhi viwango. *SACCOS* kubwa kama hii haiweza kukidhi viwango Serikali itanithibitishia kwamba sasa itafanya juhudhi za makusudi za kutoa elimu na kufuatilia kuhakikisha kwamba kipindi kijacho cha awamu ya pili ya mikopo wa JK tunaoutarajia kuja *SACCOS* kubwa kama Tujipake zitaweza kupata mikopo?

Swali la pili, kwa kuwa *center* maarufu za Jimbo la Muleba Kaskazini ikiwemo *center* ya Muhutwe, Izigo na Kwamachumu kwa kuzitaja chache wanajishughulisha na kazi ya kulima mananasi na kutengeneza baisedeli, redio pamoja na pikipiki kwa maana ya wajasiliamli wadogo ambao hawajaendelezwa.

Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kuwasaidia vijana hawa ili kuhakikisha kwamba katika mikopo unaokuja na wenyewe wanasaidiwa kupata mikopo huo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba ni jukumu pia la Serikali kutoa elimu kwa wananchi wanaojiunga na *SACCOS* pamoja na *SACCOS* ambazo zimeshaanzishwa tayari. Serikali ipo tayari kutoa elimu hiyo ili wananchi hawa na *SACCOS* ambazo zimeanzishwa waweze kutimiza masharti waweze kupatiwa mikopo.

Lakini niseme kwamba hata kama elimu itatolewa lakini kama *SACCOS* inamtaji mdogo *SACCOS* ni mpya haijanza kutoa mikopo maana lazima *SACCOS* lazima iwe imeshaanza kutoa mikopo na iwe inatunza mahesabu vizuri na iwe na viongozi waaminifu wanafahamika na wanafahamu elimu ya *SACCOS* kuendeshwa kwa kibashara na iwe na utunzaji wa kumbukumbu mzuri.

Sasa wakishatimiza vigezo hivi hapo ndipo wanapoweza kupatiwa mikopo na Benki ya *CRDB* hata awamu ya pili itakapofika.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni lile lile la kujiunga kwenye *SACCOS* na kuwa na *SACCOS* yenye sifa ambazo nimezitaja na sisi tutawasaidia waweze kupata mikopo.

Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Farkwa

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia tafiti zake iliwahi kupendekeza ujenzi wa Bwawa la Farkwa katika Bonde la Mtu Bubu Wilayani Kondoa kwa lengo la kuanzishia mradi mkubwa wa umwagiliaji katika bonde hilo, na kwa kuwa mahitaji ya mradi huu ni dhahiri hivi sasa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza mradi huo ili kuwaondolea wananchi wa Dodoma umaskini uliokithiri?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mawazo ya kuwa na mradi wa ujenzi wa Bwawa kubwa la Farkwa kwenye Mto Bubu yalianza mwanzoni mwa miaka ya 1950 na baadaye mradi ukajumuishwa katika mpango wa kuendeleza Mkoa wa Dodoma.

Mwaka 1983 programu ya uwiano wa maendeleo ya Mkao wa Dodoma (*RIDEP*) ilifanya upembusi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Farkwa.

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya mradi huo yalikuwa kutoa umeme wa maegawati 10 na kilimo cha umwagiliaji maji mashambani hekta 10,000.

Mheshimiwa Spika, upembusi yakinifu uliokamilishwa na Wahandisi Washauri, Kampuni ya Ujerumani ya *Agrar – Und Hydrotechnic GMBH*, Oktoba, 1985 ulikaridia kuwa mradi mzima ungegharimu shilingi bilioni 5.547.

Serikali ilifanya juhudini kutafuta Wafadhili wa kusaidia ujenzi wa mradi huo ikiwa ni pamoja na *UNDP, FAO* na Serikali ya Ujerumani bila mafanikio. Hivi sasa gharama za ujenzi wa mradi ulipopendekezwa zimeongezeka na zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 595.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mahitaji ya mradi huu bado ni sahihi kwa maendeleo ya wananchi wa Mkao wa Dodoma. Hata hivyo, kwa kuwa mji wa Dodoma umekwisha unganishwa na gridi ya Taifa ya Umeme, iko haya ya kurejea ripoti za upembusi yakinifu zilizofanywa huko nyuma na kuainisha vipaumbele vya sasa.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kondoa itafanya tathmini ya mradi wa bwawa la Farkwa na kuangalia uwezekano wa kuutekeleza kwa awamu kupitia Program zetu mbili za kuendeleza Sekta ya Maji na Program ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo ambayo takribani 75% ya fedha zake zinaelekezwa kwenye kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mradi huu umekuwa na gharama kubwa kutokana na kwamba kulikuwa na lengo la kuzalisha umeme pia kulikuwa na lengo la kuleta maji kwa mji Mkuu wa Dodoma na pia umwagiliaji ndiyo maana gharama imekuwa kubwa. Na kwa kuwa sasa tungelenga katika mradi mmoja. Je, haoni kwamba sasa Wizara ifanye uchambuzi haraka ili kuweza kubaini gharama halisi za umwagiliji? Kwa kuwa mradi huu utanufaisha Wilaya tatu; Kondoa, Bahi na Manyoni.

Je, Waziri haoni kwamba anatakiwa ashirikishe Wilaya zote tatu badala ya Wilaya moja tu ya Kondoa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi, mimi sasa nashauri kwamba Wizara yangu, wataalam wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya zote za Mkoa huu wa Dodoma na wadau wengine katika kipindi hiki kuelekea mwaka wa fedha ujao, tufanye mchakato kwa pamoja ili kubaini vipaumbele viliyobaki. Kipaumbele cha maji ya kunywa hivi sasa, hatutakiweka kwa sababu Mji wa Dodoma sasa unapata maji kutoka *Makutopora Basin*.

Umeme kama nilivyosema, tayari Dodoma imeunganishwa kwenye gridi ya taifa. Kwa hiyo, iliyobaki sasa ni kuangalia tunawezaje kuupunguza huu mradi halafu tuangalie uwezekano pia wa kutekeleza kwa awamu. Kwa hiyo, nakubali kwamba tutakaa wote wadau kuangalia tunawezaje kuupunguza na kuutekeleza kwa awamu.

Na. 187

Miradi ya Maji - Mikumi

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA aliuliza:-

Kwa kuwa miradi ya maji safi na salama katika jimbo la Mikumi, Wilayani Kilosa kwa vijihi vya Tundu, Iwemba, Kifinga, Msowero, Lumango, Zombo – Lumbo iliyo chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia pamoja na ile ya ufadhili wa *African Development Bank* kwa Kata ya Ruhembe imechelewa sana kutekelezwa hali inayoleta adha kubwa kiafya na kiuchumi kwa jamii:-

(a)Kwa kuwa michango ya wanavijiji imekamilika. Je, wafadhaili walengwa wa miradi hii wamekwishatoa fedha kiasi gani na hatua gani zaidi zinatakiwa kuchukuliwa ili utekelezaji uweze kuanza haraka iwezekanavyo?

(b)Je, mpango kazi wa miradi hiyo imekadirwa kukamilika baada ya muda gani tangu utekelezaji utakapoanza kama hakutatokea vikwazo vikubwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal i Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2007, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilipewa shilingi 153,990,000 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa miradi hiyo uko katika hatua mbali mbali.

Vijiji vya Tundu, Iwemba, Kifinga, Msowero, Lumango na Zombo – Lumbo vipo katika awamu ya kwanza ya vijiji 10 vya utekelezaji wa Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambayo inatekelezwa katika Halmashauri zote nchini. Hivi sasa anatafutwa Mtaalam Mshauri atakayefanya kazi za uhamasishaji, usanifu na usimamiaji wa miradi. Mtaalam Mshauri anatarajiwa kupatikana ifikapo mwezi Julai, 2008 tayari kuanza kazi katika kipindi cha mwaka 2008/2009.

(b)Mheshimiwa Spika, mipango kazi ya miradi ya awamu ya kwanza imekadiriwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu tangu ujezni utakapoanza.

Hata hivyo, utekelezaji utategemea kasi na uwezo wa Halmashauri ya Kilosa. Kama Halmashauri itamaliza ujenzi wa miradi hiyo mapema, itaruhusiwa kuendelea na ujenzi katika vijiji vingine ambavyo vitakuwa vimechaguliwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lyamba pamoja na wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa kutoa michango yao iliyopangwa katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa, napenda kuuliza. Je, Serikali iko tayari kwa kutumia teknolojia ya kisasa kufanya *survey* za upatikanaji wa maji ardhini katika Wilaya zote nchini ili kuharakisha kasi ya Halmashauri ya kuweza kutafuta fedha au kupata wafadhili wa kuchimba visima vya maji na kuongeza kasi ya upatikanaji maji licha ya hii miradi ambayo wafadhili wametusaidia?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuwapatia wananchi wote waishio vijijini na mijini. Vijijini kwa asilimia 60 na asilimia 65 katika vijiji ifikapo 2010. Sasa, ujenzi au uchimbaji wa visima ni mbinu mojawapo ya kutafuta maji. Wakati mwingine maji haya hayapatikani katika ardhi, tunatafuta njia zingine ikiwa ni pamoja na uvunaji wa maji yaliyoko juu ya ardhi.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kufanya utafiti mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuangalia jinsi tunavyoweza kupata maji chini ya ardhi katika Wilaya hiyo ya Kilosa.

Kuvisaidia Vituo Vidogo vya Afya

MHE. ENG. LAUS O. MHINA aliuliza:-

Kwa kuwa, ili kituo cha afya kiwe na sifa kamili ni lazima walau kuwe na sehemu ya wagonjwa (*O.P.D*), chumba cha upasuaji mdogo, maabara, chumba cha kuhifadhi maiti pamoja na wataalam wenye sifa:-

- (a) Je, Serikali itasaidiaje kuvipatia huduma muhimu vituo vya afya kama vya Magoma na Bungu kwa kuzingatia kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe haina uwezo kifedha kuvipatia vituo hivyo huduma kama hizo?
- (b) Je, ni lini Serikali italeta mtaalam wa maabara mwenye sifa katika kituo cha Magoma kwani mtaalam wa maabara pekee aliyekuwepo yuko kwenye masomo ya muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ili kituo cha afya kiwe na sifa kamili za kutoa huduma kinatakiwa walau kiwe na sehemu ya wagonjwa wa nje, chumba cha upasuaji mdogo, maabara, chumba cha kufulia, chumba cha maiti pamoja na wataalam wenye sifa.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imekuwa ikivisaidia vituo vyote vya kutolea huduma vikiwemo vituo vya afya vya Magoma na Bungu kwa kuvipatia fedha za kuijendesha (*O.C*), fedha za maendeleo pamoja na mishahara. Aidha, kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Serikali hutoa dawa na vifaa tiba. Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikianana Halmashauri yake kuweka mipango ya uboreshaji wa vituo vya afya vya Magoma na Bungu pamoja na vituo vingine vya kutolea huduma katika bajeti yao.

(b)Kwa mujibu wa mwongozo wa utoaji huduma za afya nchini, madaktari wanatakiwa kutoa huduma katika hospitali za Wilaya, Mikoa, Rufaa na Hospitali Maalum za tiba. Vituo vya afya na zahanati huhudumiwa na Maafisa Tabibu (*Clinical Officers*), Wauguzi (*Nurses*) na Wahudumu wa afya (*Medical Attendants*). Hata hivyo katika mpango wa kuboresha utoaji wa huduma nchini, Sertikali imeanza kuwapangia Madaktari Wasaidizi kwenda kufanya kazi katika vituo vya afya ili kusaidia huduma za upasuaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kuwasiliana na Halmashauri yake ili kuhakikisha kuwa nafasi zote za watumishi wa afya ambazo ziko wazi kwa mujibu wa ikama zitatengewa fedha katika makisio ya Bajeti ya mishahar ya

watumishi na baadaye kuombewa kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Wizara yangu itasaidia upatikanaji wa watumishi husika kwa mujibu wa kibali kitakachotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, namwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri, kumpeleka Mtaalam katika kituo cha Magoma na sehemu nyingine zenyne upungufu badala ya kuwajaza watumishi Hospitali ya Wilaya kitendo ambacho kitasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya kwa kuwapatia huduma katika maeneo wanakoishi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwishapita. Matangazo:- Naomba tuwatambue wageni kama ifuatavyo:- Kwanza tunao wageni amba ni Maafisa wa Bunge rafiki la Afrika Kusini (*South African Parliament*) Wamekuja hapa kuendelea kubadilishana uzoevu na Maafisa wetu wa hapa Bunge la Tanzania. Kwa hiyo, nitawataja mmoja mmoja; Wanaongozwa na Bwana Ntuthuzelo Vanara ambaye ndiye kiongozi wa Msafara, Bi. Koleka Beja, Bi. Refilwe Mathabathe na Bi. Sinomtha Mbuge. *Welcome to the Tanzanian Parliament. We are very very happy to receive brothers and sisters from the Republic of South Africa. You know, Tanzania and South Africa have a very long and cordial association. So it is always a pleasure to have brothers and sisters from South Africa. We wish you well! I apologize if I have not pronounced names quite as they are supposed to be pronounced, but you can imagine, it is a different culture. Thanks very much and enjoy your stay and our regards home when you travel back. (Makofi)*

Mheshimiwa Christopher Chizza, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ameniomba nitangaze mgeni wake ambaye ni Binti yake, Gloria Chizza. Ahsante sana Gloria, tunakutakia heri. Nasikia unamaliza kidato cha sita mwaka huu na *combination* yako ni CBG. Kweli, mtoto wa nyoka naye ni nyoka! Masomo magumu sana hayo! Hongera sana, tunakutakia mafanikio hadi Ph.D. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, anawaomba wajumbe wote mkutane kwa kikao kifupi sana mara baada ya kuahirisha Bunge leo katika ukumbi namba 133. Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ameniomba nitangaze kuwa Kamati ya Nishati na Madini wanatakiwa wakutane leo tarehe 25 Aprili, 2008 katika ukumbi namba 231 jengo la utawala mara baada ya kuahirishwa Bunge. Madhumuni ni kukamilisha ratiba ya kazi za Kamati kabla ya mkutano wa kumi na mibili. Mtaona tumegawa orodha ya nyongeza ya shughuli, hii ni kwa sababu jana mimi nilikubali ombi la Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kutoa ufanuzi wa swali au suala alilokerwa Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa. Kwa hiyo, tumetoa nafasi hiyo kwa wakati muafaka basi utatolewa. Pengine ni wakati mzuri pia niseme tu kwamba katika orodha ya Miswada ambayo ilikuwa isomwe mara ya kwanza, tumebaini kwamba ipo Miswada ambayo haikukidhi taratibu za Kanuni kwa sababu haikutimiza siku 21. Kwa hiyo, imebidi hiyo tuiache, nayo ni *The Animal Welfare Bill, 2008, The Public Heath Bill, 2008, The Workers Compensation Bill, 2008* na *The Public Audit Bill, 2008*. Sasa ni hivi, ingawa Miswada hii haikutimiza kile kipindi cha siku 21, lakini kwa kuwa imemfikia Katibu, Kanuni hazikatazi Waheshimiwa Wabunge kugawiwa hiyo Miswada.

Itasomwa mara ya kwanza katika Mkutano ujao. lakini mtagawiwa sasa, mwende nayo nyumbani na inawezekana mmoja au miwili kati ya hii hasa huu wa *Public Audit Bill*, ukatakiwa kupita hatua zote. Kwa hiyo, ndiyo maana mnagawiwa sasa, mpate fursa ya kusoma. Kanuni haikatazi hilo, lakini kwa kuwa siku 21 hazijapita toka kuchapishwa, hatuwezi kuweka mezani hivi leo. Badala yake ni ile ile ambayo mnaiona katika Orodha ya Shughuli za Leo.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo mwisho wa matangazo, ningeomba Katibu atusomee shughuli inayofuata.

KAULI ZA MAWAZIRI

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa maelezo kuhusu barua iliyowasilishwa kwako na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu na kunakiliwa kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, kuhusiana na kutoridhika kwake na majibu ya swali Na. 56 lililojibwa na Wizara yangu tarehe 1 Februari, 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa urahisi wa rejea, napenda kunukuu swalii la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kama alivyoliuliza siku hiyo. Nanukuu: “Kwa kuwa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya Tarehe 30 Juni, 2005/2006 inaonyesha kuwa Tanzania imezuiliwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni mbili (2) kutoka kwenye Mfuko wa *Debt Conversion Scheme* ulioko Benki Kuu kwa sababu waliochukua fedha kutoka kwenye Mfuko huo, hawajazirejesha:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?
- (b) Kama jibu kwenye sehemu ya (a) ni ndiyo. Je, waliochukua fedha hizo ni akina nani kwa majina na ni kiasi gani cha fedha kila mmoja alichochukua?
- (c) Je, hadi Disemba, 2007 ni wangapi kati yao wamelipa na ni kiasi gani kila mmoja amelipa na iwapo hawajalipa Serikali imechukua hatua gani ili Taifa lisiendelee kupoteza manufaa ya mfuko huo kwa ajili ya watu wachache?“ Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya swali hili Na. 56 tarehe 1 Februari, 2008, nilisema yafuatayo, na ninanukuu: “Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006 haioneshi popote kuwa Tanzania imezuiliwa kutumia zaidi ya shilingi bilioni mbili (2) kutoka kwenye Mfuko wa *Debt Conversion Scheme*, ulioko Benki Kuu ya Tanzania kwa sababu waliochukua fedha kwenye mfuko huo hawajarejesha”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, jibu hilo ni sahihi hadi leo, kwa kuwa Tanzania haijawahi wala haikuzuiliwa kutumia fedha zilizotajwa katika swalii la Mheshimiwa Dr. Slaa.

Aidha, jibu la kwamba Programu ya *Debt Conversion* haipo, wakati wa kujibu swali, nalo ni sahihi hadi leo. Hata hivyo, napenda kutoa maelezo ya ziada ili Mheshimiwa Mbunge aweze kupata majibu ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa kutohana na Tanzania kukabiliwa na uhaba wa fedha za kigeni mwishoni mwa mwaka 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990, palitokea limbikizo kubwa la malipo ya madeni ya nje ikiwepo mikopo ya bidhaa ambazo zililetwa nchini kwa njia ya mikopo ya biashara ya muda mfupi (*Suppliers Credits*). Serikali ilianzisha mpango wa *Debt Conversion Programme (DCP)* kama njia mojawapo ya kupunguza malimbikizo ya malipo hayo. Madhumuni kamili ya mpango huu yalikuwa haya yafuatayo:-

Moja; kuvutia uwekezaji katika sekta za kipaumbele ambazo ni pamoja na kilimo, utalii, viwanda na usafirishaji. Pili; kupunguza malimbikizo ya madeni ya nje. Mpango huu uliana kutumika mwaka 1990 na ulisitishwa. Narudia, ulisitishwa mwaka 1994 baada ya kuonekana kwamba unachangia katika kuongeza mfumko wa bei (*inflation*). Mpango mbadala wa kupunguza madeni hayo, uliofadhliliwa na Benki ya Dunia uliojulikana kwa jina la *Debt Buy Back Scheme*, ulianzishwa.

Wakati mpango wa *Debt Conversion* unasitishwa, nchi iliweza kupunguza madeni yenye thamani ya dola za kimarekani 182,000,000 na fedha zilizotolewa na Serikali kulipia madeni haya zililipwa kwa shilingi ya Tanzania na miradi ipatayo 82 ilitekelezwa na makampuni yaliyokuwa yameruhusiwa kununua madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *Debt Conversion Programme* ulikuwa na masharti kwa wawekezaji ili kuhakikisha kwamba madhumuni ya mpango huo yanatimizwa.

Kwa mfano, kabla ya kupewa ruhusa ya kununua deni, mwekezaji alitakiwa kuwa na mradi kwenye sekta ya kipaumbele na baada ya kununua deni kutoka kwa mdai (*Creditor*) mwekezaji huyo alilipwa kwa awamu kulingana na jinsi anavyotekeleza masharti. Fedha zilitunzwa na Benki Kuu kwenye akaunti ya iliyokuwa *Debt Conversion Scheme*.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna bakaa la shilingi 2,069,000,000/= kwenye akaunti ya iliyokuwa *Debt Cenversion Scheme* iliyoko Benki Kuu. Bakaa hili liko katika mafungu mawili. Moja lina shilingi 965,000,000/= zikiwa fedha halali za wawekezaji zilizozuiliwa na Benki Kuu kwa kuwa wahusika hawajatimiza masharti ya kuendeleza miradi na lingine la shilingi 1,104,000,000/= zikiwa ni fedha zilizowekwa na Makampuni ambayo madeni yake nje ya nchi yalilipwa na Benki ya Duni chini ya utaratibu wa ununuzi wa madeni wa *Debt Buy Back* uliofadhliliwa na Benki ya Dunia.

Napenda kusitiza kuwa Tanzania haijawahi kuzuiliwa wala hajazuiliwa kutumia fedha zilizoko kwenye akaunti ya iliyokuwa *Debt Conversion Programme*. Aidha, hakuna mwekezaji aliyekopa kutoka kwenye akaunti hiyo na hivyo kuhitajika kurejesha deni. Ukweli ni kwamba kuna bakaa linalostahili kulipwa kwa wawekezaji wanaohusika

pindi watakapotimiza masharti. Hata hivyo, kwa kuwa wawekezaji husika hawakutimiza masharti ya kuendeleza miradi yao, pesa hizo bado zinashikiliwa na Benki Kuu. Ni vizuri ikumbukwe kuwa wawekezaji hawa walitoa fedha zao kununua deni kutoka kwa wadai katika fedha za kigeni na hivyo kulipunguzia Taifa mzigo wa madeni. Aidha, bakaa ya shilingi 1,104,000,000/= iliyoko kwenye akaunti ya iliyokuwa *Debt Conversion Scheme* ni fedha za Serikali ambazo zitatumika baadaye kulingana na maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwishoni mwa Desemba, 2007, orodha ya makampuni ambayo yanastahili kulipwa bakaa ya shilingi 965,000,000/= yatakapotimiza masharti. Narudia, yatakapotimiza masharti, siyo Serikali itakapotimiza masharti, ni haya yafuatayo:- Kwanza, *Kibo Match Cooperation* – shilingi milioni 9.3, *Aqua Teller Project* – shilingi milioni 63.7, Arusha Farms – shilingi milioni 71.2, *Commercial and Industrial Combine* – shilingi milioni 262.5, *Integio Tanzania Limited* shilingi milioni 28.9, Kiwange Sisal Estate – shilingi milioni 67.3, *Leisure Holding Tanzania Limited* – shilingi milioni 331, *Makinyumbi Tea Estate Limited* – shilingi milioni 77.4, *Sunrise Kilimanjaro Limited* – Shilingi milioni 14.8, *TanFarms Limited* – shilingi milioni 38.7, *Tanpech Limited* – shilingi 200,000/=, Jumla shilingi milioni 965. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, endapo wawekezaji hawataendeleza miradi yao kulingana na masharti yaliyowekwa, fedha hizo zitaendelea kuzuiliwa kwenye akaunti ya iliyokuwa *Debt Conversion Scheme* iliyoko Benki Kuu. Kwa hiyo, kilichopo kwenye ile *Audit Report* ni Benki Kuu ndiyo imezuia fedha za wawekezaji ambao hawakutimiza masharti na siyo Benki ya Dunia au *IMF* au nchi yoyote imeizuia Tanzania. Tanzania haijazuiliwa na mtu yejote yule kukopa pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya ni wazi kuwa hapakuwa na nia au kusudio au lengo lolote la kupotoshwa kwa makusudi hoja ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu na Serikali kwa ujumla wake, hawakulidanganya Bunge wakati wa kujibu swali Na. 56 mwezi Februari mwaka huu 2008. (*Makofi*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria Kwa ajili ya Kutoa Huduma Bora, Kulinda na Kufuatilia Haki za Watu wenye Ugonjwa wa Akili, Kutoa huduma ya Kulazwa kwa Hiari katika sehemu ya Kutolea huduma ya Wagonjwa wa Akili pamoja na Mambo yanayohusiana nayo (A Bill for an Act to Provide for the Care, Protection and Management of Persons with Mental Disorders and to Provide for their Voluntary or Involuntary Admission in Mental Health Care Facility and Other Related Matters)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga sheria mpya itakayosimamia Uzalishaji, Usindikaji na Biashara ya Ngozi na mambo yanayohusiana nayo (A Bill for an Act to

(Develop and Regulate the Production and Reservation of Hides, Skins and Leather and to Promote Trade in Hides, Skins and Leather and to Provide for Related Matters)

(Miswada miwili ya Sheria ya Serikali iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Ahsante sana! Miswada hiyo kama mlivyoisikia sasa imesomwa kwa mara ya kwanza Bungeni. Sasa tunaendelea.

HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

Hoja ya Uuzwaji wa Nyumba za Serikali

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpa nguvu Mheshimiwa Kimaro, kwamba nami naunga mkono kwa asilimia mia na kumi, nitaeleza ni kwa nini nimeongeza asilimia kumi ya kumwunga mkono Mheshimiwa Kimaro hapo baadaye.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni takriban miaka mitano sasa toka Serikali ilipofanya uamuzi wa kuziwa nyumba za Serikali ambazo ni nyumba za Wananchi, Serikali inapaswa ijiulize ni kwa nini sasa hata baada ya miaka mitano hili jambo linaonekana bado ni bichi na linawakera wananchi. Ni lazima Serikali ijiulize kuna nini, inawezekana dhamira ya Serikali ilikuwa nzuri lakini utekelezaji wake ulikuwa mbovu sijawahi kuona. Katika mambo ambayo hayatakuja kusahaulika katika historia ya Watanzania ni pamoja na kuuza nyumba za Serikali. Ninayasema haya kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa hii ndiyo mali pekee aliyoutuachia Marehemu Baba wa Taifa na nyumba hizi nyingi zilijengwa wakati wa Ukoloni na zingine zilijengwa awamu ya kwanza ya Serikali yetu. Hizi ni rasilimali yetu, lakini baya kabisa maamuzi haya ya Serikali hayakupitishwa na Bunge letu Tukufu, Bunge ambalo Kikatiba ndilo lenye jukumu la Kikatiba kuisimamia Serikali yetu. Ndiyo lenye jukumu la kulinda maslahi ya wananchi wa Tanzania. Kama ni suala la Utawala Bora kwa nini basi Serikali haikutaka maamuzi haya mazito yanayowagusa wananchi yasipitishwe na kuridhiwa na Bunge?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwa nini nimesema ni maamuzi mabaya, kwa sababu kwanza yanaturudisha kwenye matabaka ya wafanyakazi, nyumba zile 7,921 waliofaidi ni wakubwa, ni kada za juu ndiyo walifaidi, kati ya wafanyakazi takribani laki mbili na nusu ya wakati huo ni wafanyakazi 8,000 tu ambao walifaidika na nyumba hizi, huku ni kujenga matabaka. Wakubwa hawa ndiyo wenye magari, wakubwa hawa ndiyo wenye ofisi zenye viyoyozi, wakubwa ndiyo wanatembelea magari yenye bendera

zinazowaambia wananchi pisha apite. Wanyonge wanaouumia madarasani na vumbi la chaki hata nyumba yenze chumba kimoja hawakufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, wanyonge askari wetu wanaotulinda usiku na mchana wanalala kwenye suti za mabati, jua linapiga Dodoma hii, hata huruma ya kusema tunaamua kuuziana nyumba za *Railway* zilizo nyingi basi angalau hawa Askari wetu ambao ukipita pale utawaonea huruma wanalala kwenye suti hakuna mtu aliyekuwa analiona hili. Huu ni unyang'anyi na uporaji wa mali za umma, hatuwezi kuvumilia hali ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kada ya kati ni watu wangapi walifaidika na nyumba hii, kada ya chini ni watu wangapi walifaidika na nyumba hizi, tunatakiwa tujenge mazingira ya kutomwonea na kumpendelea mtu, zoezi zima la uuzaaji wa nyumba za Serikali lilikuwa la upendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza kwa masikitiko kwa sababu nimekutana na watu ambao wameumia kwa sababu ya zoezi hili. Wapo watumishi ambao ilibidi waandaliwe uhamisho ili kuachia ile nyumba, lakini tumewatesa sana watumishi. Mimi ninao mfano kule Mbeya kwa kiongozi wangu Mwandamizi wa Mahakama, amehama karibu hoteli zote za Mbeya Mjini, amefikia Mount Livingstone akaambiwa Serikali imeshindwa kulipa pesa akahamia Mbeya Peak, amekaa huko akahamishwa tena kwa sababu nyumba aliyostahili kufikia na huyu alikuwa ni Kiongozi Mwandamizi wa Mahakama. Mtu ambaye tunampeleka pale kulinda haki ya wananchi tunamwacha anatangatanga kwenye mahoteli kana kwamba hana mwenyewe, mpaka anajuta kwa nini alikwenda kusoma.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake kiongozi huyu wa Mahakama inabidi nimfuate na kumpooza alipofikia hatua ya hoteli ya tatu mpaka wakati huo na gharama ya mtu mmoja ilikuwa ni shilingi milioni 41 kwa kipindi chote alichohangaika kwenye hizo hoteli.

Mheshimiwa Spika, tujiilize Wabunge ni Watanzania au watumishi wangapi walihamishwa kwa mtindo huo na walitumia kiasi gani fedha za wananchi, unaenda hospitali hakuna dawa, barabara zetu zimejaa mashimo lakini fedha zinatumika bila sababu hatuwezi kukubaliana hii nchi ni ya kwetu sote siyo ya watu wachache tu. Nataka hili lieleweke wazi na wenye dhamana ya nchi hii ni wananchi wanyonge wadogo ambao ndiyo wanaotuleta Bungeni. Tusifike mahali tukawafikisha mahali ambapo watakuwa wanunung'unika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kubwa na baya zaidi ni uuzaaji na wa nyumba za Halmashauri. Mimi ninazungumza kwa sababu nilipokuwa Meya wa Jiji la Mbeya nilihamasisha Madiwani tujenge nyumba kwa ajili ya Mkurugenzi wetu na Mtunza Hazina. Madiwani hawa hawajahusishwa na kushirikishwa na nyumba walizozijenga zimeuzwa na Serikali. Matokeo yake anakuja Mkurugenzi anahangaika hana mahali pa kulala anahama kama popo. Mji utaachaje kuwa mchafu namna hiyo, wakati yeye

mwenyewe hana *peace of mind*, atatekelezaje majukumu. Ndugu zangu wapendwa katika jina la Bwana mlifikia hata kuuza ah? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Bwana ndiyo nani sasa?

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Naomba Serikali irudishe nyumba za Halmashauri, nyumba za Halmashauri zilijengwa na Waheshimiwa Madiwani na kwa unyonge wao, tunaomba Serikali kama katika mtindo huo zile ambazo ni za Halmashauri *passé* zirudishwe mikononi mwa Halmashauri. Naomba sana katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo wananchi wanasikitika nyumba hizi pamoja na kusema zilikuwa za zamani kama mnavyoziita. Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Hapa tuko kwenye kikao tunajadili kumhoji baba mdogo ameuza nyumba ya urithi, kitu ambacho hakiwezikani.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya nyumba hizi zilikarabatiwa kwa fedha za Serikali, fedha nyingi sana zilitumiwa zilikarabatiwa kwa shilingi milioni 250, lakini ikauzwa kwa shilingi milioni 50. Mbaya zaidi Serikali inaji-*contradict* yenye tunasema ni vyema zaidi maeneo yale ambayo ni *prime arears* palipo na boma pana nyumba ya *DO*, pana nyumba ya Mkuu wa Wilaya na nyumba zingine zote zinazofuata watu hawa wanaunda Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mara nyingi na wakati mwingine wanaitisha vikao hata wakati wa usiku.

Nyumba hizi za karibu na maboma ya Serikali zimeuzwa watu walioingia kwenye nyumba ile hawamjui *DC* wala hawamjui nani wala hawaijui Serikali. Sasa ni nani atakayelinda Boma la Serikali? Sasa tunashangaa nini tunapoona nyaraka za Serikali zinazagaazagaa. “Hawawezi nimekemea”.

Ninaomba niungane na Mheshimiwa Kimaro nyumba zote za Serikali hasa katika ngazi ya Wilaya zirudishwe. (*Makofi*)

Ndugu zangu nasema hivi wale wenzangu wote mliopata nyumba za Serikali mimi sina wivu kwa sababu kwanza sina *interests* ya kuwa na nyumba tatu, nne, tano hazina haja kwangu. Ila nawapa tahadhari tu mjenge na zingine za pembeni, hizi zitakuja rudi ni za wananchi. Ni suala la muda tu, tunajianda sasa tunafanya mazoezi tutakuja huko.

Mheshimiwa Spika, jambo hili wala si geni. Chile walifanya mambo hayo hayo. Nigeria walifanya makosa hayo hayo lakini alipoingia Rais aliyefuatia aliamua maeneo yale ambayo ni nyeti kwa Serikali kuipa heshima Serikali, nyumba zote zilirudishwa. Ila cha msaada tu kama alitoa shilingi milioni tano gharama itafikiriwa. Kwa hali ilivyo sasa hivi arudishiwe na aende akatafute nyumba mahali pengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu mambo haya kama yangepitia Bungeni, pengine haya tunayoshauri yangelikuwa yamefanyiwa kazi na Serikali ikaamua kufanya maamuzi ambayo leo hii baada ya miaka mitano tusingekuwa tunanyoosheana vidole

hana. Hili aliloliletu Mheshimiwa Kimaro na mimi Mheshimiwa Kimaro nakuunga mkono kwa sababu kwanza nimesimama kama Mbunge lakini, pili nimesimama kama kiongozi wa kiroho kama ulivyotoa hoja yako.

Ninaomba tuwatendee haki Watanzania kwa kulinda mali zao. Serikali ijielekeze mtindo mzuri ambao hautakuwa na upendeleo ni kuwafanya wafanyakazi wote, *cadre* ya chini, *cadre* ya kati na ya juu wapewe mikopo isiyokuwa na riba wajenge nyumba sio kuuza nyumba za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukazungumza halafu ukaharibu, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii naunga mkono asilimia mia moja na kumi kwa sababu nataka nyumba za Halmashauri zirudishwe. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mpesa nimenong'onezwa hapa wewe unafahamika kama *Bishop*.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kunipa nafasi niweze kutoa ufanuzi kidogo kwa hoja hii iliyoko mbele yetu ya nyumba za Serikali. Nitangulize kusema kwamba hoja hii naiunga mkono si tu kwa sababu imeagizwa na Bunge lakini ni hoja ambayo inaunga mkono maagizo ya Rais. Kwa hiyo, ni utekelezaji vile vile wa maagizo ya Rais Kikwete. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna haja ya kwenda sana kwenye historia ya suala la kuuza nyumba katika nchi yetu. Lakini niseme tu kwamba, katika Waraka huo wa Serikali wa mwaka 2001 na wala sio wa mwaka 2002 iliamuliwa kwamba nyumba za Serikali ziuzwe kwa wale watumishi na viongozi waliokuwa wanaishi mle ndani. Kwa maana hiyo ni wale tu waliokuwa wanaishi mle ndani na nilitaka nimwambie Mheshimiwa Ndugu yangu *Bishop* kwamba haikuwa na upendeleo. Kama ulikuwa unaishi ndani ya nyumba hiyo hata kama ulikuwa na cheo kidogo, kama kilitokea na watu wachache waliohamishwa ili auziwe mwingine ilikuwa ni kuvunja utaratibu na labda kesi kama hizo zinaweza zikafuatiliwa.

Lakini ni kweli kwamba katika nyumba hizo kulikuwa na viongozi wale wanaostahili kupewa nyumba kwa mujibu wa utumishi wao na wale wafanyakazi wengine kwa sababu nyumba zingine hazikuwa hata na hadhi za kupewa watu au watumishi au viongozi wanaostahili kupewa nyumba. Hii ilikuwa ni kwa sababu Serikali iliona kwamba iwasaidie hawa watumishi wa Serikali ambao wanaishi humo ndani wakati wakiwa bado watumishi na baada ya kustaafuli. Lakini vile vile kuondoa gharama kubwa ambazo zilikuwa zinatumika na Serikali kwa matengenezo na ukarabati. Sasa hili tumeshalisema muda mrefu na maamuzi mengine yalikuwa kwamba fedha zinazopatikana ziwekwe kwenye *revolving fund* ili zitumike kujenga nyumba zingine ukiongeza na bajeti ya Serikali ili kuwezesha sasa watumishi wengine ambao watakuwa wanaajiriwa ambao wanastahili kupewa nyumba na hawana nyumba waweze kupata nyumba na katika kufanya hivyo mpaka sasa nyumba 645 zimeshajengwa na zingine 265 zinaendelea kujengwa. Zilizokwishajengwa shilingi bilioni 29 zimetumika na zinazoendelea kujengwa karibu shilingi bilioni 8.7. Baadaye kwa sababu tumeshapata

maagizo haya tutatoa taarifa kama ambavyo azimio linahitaji. Lakini nitatoa takwimu hapa ambazo ni za haraka haraka tutatoa taarifa kamili baadaye.

Sasa baada ya zoezi hili kuanza limeanza kwenye mwaka 2002 mpaka 2004 kwa sana nyumba zilizouzwa ni zile ambazo tumeshazitaja karibu 7,900 zenye thamani ya shilingi bilioni 59. Lakini kati ya hizi shilingi bilioni 59, karibu shilingi bilioni 32 tumeshakusanya bado shilingi bilioni 27. Lakini hizi shilingi bilioni 27 ambazo bado nitazielezea kwa sababu ieleweke kwamba katika shilingi bilioni 27 nyumba hizi zilikuwa zinauzwa kwa mkataba wa miaka 10 kurudisha. Sasa hivi ni miaka minne au mitano na wengine mitatu toka wanunue. Ina maana bado wana muda wa kurudisha mpaka 2012 mpaka 2014. Lakini nitaelezea mpaka sasa wangapi wame-*default* ambao ni *overdue* walitakiwa wawe wameshalipa mpaka sasa. Sio zile ambazo walitakiwa walipe baadaye mpaka mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, waliokwishalipa wamemaliza kabisa nyumba hizo ni nyumba 2,780 na 5,141 bado wanaendelea kulipa na wengine walilipa haraka. Lakini niseme katika zile nyumba 7,921 nyumba za Serikali yenewe kama *Central Government* zilikuwa 4,904 na za Mashirika ya Umma 2,952. Sasa maamuzi ambayo yalifanyika kwamba sasa baada ya kufanya hivyo tunahakikishaje kwamba wale watumishi na viongozi wa Serikali wanaostahili kuwa na nyumba wanakuwa nazo. Kwa hiyo, maamuzi yakafanyika kwamba sasa nyumba zitengwe na hii imekuja kwa kweli kwenye awamu ya nne. Nyumba zitengwe au zижengwe kwa viongozi na watumishi wote waandamizi wenyе stahili ya kupata nyumba kwa mujibu wa Waraka wa Serikali. Na hao tunawajua Mawaziri, Makatibu Wakuu na zile Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa watu 6 kila Mkoa na watu 6 kila Wilaya, pamoja na Mahakimu, Majaji, Wasajili wa Mahakama, wote hawa tuhakikishe kwamba nyumba zimetengwa kwa ajili yao na ziwe *tied* na zisiuzwe.

Kwa maana nyingine kuanzia sasa nyumba kwa hawa wanaostahili kupewa nyumba zinazojengwa na zinazotengwa kwa ajili yao kwenye Mikoa na kwenye Makao Makuu ya Taifa nyumba hizo hazitauzwa. Zitatengwa, zitajengwa na nitaeleza utaratibu na *thrust* tunayoendelea kujenga. Kwamba hizi zitakuwa *tied quarters*. Katika hizi nyumba ambazo zimeshajengwa kweli kuna zingine ambazo zinastahili kupewa hawa watu kama Mawaziri wameshapata, Makatibu Wakuu wa Mikoa zenyewe zilikuwa zimebaki na zingine zilikuwa zinaendelea kujengwa.

Lakini kuna zile nyumba ndogo ambazo zingine zilijengwa Dodoma ambazo wamepewa watu wengine. Lakini sasa *thrust* ya Serikali kukamilisha zoezi la kupata nyumba zote kwa wale wanaostahili bado nyumba 339 ambazo thamani yake ni kama shilingi bilioni 27.5 hizi sasa ndizo tunaziwekea Bajeti. Nataka nitangaze hapa kuanzia sasa kwa Bajeti ya Serikali na mauzo ya nyumba ya Serikali tutaelekeza nguvu zetu kujenga hizi nyumba 6 kila Wilaya zitimie. Kuna Wilaya zimeshapata mbili, moja na Mikoa zitimie 6 na hao Majaji pamoja Mahakimu na wengine ili zitimie zile ambazo sasa zitakuwa haziuzwi ziko *tied* na mpango huu tukipata fedha kutoka Serikalini ukamilike ndani ya miaka labda mitatu ijayo tuwe tuna hakika sasa tunazo nyumba ambazo wanaostahili kupata nyumba kwa mujibu wa nafasi zao wana nyumba.

Mheshimiwa Spika, huu ndio ufumbuzi, kwa wale wafanyakazi wa Serikali wengine utaratibu kwamba kwenye soko kwenye *private sector* tunakaribisha kwanza tunaanzisha Benki ya Nyumba, kuna Shirika la Nyumba na hata sisi kama *TBA* tuna viwanja tutakaribisha sekta binafsi iingie ijenge nyumba ndogondogo kwa ajili ya kuwauzia kwa mikoa watumishi wengine.

Lakini kwa maana ya Bajeti ya Serikali na hizi fedha tunazouza nyumba zitaelekezwa kuhakikisha kwamba kwanza nyumba hizi 339 zilizobaki zinajengwa nchi nzima baada ya hapo ndio tunaweza kuangalia na sisi tuingie labda kwenye kujenga zingine ndogo kwa ajili ya kuwauzia wafanyakazi wengine. Kwanza lazima tuwamalize hao wanaostahili wawe na nyumba ambazo zitakuwa pale katika Serikali zote zitakazokuja katika kurekebisha hii hali iliyojitekeza.

Mheshimiwa Spika, kuna kasoro zilizojitekeza ambayo sasa tunakuja kwenye hoja. Katika kutekeleza uuzaaji wa nyumba kuna kasoro nne zilizojitekeza kubwa. Kwanza ilikuja kuonekana kwamba nyumba zisizostahili kuuzwa ziliuzwa na ndiyo hayo makambi ambayo wakuu wamesema sana. Sio nyingi lakini zipo. Wasiostahili kuna nyumba zingine ambazo wale walikuwa hawastahili kuuziwa waliuziwa, nazo ziko chache.

Tatu, ambayo amesema vile vile Mheshimiwa Mpesya kuna nyumba za Halmashauri chache ziliuzwa. Nne, ni baadhi ya wale waliouziwa kutotimiza mikataba yao ya kulipia nyumba kwa wakati.

Sasa kasoro hizi ndiyo ikaundwa Tume ya Rais wakisaidiana na sisi Wizara yetu tuweze kubainisha kasoro hizi. Tume ile inaendelea na kazi lakini kila tunapopata taarifa tunachukua hatua zinazostahili.

Kwa mfano mpaka sasa nyumba saba ambazo zimeshaainishwa kwamba zimeuzwa kwenye makambi tumezishaainisha na sasa hivi ni kuomba Serikali zile nyumba tuzirudishe kwa sababu ziko sehemu ambazo kama ambavyo nasema Mkuu wa Kituo amenunua karibu na kituo cha polisi ametoka, ameshastaifu na ameifanya baa. Ssasa baa iko karibu na Kituo cha Polisi na kadhalika. Kwenye Majeshi na kwenye hospitali shule na kadhalika. Hizi saba ni mwanzo tu tutakapokuwa tunaleta taarifa kwa mujibu wa maagizo ya Bunge, tutakuwa tumepata orodha kubwa zaidi na kila tutakapopata tutachukua hatua. (*Makofi*)

Ambao hawakustahili kuuziwa lakini wakauziwa tumeshapata chache kama nne, tatu tumezirudisha, mmoja akawa amekwenda Mahakamani juzi tumemshinda kesi Mahakamani na tutamwondoa kwa nguvu hivi karibuni na tunaendelea kuainisha kama kuna yoyote ambaye anaweza kudhani kuna mtu huyu alikuwa hastahili akatupatia *tip* kwa sababu mwingine ilikuwa ni vigumu hawa walifanya wakati mwingine ni *forgery*. Barua iliyokuja ilionesha kwamba yeche ni mtumishi wa umma kuja kuchunguza kumbe hakuwa mtumishi wa umma.

Hizi za Halmashauri tumegundua mpaka sasa nyumba 14 ambazo ziliuzwa kimakosa na ni za Halmashauri. Mheshimiwa Mpesa amesema hizi nyumba na zenyewe tunaomba sasa Serikali ituruhusu kwa sababu zenyewe ziliuzwa nyingine sio kwamba ziko kwenye maeneo kama yale ya makambi ambao kwa kweli ni *strategic* ziko kwenye maeneo tu ya kawaida na wameshafanya ukarabati ambao kwa kweli ni kama hao wengine. Kwa hiyo tunasema Serikali iwajengee nyumba zingine mbadala Halmashauri hizo, tumeomba fedha Serikalini.

Lakini suala la nne, ilikuwa ni baadhi ya waliouziwa sasa kutotekeleza masharti ya mkataba ambayo ni kulipa kwa mujibu wa mkataba. Ni kweli na ndiyo maana nilitaka kumwambia Mheshimiwa Kimaro katika zile shilingi bilioni 59 hizo bilioni 27 ambazo hazijalipwa si kwamba zilitakiwa zilipwe kufikia leo zote hizi 27 kwamba zilitakiwa zilipwe kufikia mwisho wa mkataba ambao ni mwaka 2012 na 2014.

Lakini kuna wengine kufikia sasa hivi walitakiwa kuwa wawe wameshalipa kama shilingi bilioni 1.9 lakini wamelipwa shilingi bilioni 1 idadi yao wala si kubwa katika wale ambao wanaendelea kulipa 5,141 ni 193 tu ambao hawako *up to date* na hao wamepewa notisi tarehe 21 Aprili, 2008 waweze kukamilisha malipo yao kufikia Machi, 2008 ambayo walikuwa wanadaiwa.

Kwa hiyo, kufikia tarehe 5 Mei, 2008 kama watakuwa hawajalipa ni kama shilingi milioni 900.7 hatua za kuchukua katika zile nyumba. Tumekuwa tukifanya hivyo na mara nyingi kwa kweli ukishafanya notisi kabla haijaisha unakutaa wanakimbia wanakuja. Sasa hilo halina tatizo kama watalipa *well and good*.

Mheshimiwa Spika, hizi hatua ambazo tunazichukua nimesema *data* hizi na takwimu hizi tutaziweka vizuri kwa maana ya *up date* wakati ule ambapo sasa tutakuwa tayari kuleta taarifa hii kwenye Bunge hili Bunge ione kwamba tumefanya kazi gani mpaka sasa.

Lakini niseme tu kwamba hii Kamati tuipe muda kidogo kwa mujibu wa maagizo yenu na sisi tutafanya nao kazi kwa karibu ili tuweze kupata sasa halisi halisi ni nyumba zipi ambazo hazikustahili kuuzwa na zimerudishwa ngapi kufikia hapo kwa sababu nia ni kuzirudisha hizo ambazo zimekaa sehemu *very strategic* na *sensitive* na wale ambao hawakustahili kuuziwa, wakauziwa tunawatoa na kuwanyang'anya hivo nyumba na Halmashauri tunawajengee nyumba mbadala na hawa wanatimiza mikataba yao.

Haya ndiyo mambo ambayo tunayafanya na ndio maagizo ya Bunge na ndiyo maagizo ya Rais kwa kweli na sisi tunaahidi kwamba katika muda ambao tumepeewa tutaleta sasa taarifa ambayo ni *up to date* na ambayo itakuwa inaonyesha tunachukua hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize kwamba nyumba ambazo zitatengwa kwa ajili ya viongozi na watumishi waandamizi wa umma ambao wanastahili kupewa nyumba kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi hazitauzwa tena. Hizi ambazo tunazijenga sasa

kwa ajili yao hazitauzwa isipokuwa hizo za zamani ambazo kwa kweli tuseme zote kama zimeshauzwa na kwamba sasa tunaelekea katika utaratibu huo ambao utatuwezesha kuwa na nyumba.

Kwa kweli nyumba ambazo ni mpya gharama za matengenezo sasa kwa miaka mingi itakuwa ni kidogo ukilinganisha na zile ambazo ziliuzwa.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kuunga hoja mkono na taarifa hiyo tutaileta tutakapokamilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, nyumba za Serikali ni mali ya Watanzania wote na siyo za Wafanyakazi wa Serikali. Uuzaji wa nyumba hizi, haukuzingatia Sheria ya Manunu na Uuzaji wa Mali za Serikali. Walionunua nyumba hizi wengi wao hawaishi katika hizi nyumba, zimegeuka ni miradi yao. Maendeleo ya nchi yanarudi nyuma sana, kwa sababu Serikali inatumia pesa nyingi kuwaweka maofisa hotelini, badala ya kupeleka hizo pesa kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uuzaji huu umepigwa kelele na zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania. Tunajua sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Kwa nini Serikali haitaki kusikia hoja hii ya Watanzania wengi wanaotaka nyumba zote bila kubagua, zirudishwe Serikali na zibakie kuwa ni mali za Watanzania wote?

Mheshimiwa Spika, hisia za Watanzania wengi ni kwamba, kiongozi mkubwa mmoja alipotamani nyumba moja na kuinunua na hapo ndiyo na wengine wakaanza kuomba kununua. Baada ya Maofisa wengine kuona yanayotokea, nao wakataka wapewe nyumba, kwa kuwa wakubwa walikwisha anza kununua, palikuwa hakuna njia ya kuwanyima. Tuliambiwa waliopewa hizi nyumba ni Wafanyakazi wa Serikali wanaokaa katika hizo nyumba, lakini cha ajabu, wanapewa nyumba wasiasa na *ambassadors* walio nje ya nchi; huku ni kugeuka misingi ya uuzaji wa hizi nyumba. Ili imani ya Watanzania iwe na Serikali yao, ninaitaka Serikali isione aibu, irudishe nyumba zote na wale waliokwishalipa warudishiwe pesa zao.

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena, nyumba hizi sasa zimekuwa za biashara na hazikaliwi na waliouziwa. Uuuzaji wa nyumba hizi haukufta hali halisi ya bei ya nyumba na ardhi; mfano, kiwanja kitupu Oysterbay kinauzwa kwa zaidi ya shilingi milioni 500, lakini pamoja na nyumba zilizouzwa kwa bei ya kutupa, yaani kati ya shilingi milioni 10 na milioni 100 tu; hii ni hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali imewajengea nyumba mbali sana na mijini na Serikali inapata hasara kubwa kwa matumizi ya mafuta ya magari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nyumba zote zirudishwe kwa wananchi wenyewe.

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote makini duniani, huwa inahifadhi nyumba za Watumshi wake; kwa mfano, kuna Ikulu za Mara, Wakuu wa Majeshi, Polisi, Mahakama, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika historia ya Tanzania, tangu tumeporta uhuru kumekuwa na nyumba hizo hadi Awamu ya Tatu, Baraza la Mawaziri lilipoamua kuuza nyumba kupitia Waraka wa Serikali Namba 7 wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, uuzwaji huo umekiuka utaratibu wa kawaida wa kuwa na nyumba za Watumishi wa Serikali, kwani nyumba hizo zimejengwa kwa kodi ya wananchi hivyo, kuziuza kwa watu binafsi ni hasara kubwa, kwani watumishi wapya wenye stahili za hizo nyumba, itabidi wakae hotelini, kitu ambacho ni gharama kubwa sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi, nyumba hizo ziliuzwa kwa bei ya kutupa, hasa ikizingatiwa nyumba zenyewe ziko kwenye *prime areas* kama Msasani, Masaki, Osterbay na kadhalika. Kiwanja peke yake, kinafikia shilingi milioni 200, lakini pamoja na nyumba wameuziwa kwa shilingi milioni 15 – 20; hii ni aibu sana kwa Taifa!

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuuzwa kwa bei ya chini sana, bado wanunuzi hao wameshindwa kulipa kwa wakati, lakini si hilo tu, nyumba hizo zimebadilishwa kabisa, wengine wamefanya ni maeneo ya biashara na hata kuongeza nyumba nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha, kuona Serikali inayodai inafuata ukweli na uwazi (Awamu ya Tatu), ndiyo hiyo iliyouza nyumba hizi kwa usiri. Lazima Serikali ikubali kuwa, ubinafsi ulizidi busara na hivyo kuamua kwa makusudi, kuuza nyumba hizi huku wakijua walikuwa wakimaliza awamu yao ya uongozi. Huu ni ufisadi na kukosa maadili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, wakati anaingia madarakani, aliahidi kuwa baadhi ya nyumba zingerudishwa, lakini hadi leo sijasikia chochote. Tunaomba Serikali iwe wazi na itueleze ukweli wa jambo hili.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kauli yake ya kuzirejesha nyumba ambazo hazikufuata utaratibu, yafaa zirejeshwe Serikalini kwa manufaa ya viazi vijavyo na kwa manufaa ya umma. Kauli ya Mheshimiwa Rais ni muhimu sana na yafaa iheshimike.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana mtoa hoja binafsi na ninaiunga mkono hoja yake.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Hongera kwa hoja muhimu sana.

Kwanza, uuzaji wa nyumba ulikuwa na ninadhani hadi leo, hauna vigezo wala kumbukumbu za zoezi lenyewe. Kwa maana vigezo vyta nani anayestahili kuuziwa na gharama za kuuza zimefikiwaje.

Pili, utaratibu ulienda chini chini sana, hadi zoezi lilipofanyika watu walipewa vyeo na kuhamishwa nyumba zichukuliwe. Si haki mtu anayekaribia kustaafu, nyumba yake inapangiwa mtu mwingine akistaafu tu anaondolewa.

Tatu, watu wana wasiwasi; zoezi hili kushindikana, itakuwa kichekesho, ikiwa Bunge hili limezungumzia na kuelekeza mikataba muhimu, tena ya Kimataifa na kuweza kuwajibisha Viongozi Wakuu; leo kuna ugumu gani kutengua mikataba ya hapa kwetu? Kama tumeamua kuondoa uchafu tufanye hivyo.

Nne, nina wasiwasi wa utekelezaji wa hao wanaokusudiwa na hoja hii, kwani wengi wao wanahuksika na ununuzi wa nyumba hizo, labda tuwape muda hadi Juni; kama utekelezaji utakuwa bado, tuchukue hatua nyingine. Ahsante.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja. Hata hivyo, ninapenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

- (i) Kwa vile hata wale waliouziwa nyumba hizo, kuna taarifa kati yao wapo walioziwa na kujipatia faida kubwa kinyume na mikataba ya mauzo hayo, hao nao wanyang'anywe nyumba hizo kwa kukiuka mikataba na malengo ya mauzo.
- (ii) Mauzo hayo pia yalihusisha nyumba ambazo zipo chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa na au kujengwa katika Ardhi ya Mamlaka hiyo, kwa nia ya nyumba hizo kutumika na Serikali kwa matumizi ya umma. Mauzo ya nyumba yamekiuka lengo hilo na hivyo mkataba kuvunjwa na hivyo nyumba hizo zirejeshwe kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
- (iii) Serikali ilitoa taarifa ndani ya Bunge hili kuwa, kuna Kamati imeundwa kuchunguza mchakato wa mauzo ya Nyumba ya Serikali na Kamati hiyo ilitegemewa kumaliza kazi mwezi Februari, 2007, lakini hadi sasa Serikali imekaa kimya!

Hivyo basi, Azimio la Bunge liwe ni pamoja na kuitaka Serikali itoe hadharani, Taarifa ya Kamati hiyo. Vinginevyo, Bunge hailiwezi kutekeleza vyema wajibu wake kama ulivyo kwenye Katiba; ibara ya 63(2) ya kuisimamia Serikali. Iwe sehemu ya Azimio, Serikali kuleta taarifa hiyo Bungeni, ikiwa ni pamoja na taarifa ya utekelezaji wa Maazimio haya. Mheshimiwa ninatanguliza shukrani za dhati.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana hoja hii na bahati mbaya imechelewa sana kuletwa.

Heshima na sifa kwa viongozi imekwisha kabisa, baada ya nyumba kununuliwa na ye yote aliyebahatika Viongozi sasa hawaheshimiki na kukosa sifa za uongozi wao

kabisa, badala yake kuvutia kuwepo kwa mazingira ya rushwa; viongozi kunyanyasika; eneo wanaloishi kuwa hatarishi; na viongozi kudharaulika. Maeneo ya kuishi viongozi kabla ya kuuzwa yalikuwa yana ulinzi maalum. Kwa hivi sasa ulinzi haupo na kama upo ni hafifu sana. Labda suala lingine la kujiuliza; je, maeneo yaliyokuwa yanatumika kama eneo la jengo la mtumishi (*house boy quarter*), yapo kule Viongozi wanakoishi?

Mheshimiwa Spika, masuala yafuatayo yamejitokeza baada ya nyumba hizo kuuzwa: Nyumba hizo zimebomolewa; nyumba hizo zimekarabatiwa; na baadhi ya nyumba zimefungwa. Nyumba tajwa hapo juu ni zile ambazo zilinunuliwa na Serikali, hivyo zinasubiri uamuzi wa Serikali (Mahakama). Je, huu siyo usumbu kwa Viongozi?

Mheshimiwa Spika, viongozi waliobahatika kuwa wazoefu na zoezi la kununua nyumba sehemu moja, waliendelea kununua kila sehemu walikohamia. Je, wengine wataishi wapi watakapohamishwa?

Serikali itii Tamko la Rais la kurejesha nyumba hizo za Watumishi wa Serikali. Sensa ya nyumba hizo ijulikane Bungeni; Kama nyumba ilikarabatiwa au ilibomolewa, Serikali iwjajibike kikamilifu na fidia ya ujenzi wa nyumba hizo; Mikataba ifuwe; na hoja kama hizi ziwe zinaletwa Bungeni, kabla ya utekelezaji katika mfumo wa Miswada

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali, kuwauzia wafanyakazi wake nyumba ili kuwapa unafuu wa maisha au kuipunguzia Serikali mzigo wa kutunza nyumba za Serikali, mimi ningali ninasisitiza kuwa, hatua hiyo haikuwa na maslahi yoyote kwa wananchi wa kawaida, yaani kwa umma.

Mheshimiwa Spika, laiti wengi wa waliouziwa nyumba hizo wangeishi huko, ingeeleweka kuwa kweli walikuwa na uhitaji. Lakini katu, hali siyo hivyo. Ukweli ni kwamba, wengi wao wamechukua nyumba hizo, wakakarabati na wakazikodisha. Athari zilizojitokeza kwenye miji mingi ni kama zifuatazo:-

(i) Nyumba hizo kutumika tofauti na zilivyokusudiwa, yaani badala ya kutumika kwa *residential*; zimetumika kwa maduka, baa, hoteli, shule, *night clubs* na kadhalika; je, hii ni sawa viongozi kuharibu makazi kiasi hicho?

(ii) Viongozi ambaao walikuwa walengwa wa nyumba hizo, wakiwemo Wakuu wa Polisi Mikoani, Majaji na hata Wakuu wa Mikoa sasa wanaishi kwenye maeneo ambayo siyo salama sana kwa nafasi zao.

(iii) Baadhi ya nyumba chache zilizojengwa kuziba pengo hilo, zikiwemo hizo za Kisasa – Dodoma, hazina hadhi kabisa tena ziko mbali sana na maeneo ya ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kuihoji Serikali kama ifuatavyo: Je, zoezi hilo lililofanyika katika Awamu ya Tatu litakuwa endelevu, yaani Serikali kujenga nyumba na kuuzia wafanyakazi wake kila Awamu au la?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Umma wa Watanzania, wapatiwe elimu kuhusu jambo hili kwani wangali wanasononeka sana na kodi zao.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, mimi ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ni hoja ambayo kwa kweli imekuja/imeletwa ikiwa imechelewa, ilitakiwa iletwe katika Bunge hili miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kama Katiba inavyobainisha; Ibara ya 8(1)(a) inasema: “Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.”

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, utaratibu uliotumika kufikia umauzi wa kuuza nyumba hizo na kutokuwepo kwa idhini ya Bunge; zoezi zima ninaliita ni uporaji wa mchana wa mali ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, kukiukwa kwa dhahiri kwa Katiba kulifanywa kwa makusudi na Serikali. Hivyo, kimsingi ilipaswa nyumba zote zirejeshwe. Uamuzi huo kwa hakika ni ufisadi na udhalimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninakubaliana na mapendekezo ya mtoa hoja, waliokopeshwa kimakosa warudishe nyumba hizo. Aidha, nyumba zote zilizokuwa zikitumiwa na Maafisa kama wa Polisi, Mahakama, Magereza, Jeshi na kadhalika, nazo pia zirudishwe.

Mheshimiwa Spika, kama mtoa hoja alivyobainisha ni vyema majina ya wote waliouziwa nyumba hizo yaainishwe, pamoja na jinsi ambavyo wamekuwa wakizilipia.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya uuzwaji wa Nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama lengo ni kumsaidia mfanyakazi kupata nyumba asihangaike anapostaifu, mbona ni wa ngazi za juu tu; je, wale wa kati na chini wao watasaidiwa vipi? Nyumba zilizouzwa ndani ya maeneo ya kazi na za Viongozi wa Majeshi, zirejeshwe mara moja ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), iletewe orodha yote ya kila nyumba ilivyozwa na aliuziwa nani? Je, hakuna waliouziwa mara mbili; mfano, mtumishi aliyekaa kwenye nyumba ya Dar es Salaam na familia yake ikabaki humo wakati amehamia Sumbawanga ambako nako alinunua nyumba; mume na mke ambao wote walikuwa *entitled* kupata nyumba na walipewa kwa vile walikaa miji tofauti, mfano, Dar es Salaam na mwingine Morogoro?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nyumba zisizuwe tena. Ninaunga mkono hoja hii.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni makosa makubwa kwa Serikali kuuza nyumba zake. Mfano mdogo tu, nyumba za madaktari; unakuta madaktari wanatibu katika Hospitali ya Mawenzi, Moshi Mjini, lakini inabidi atafute nyumba ya kuishi mbali kabisa na hospitali. Sasa inapokuja dharura, watu wanapoteza maisha wakisubiri daktari atoke mbali ili kuja kutibu. Vilevile nyumba za Mahakimu, unakuta wanakodishiwa hoteli kwa bei kubwa, wakati Serikali ilikuwa na nyumba! Ninaunga mkono hoja, nyumba hizo zirudishwe Serikalini. Mpaka sasa bado kuna Wafanyakazi wa Serikali, ambao hawana nyumba za kuishi wanakodishwa. Nyumba zote zirejeshwe Serikalini.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kurejea swalı langu hapa Bungeni mwaka 2006, juu ya nyumba za Madakatari wa Hospitali ya Mkoa wa Singida, ambazo waliuziwa Madaktari. Niiombe Serikali irejeshe hizi nyumba, kwani madokta waliouziwa walishahama na wengine wamestaafu.

Mheshimiwa Spika, kero hii imekuwa kubwa, kwani madaktari wakipangiwa kuja Singida wanakataa. Hata hivyo, daktari kukaa mtaani haipendezi, pia kukaa mbali na eneo la huduma, wanapata shida pale panapotokea dharura ya mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliunda Kamati kufuatilia nyumba hizi, sasa nipewe jibu juu ya uamuzi uliofikiwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika; kuuza nyumba za Viongozi, pamoja na Watendaji Wakuu, jambo hili halikuwa la busara, kwani nyumba za Viongozi zilikuwa katika eneo maalum na zilikuwa na ulinzi wa kutosha, pia heshima ilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuuza nyumba za Watendaji haikuwa busara, kwani nyumba nyingine zilikuwa kwenye maeneo ya kazi. Hivi Serikali ilisahau kuwa huyo Mtendaji angestaafu kama ilivyotokea sasa, kwani waliouziwa nyumba wengi wao wamestaafu au wamehama? Hali hii imesababisha Watendaji hawa kukaa eneo mbali na kituo chake cha kazi; mfano, *OCD, RPC* na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, maeneo niliyotaja hapa juu ni maeneo ambayo hukaa Viongozi Wakuu, bali nyumba hizi ziliuzwa kwa Viongozi waliokuwa wanaishi humo bila kujali kuwa kuna kustaafuli, kukosa madaraka, mfano Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na kadhalika. Vilevile, Viongozi hawa huhama pia kama ilivyotokea kwa baadhi, sasa atakayekuja atakaa wapi?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nyumba mpya za Masaki na Kijitonyama, sio nzuri sana, kwani zimekuwa nyingi kiasi kwamba, likitokea baya tutawapoteza Viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuwa, zile nyumba ambazo zina umuhimu wa pekee, zirudishwe Serikalini na wanaoishi humo au walionunua, warudishiwe fedha zao; mfano, nyumba za Madaktari wa Hospitali ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaomba nyumba za Wakuu wa Idara; mfano, *OCD* na kadhalika, ambazo zimeuzwa zirudishwe, kwani raia kununua nyumba ndani ya eneo la Taasisi za Serikali sio vizuri sana; kuna siri za nchi, anaweza kutoa siri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nyumba ziliishauzwa, ninaishauri Serikali, wale wote ambao wanadaiwa, wapewe muda mfupi kulipa. Atakayeshindwa arudishe nyumba Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza mtoa hoja na jinsi alivyoonyesha mchakato mzima wa uuzaji wa Nyumba za Serikali.

Niungane naye kuwa, wananchi wengi wamekuwa wanalamikia zoezi hili kwa ujumla. Pamoja na nia nzuri ya Serikali, ilikuwa nia njema kama lingechukuliwa fungu, vikapimwa viwanja kwenye maeneo mbalimbali na awamu kwa awamu, watumishi wangejengewa nyumba kadiri alivyoochagua wapi wajengewe.

Kosa ni kuwauzia nyumba zilizojengwa eneo la Taasisi; mfano, nyumba ipo karibu na Mahakama, Makao Makuu ya Wilaya, Maregereza na kadhalika, hilo si zuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ione umuhimu wa kuwabdalishia nyumba wapewe/wajengwe sehemu watakayochagua. Sikubaliani na kuwanyang'anya bila mbadala.

Kuhusu watu wasio watumishi wa Serikali, wakati huo wa zoezi, lakini waliuziwa nyumba hao wazirudishe. Uhakika wa watu wa aina hiyo wapo na pia Serikali inawafahamu, ubinadamu wa kuihurumia mali ya umma utumike na isije ikazaa kuunda Tume kuwatambua. Serikali iwataje au wao wajisalimishe, nyumba za Serikali zirudishwe.

Hali ya uuzwaji wa nyumba za Serikali ilivyoithiri Wilaya ya Misungwi: Kwanza, Wilaya ya Misungwi ni Mpya ilianzishwa mwaka 1997 hivyo, haikuwa na nyumba nyingi za Serikali. Hata hivyo, zoezi la uuzaji wa nyumba lilichukua nyumba au waliuziwa wafuatao: Aliyekuwa *DC* aliuziwa nyumba aliyokuwa anaishi; Afisa Utumishi wa Halmashauri aliuziwa nyumba aliyokuwa anaishi; Afisa Usalama wa Wilaya aliuziwa nyumba aliyokuwa anaishi; Afisa Utumishi wa Wilaya aliuziwa nyumba

aliyokuwa akiishi; Mwekahazina wa Halmashauri ya Wilaya aliuziwa nyumba aliyokuwa akiishi; na *OCS* aliuziwa nyumba aliyokuwa akiishi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Halmashauri ya Wilaya, inahangaika kuwapangishia watumishi wake sehemu mbalimbali. Tuna matatizo makubwa sana ya Nyumba za Watumishi, mbaya zaidi nyumba zenyewe zipo maneo nyeti; ni hatari kiulinzi.

Ninaishauri Serikali iwatafutie viwanja na iwjajengee. Nyumba za Serikali zirudishwe, hii ni moja ya kero za Wananchi wa Misungwi.

Mwisho, ninalipongeza wazo hili, ambalo kama ushauri wangu utazingatiwa nitafurahi. Ninazidi kusisitiza, nyumba zilizo katika maeneo ya Utawala zote zikaliwe na watumishi si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza mtoa hoja na ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuwawezesha *Civil Servants* kumiliki nyumba ni nzuri na ni vyema iwaguse watumishi wote. Njia sahihi na ya haki ni mikopo isiyo na riba ili haki na usawa vitendeke. Njia ya kuwauzia nyumba baadhi tu ya watumishi na kadhalika kwa bei chee ni batili, ya upendeleo na ya hasara kwa Serikali na Taifa. Dhambi kubwa ni kule kuuzwa nyumba za Serikali Wilayani, kwa watumishi wanaohama na kuhamishwa wengi wao wala si wakazi wa wilaya hizo.

Wilayani Lushoto, nyumba za *DAS*, *OCD*, *DED*, Madaktari na kadhalika; ziliuzwa kwa watumishi ambao wamehamia kwingine. Haikujengwa nyumba mpya hata moja na watumishi nyeti wanaishi mitaani! Busara gani hii?

Mwisho, nyumba zote za Serikali Wilayani zirejeshwe.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa ni zamu ya mtoa hoja. Sasa namwita mtoa hoja ahitimishe hoja yake. Ni matumaini yangu kuwa kwa sababu Serikali imeiunga mkono hoja yako hutakuwa na haja ya kuzungumza kwa kirefu.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu naomba niwatambue Wabunge ambao wameungana na mimi kwa kuchangia kwa kuzungumza hapa Bungeni amba ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Teddy Kasela Bantu, Mheshimiwa Benson Mpesa na Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Makongoro Mahanga.

Mheshimiwa Spika, sasa niendelee kuwatambua waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Philemon

Ndesamburo, Mheshimiwa Suzan A. Lyimo, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa James Lembeli.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mheshimiwa Lucy Fedelis Owenya, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Yono Stanley Kivela, Mheshimiwa Mchungaji Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shelukindo na Mheshimiwa Manju Omar Salum Msambya.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niishukuru Serikali kwa kukubali hoja. Mimi ninasema mwendo huu tunaokwenda nao sasa ni mzuri, tunafanya kazi vizuri, ambazo tulitumwa na wapiga kura na Serikali vilevile inatimiza sasa wajibu wake kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja imefika na kwa kuwa Wabunge walichangia, nипитие kwa haraka haraka michango yao kwa ujumla. Wabunge, wameunga mkono hoja na wametoa maoni yafuatayo: nyumba za Serikali ni mali ya Watanzania wote, uuzaji wa nyumba hizo haukizingatia maslahi ya Taifa, bali ya watu binafsi waliopewa dhamana ya uongozi wa wananchi. (*Makofi*)

Utaratibu uliotumika kuuza nyumba za Serikali, haukuhusisha wananchi, kwani haukupitia kwenye Bunge ambalo ndiyo chombo chao. Uuzwaji wa nyumba hizo, haukizingatia taratibu za kawaida za uuzaji wa mali za umma na haukizingatia Sheria ya Manunuzi. Mauzo ya nyumba hizo, yalikiuka malengo ya kujenga nyumba hizo kwa kodi za wananchi. Baadhi ya watumishi na viongozi, waliuziwa nyumba zaidi ya moja katika maeneo tofauti na ambazo walikuwa hawaishi. Baadhi ya watumishi waliouziwa kwa bei nafuu, waliziuza kwa watu wengine kwa bei ya juu sana, kinyume na mikataba yao. (*Makofi*)

Madhara yaliyotokana na Serikali kuuza nyumba za viongozi na watumishi wake ni pamoja na baadhi ya viongozi na watumishi, kutoheshimika na kupungua thamani yao kwa wananchi, kwani baadhi walizikodisha na kulazimika kuishi katika *servant quarters* na baadhi hupanga nyumba hafifu, kwenye mazingira ambayo ni hatarishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haikuwa busara kuuza nyumba hizo, kwani baadhi ya watumishi wanaopangwa kazi mikoani kama Madaktari, hushindwa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi kutokana na kuishi mbali na kituo cha kazi na baadhi kushindwa kuendelea na kazi baada ya kukosa nyumba inayokidhi matakwa ya kawaida ya mtumishi. (*Makofi*)

Serikali hulazimisha kuingia gharama kubwa za kuweka watumishi wake hotelini, wakati inahangaika kuwatafutia nyumba za kuishi. Mmemsikia hata Mheshimiwa Mpesya amesema, shilingi milioni 41 zilitumika kule kwake. Ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge; Serikali itekeleze Agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuzirejesha nyumba ambazo ziliuzwa kwa watu ambao siyo watumishi, ambazo watumishi walishindwa kulipia ili zitumike kwa manufaa ya umma. (*Makofi*)

Serikali iwasilishe Bungeni, taarifa ya uchunguzi na mchakato mzima wa kuza nyumba za Serikali, ambayo Kamati husika ilimaliza kazi yake mwezi Februari, 2007. Nyumba zote zilizouzwa kwenye maeneo ya kazi na zile zilizojengwa maalum kwa ajili ya Viongozi wa Serikali na vyombo vyake, zirejeshwe Serikalini ili walengwa waweze kuzitumia kwa manufaa ya umma. Watumishi wa Serikali waliouziwa nyumba kwa mkopo na kuziua kwa watu wengine kinyume na mikataba yao ya mauzo, wanyang'anywe na mikataba yao ivunjwe. Iwapo Serikali itakuwa na mpango wa kuza mali za umma ni vyema Bunge lihakikishe, kabla ya kutekeleza mpango huo ambao hatima yake ni madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha, ningeomba nisisitize tu kwamba, nyumba zilizouzwa huko Mawilayani, nyumba za Halmashauri na nyumba zilizoko sehemu nyeti; zirejeshwe kama Wabunge walivyoshauri na kama Serikali ilivyokubali hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kusoma mchango wa Mheshimiwa Balozi Mshangama unasema; hoja ya kuwawezesha *civil servants* kumiliki nyumba ni nzuri na ni vyema iwaguse watumishi wote. Njia sahihi na ya haki ni mikopo isiyo na riba ili haki ya usawa itendeke. Njia ya kuwauzia nyumba baadhi tu ya watumishi kwa bei ya chini, yeche amesema kwa bei chee ni batili na ya upendeleo na ya hasara kwa Serikali na Taifa.

Dhambi kubwa ni kule kuuzwa nyumba za Serikali Wilayani, kwa watumishi wanaohama na kuhamishwa na wengi wao wala siyo wakazi wa Wilaya hizo. Wilayani Lushoto nyumba za *DAS*, *OCD*, *DED*, za madaktari na kadhalika, ziliuzwa kwa watumishi ambao wamehamia kwingine. Haikujengwa nyumba mpya hata moja na watumishi nyeti wanaishi mitaani. Anauliza; je, hii ni busara? (*Makofî*)

Ninaungana naye kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema, kati ya nyumba 7,921 ambazo ziliuzwa, mpaka sasa zimejengwa, nyumba 650 tu. Kwa hiyo, watumishi waliopo Wilayani na Watumishi wa Halmashauri, hawana mahali pa kuishi. Madiwani wanapata tabu sana, kutafuta fedha kwa ajili ya kuwaweka hawa watumishi kwenye nyumba za kupanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukivaa nguo kwa muda mrefu bila kuifua, itakuwa na chawa na ukija kuifua, lazima kwa upande mwingine itachanika. Kwa kuwa unataka kuivaa ni sharti uishone. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaliomba sasa Bunge lako likubali hoja hii. Ninaomba kutoa hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Hoja iliyopo mbele yetu ni ile iliyopo ukurasa wa pili na wa tatu wa mtiririko wa maazimio yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Kimaro. Ninasema hivyo, kwa sababu jambo hili linaweza kuleta mkanganyiko mkubwa.

Wakati akichangia, ameongeza aina nyingine za nyumba ambazo hazimo katika azimio alilolipendekeza hapa. Sasa hata jana nimesikia redio moja wakisema, nyumba

zinarudishwa. Ndiyo maana ninasema, tunajielekeza katika maazimio ambayo yapo hapa ambayo ni manne.

Kwanza, kutekeleza Agizo la Rais la kurejeshwa nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu. Pili, ambalo ina-*qualify* lile lile, zirejeshwe nyumba hizo zilizouzwa kinyume cha utaratibu. Tatu, kuwepo orodha ya nyumba ambazo ziliuzwa kwa watu amba si watumishi wa Serikali, kinyume na utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali.

Mwisho, Serikali ichukue hatua wale amba yo hawajalipia, mikataba yao ya kuuziwa irejewe kuhakikisha kuwa, malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao ifutwe.

Haya ndiyo maazimio yaliyowasilishwa rasmi hapa. Mjadala ulikuwa mpana zaidi kuliko hapo. Kwa hiyo, sasa ninawarejesha kwenye maazimio na kwa hiyo, nitawahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Hoja Binafsi ya Uuzwaji wa Nyumba za Serikali
ilipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana wakati wa mjadala wa *TICTS*, niliagiza upatikane ushahidi kutoka kwa Mheshimiwa Nazir Karamagi, aliyechangia hoja hiyo binafsi ya Mheshimiwa Zambi. Leo ameniandikia ifuatavyo; ninaisoma barua yake:-

Mheshimiwa Spika, Waraka wa Baraza la Mawaziri, kuhusu kuongeza Mkataba wa *TICTS* kwa kuzingatia maagizo yako, ninapenda kutoa taarifa kuwa, kiutaratibu Waraka wa Baraza la Mawaziri huwa ni siri. Hivyo, kudai kuwa niwakilishe kwake Waraka kama huo ni kitu ambacho hakiwezekani. Kawaida kitu ambacho kinafanyika ni kuomba na kunukuu kumbukumbu za kikao. Taarifa kuwa uamuzi wa kuongeza Mkataba wa *TICTS*, ulifanywa na Baraza la Mawaziri, ultolewa ninadhani alikuwa na maana ilitolewa hiyo taarifa wakati wa majadiliano kati ya *TICTS* na Serikali, yaliongozwa na *PSRC*. Nukuu ya Kikao cha Baraza la Mawaziri nitaitafuta na kuiwasilisha kwako, kabla ya Kikao cha Bunge kinachofuata. Ninashukuru. Ameweka sahihi, Mheshimiwa Nazir Karamagi.

Nimeitisha *Hansard*, inasema ifuatavyo:-

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mwongozo wa Spika,

SPIKA: Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Anna Abdallah.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), ninaomba mwongozo wako, msemaji wa sasa atusaidie. Hakuwa Waziri wakati ule, lakini anathabitisha hapa kwamba, jambo hili liliamuliwa na Baraza la Mawaziri. Mimi

kwa uelewa wangu, jambo likishaamuliwa na Baraza la Mawaziri, mwandishi anakuwa ni Katibu wa Baraza. Sasa pengine hayo anayajua zaidi kuliko sisi tunavyojua, pengine ungemtaka pia atufafanulie juu ya jambo hili. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Anna Abdallah. Ninadhani hili ni la msingi, katika vile viambatisho ambavyo niliruhusu viingie ndani ya Bunge, ingependeza kama tungekuwa na barua inayonukuu uamuvi wa Baraza la Mawaziri. Sasa kama kweli ulikuwepo uamuvi huo na tunajua maamuvi hayo huwa yanaandikwa rasmi, kama alivyosema Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa dokezo la *Chief Secretary*; sijui Mheshimiwa Karamagi, kama upo ushahidi huo basi useme na udhihirike kama haupo basi uondoe maneno kwamba, mkataba huu ulipitishwa na Baraza la Mawaziri.

MHE. NAZIR M. KARAMAGI: Mheshimiwa Spika, mimi nina ushahidi kutokana na maandishi ambayo yalitumika wakati tunafanya majadiliano na *PSRC*, ambao mbele yao walikuwa na Waraka ambao ulikuwa unatoka kwa Baraza la Mawaziri, ambao unaruhusu waanze kufanya majadiliano na *TICTS*.

SPIKA: Basi ninakupa hadi kesho uweze kuwasilisha ushahidi vinginevyo, itabidi Kanuni zitumike kuhusiana na kulidanganya Bunge. Kwa hiyo, ninakupa hadi kesho saa 5.00 uweze kunifikishia ushahidi huo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mtaona wazi kwamba hapa Spika, hakuomba Waraka wa Baraza la Mawaziri. Spika ameomba ushahidi kwamba, uamuvi ni Baraza la Mawaziri. Sasa saa tano imepita, ushahidi sijaupata na kwa kuwa ninadhani Mheshimiwa Karamagi hakufuatilia vizuri, basi ninampa muda zaidi ili auwasilishe huo ushahidi kwamba, jambo hili liliamuliwa na Baraza la Mawaziri. Ninasema tena, sidai Waraka wa Baraza la Mawaziri. Mimi nimekuwa Waziri kwa miaka 14, ninajua taratibu zote zinazohusiana na Baraza la Mawaziri, sidai Waraka wenye, lakini ninadai ushahidi kwa maana ya kwamba, kutoka kwa Katibu wa Baraza tuweze kuthibitishiwa hilo. Kwa hiyo, siwezi kusubiri mpaka Mkutano wa Kumi na Mbili, ninaombwa wiki ijayo kabla ya Ijumaa niweze kupata ushahidi huo ni rahisi tu kwa sababu unapatikana pale Ikulu. Baadaye mimi ndiyo nitatoa taarifa sasa kwa Bunge zima. Vinginevyo, itanibidi nilepeleke suala hili kwenye Kamati ya Maadili, kama utaratibu unavyohitaji, kwa sababu ni jambo la hatari kulidanganya Bunge, kwa kitu kizito kama hiki, kama ndiyo hivyo ilivyotokea. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, la pili, nimekuwa nikiangalia, tunafuatilia kiti kile katikati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Jamani kinatumika vibaya sana. Jana kulikuwa na msululu, maafisa hapa mezani wamehesabu jana kati ya saa tatu na saa saba; Wabunge 14 wamekwenda pale kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu muungwana, mstaarabu kwa hiyo, hajnilalamikia, msidhani amelalamika. Mimi nimeona kwa uendeshaji mzuri wa Bunge na tunamtazamia Mheshimiwa Waziri Mkuu, afuatilie mijadala ya Bunge na kwa hakika hapo panapendeza kwa Waheshimiwa Mawaziri, kwenda kumshauri juu ya mambo yanayoendelea kwa kifupi.

Mbunge kama kuna tatizo, kuna ngedele wameingia kwenye shamba kule jimboni na kadhalika, sasa Waziri Mkuu ni Muungwana atakusikiliza, lakini wakati huo yale mengine ya maana ambayo ndiyo michango ya Wabunge, vinampita pemberi. Kwa hiyo, hawezi kujibu swal la nyongeza, pengine kwa jambo la msingi. Kwa hiyo, ninaomba sana kwenye *budget session*, Waheshimiwa Wabunge tufanye jitihada, Waziri Mkuu anapatikana Ofisini kwa masuala mengi ya Jimbo tunaweza kumpata. Kukaa muda mrefu naye pale, kwa hakika na kwa wingi kabisa, wengine wanavizia tu akiondoka mwingine, mwingine kaja kama jana wale Wabunge 14. Kwa hiyo, ninaomba sana tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuweza kufuatilia mijadala na kuweza na yeze kuona mchango wa Wabunge na kuutathmini, kwa sababu yeze ndiye mtekelezaji mkuu, kwa hiyo ni vizuri aweze kufuatilia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao Wenyeviti watatu, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge na kwa safari hii ni kwamba, nimefanya makusudi kuwe na uwakilishi wa pande zote za Muungano. Sasa Wenyeviti wawili, wamekaa hapa na kuongoza shughuli, nilikuwa ninadhani haitapendekeza kumaliza Mkutano wa Kumi na Moja bila Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kuweza kuketi hapa na kuongoza mambo. Kwa hiyo, kwa maana tu ya maazimio haya au shughuli hizi zinazokuja za maazimio, nimeamua nimpishe kidogo, aanze kuzoea kwa sababu nitamtumia sana wakati wa *budget sesssion*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mwenyekiti, ninaomba uje Kitini. Ila baada ya maazimio, mimi mwenyewe nitarejea. (*Kicheko/Makofi*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Waheshimiwa Wabunge, labda nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati sana kwanza kwa imani yenu kuniamini na mimi niweze kukalia hiki kiti kizito kabisa. Naamini nkipata ushirikiano wenu tutafanyakazi vizuri sana na tutaweza kuwawakilisha wananchi vizuri sana. Kwa kumalizia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuweza kuniamini kama Mbunge wao kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofi*)

**AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MKATABA WA USALAMA, AMANI NA
MAENDELEO WA UKANDA WA MAZIWA MAKUU WA MWAKA 2006**
*(PACT ON SECURITY, STABILITY AND DEVELOPMENT IN
THE GREAT LAKES REGION)*

WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu, kwa kuweza kupewa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa juu ya pendekezo la kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa nchi 11 wa Angola, Afrika ya Kati, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kenya, Rwanda, Uganda, Sudan, Tanzania na Zambia, ambazo ni wanachama wa mchakato wa Amani wa Ukanda wa Maziwa Makuu, waliweka saini Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo ya Ukanda wa Maziwa Makuu (*Pact on Security, Stability and Development of the Great Lakes Region*), tarehe 15 Desemba, 2006, Jijini Nairobi, Kenya. Chimbuko la Mkataba huu ni maelekezo ya Azimio la Dar es Salaam, lililotokana na Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi wa Ukanda wa Maziwa Makuu, uliofanyika tarehe 19 – 22 Novemba, 2004 chini ya Uenyekiti wa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ambapo Tanzania ilisimamia kikamilifu, mchakato wa kutekeleza Azimio la Dar es Salaam hadi kufikia kupatikana kwa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Maziwa Makuu una wigo mpana kutokana na mahitaji na changamoto za usalama, amani na maendeleo katika kanda yetu. Hivyo, Mkataba huu unajumuisha Azimio la Dar es Salaam, Itifaki kumi, Mipango minne ya utekelezaji, Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji na Mfuko wa Ustawishaji na Maendeleo (*Special Fund for Reconstruction and Development (SFRD)*). Itifaki kumi zinazohusika ni kama ifuatavyo:

- (i) Itifaki inayohusu Kujiepusha na Vitendo vya Uchokozi na Kudumisha Ulinzi wa Pamoja;
- (ii) Itifaki inayohusu Demokrasia na Utawala Bora inayohimiza Nchi Wanachama kuheshimu Kanuni na Maadili ya Kidemokrasia;
- (iii) Itifaki inayohusu Ushirikiano wa Kimahakama, inayozitaka Nchi Wanachama kushirikiana katika masuala ya kurejesha washtakiwa, uchunguzi wa kimahakama na uendeshaji mashtaka;
- (iv) Itifaki ya Kuzuia na Kuadhibu Makosa ya Mauaji ya Kimbari, Uhalifu wa Kivita na Uhalifu dhidi ya Ubinadamu na aina zozote za Ubaguzi;
- (v) Itifaki dhidi ya Uvunaji Haramu wa Maliasili inayozitaka Nchi Wanachama kuanzisha taratibu za kikanda za kuhakiki maliasili kwa ajili ya uvunaji, usimamizi na uthibitishaji wa maliasili katika Ukanda wa Maziwa Makuu;
- (vi) Itifaki inayohusu Eneo Maalum la Ustawishaji na Maendeleo;
- (vii) Itifaki inayohusu Kukinga na Kukomesha Unyanyasaji wa Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto;
- (viii) Itifaki inayohusu Kuwalinda na Kuwasaidia Watu Wanaolazimika kuyahama Makazi yao;
- (ix) Itifaki inayohusu Haki ya Mali Miliki za Watu Wanaorejea kwenye Makazi yao; na

(x) Itifaki inayohusu Usimamizi wa Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu unaongozwa na Kanuni zinazohamasisha Nchi Wanachama, kuridhia na kutekeleza vipengele vyote vya Mkataba na mipango ya utekelezaji. Mipango hiyo ni pamoja na Usalama na Amani, Demokrasia na Utawala Bora, Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda na Masuala ya Kijamii na Kibinadamu. Sambamba na mpango wa utekelezaji, vyombo vya ufuatiliaji vilivyoainishwa chini ya mfumo huo, ambavyo kila kimojawapo kimepangwi majukumu yake mahususi ni Mkutano wa Wakuu wa Nchi, Kamati ya Mawaziri, Sekretarieti ya Mkutano na Kamati za Kitaifa za Uratibu

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba umeanzisha Mfuko wa Ustawishaji na Maendeleo, ambao ni chachu katika utekelezaji wa Mkataba huu, kwani fedha za Mfuko huo zitatokana na michango ya wanachama na nchi marafiki. Vilevile, Kuridhiwa kwa Mkataba, kutatoa msukumo katika kupata suluhisho la kudumu la usalama na utulivu katika Ukanda wa Maziwa Makuu na hivyo, kufungua fursa za kiuchumi baina ya nchi wanachama. Aidha, utekelezaji wa Mkataba, utasaidia kutatua tattizo la wakimbizi na wahamiaji haramu na hivyo, kuongeza kasi ya maendeleo katika Mikoa ya Magharibi mwa nchi yetu. Vile vile, utekelezaji wa Mkataba, utatoa fursa kwa Tanzania kufaidika na miradi ya kikanda kwa ufadhili wa Mfuko wa Ustawishaji na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu kwenye Sekta za Miundombinu na Usalama Mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Maziwa Makuu, utaanza kutekelezwa baada ya Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Maziwa Makuu, kupokea hati ya nane ya kuridhia Mkataba. Kwa kuwa hadi sasa, nchi zilizoridhia Mkataba ni saba, ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kenya, Rwanda, Uganda na Zambia ni dhahiri kuwa, Bunge lako Tukufu likiridhia azimio hili leo, Mkataba wa Maziwa Makuu utaanza kutekelezwa mara moja. (*Makofi*)

Jukumu la msingi la utekelezaji wa Mkataba huu ni la Nchi Wanachama. Hali kadhalika, Mkataba unatoa nafasi kwa wadau wengine kama vile Jumuiya ya Kimataifa, Sekta Binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Jumuiya za Kiraia, Wanawake na Vijana katika utekelezaji wa miradi iliyo katika Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni mhimili mkuu katika mchakato mzima wa usalama, amani na maendeleo ya Maziwa Makuu kwa sababu zifuatazo:-

- Nafasi ya Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Maziwa Makuu sasa hivi inashikiliwa na Mtanzania, Balozi Liberata Mulamula.
- Utekelezaji wa mkataba huu, utazifanya nchi kadhaa za bara (*land locked countries*) kutumia bandari zetu, reli yetu, barabara zetu, ndege zetu na hivyo kuiwezesha Tanzania kuongeza Pato la Taifa na ajira kwa vijana wetu.
- Rais wetu ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, ambaye pamoja na shughuli nyingine, anashughulikia masuala ya amani, usalama na uhimizaji wa ushirikiano wa

kiuchumi wa kanda mbalimbali. Kuridhiwa kwa mkataba huu na Bunge lako Tukufu leo hii, kunaipa nchi yetu na Rais wetu, heshima kwani tunatekeleza maagizo ya Umoja wa Afrika kwa vitendo.

- Matarajio ya Ukanda na Jumuiya ya Kimataifa kwa Tanzania ni makubwa kutokana na nchi yetu kusimamia vyema ajenda ya amani ya Ukanda wa Maziwa Makuu katika kipindi chote cha uanachama wetu katika Baraza Kuu la Usalama wa Umoja wa Mataifa na hasa katika kipindi chake cha Urais wa Baraza hilo Januari, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuridhia Mkataba huu, Tanzania itawajibika kuchangia kiasi cha dola za Marekani 1,269,784.60 kwa miaka mitano, ambacho ni sawa na wastani wa dola za Marekani 312,299.00 kwa mwaka. Hadi sasa, Tanzania imeweza kuchangia katika msimu wa mwaka huu dola 258,000.00, tumbakiwa na deni la dola za Kimarekani 54,299.00, ambazo tutazitekeleza kuzilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu ni kielelezo cha nia thabiti ya Wakuu wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu, kuligeuza eneo hili kuwa eneo la ustawishaji na lenye fursa lukuki za maendeleo. Matarajio na imani ya wadau wetu katika Ukanda wa Maziwa Makuu na Jumuiya ya Kimataifa, juu ya utashi wa Tanzania katika utekelezaji wa Mkataba huu ni makubwa. Si desturi yetu kuwaangusha, kama nilivyosema, kuridhiwa Mkataba huu na Bunge la Tanzania leo hii, kutaifanya Tanzania na hati yetu ya kuridhia kuwa ya turufu, ikizingatiwa kuwa ni nchi nane zinazotakiwa kuridhia ili uanzesha kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Nchi na Serikali za Ukanda wa Maziwa Makuu ulionzishwa mwaka 2004;

NA KWA KUWA katika Mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Dar es Salaam Tanzania mwezi Novemba, 2004 ulizaa Azimio la Dar es Salaam juu ya Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo;

NA KWA KUWA Mkutano huo uliagiza nchi Wanachama kulitafsiri Azimio la Dar es Salaam kwa vitendo;

NA KWA KUWA Azimio hilo lilizaa Mkataba huu uliosainiwa tarehe 15 Desemba, 2006 Mjini Nairobi Kenya;

NA KWA KUWA Mkataba huu una Itifaki mbalimbali zenye nia na azma ya kuzishirikisha nchi wanachama ili kujiepusha na vitendo vya uchokozi; ili kuheshimu kanuni na maadili ya kidemokrasia; ili kuwa na ushirikiano wa kimahakama; ili kuzuia na kuadhibu makosa ya mauaji ya Kimbari; uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya ubinadamu

na ubaguzi; ili kuzuia uvunaji haramu wa maliasili; ili kusitawisha maendeleo; ili kuzuia na kukomesha unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto; ili kuzingatia haki miliki za watu wanaorejea kwenye makazi yao; ili kuwalinda na kuwasaidia watu wanaolazimika kuyahama makazi yao; na ili kuimarisha usimamizi wa habari na mawasiliano;

NA KWA KUWA gharama za uanachama katika umoja huu ni ndogo kiasi cha dola za Kimarekani milioni moja na laki mbili kwa miaka mitano, kulingana na faida na manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano itayapata;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata uwezo wa kutekeleza Mkataba kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kupata suluhisho la kudumu la usalama katika Ukanda wa Maziwa Makuu na hatimaye kuimarisha usalama katika mipaka yetu na kuondokana na tatizo la wakimbizi;

NA KWA KUWA mpaka sasa nchi za Burundi, Congo DRC, Rwanda, Kenya, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Uganda na Zambia zimekwishardhia Mkataba huo;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huu na manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itayapata kwa kuridhia, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya Pili, linaazimia kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2008 (*Pact on Security, Stability and Development in the Great Lakes Region*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono na Serikali. Sasa atafuatia mchangiaji wetu mwingine, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Azimio hilo; Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

MHE. WILSON M. MASILINGI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu. Nianze kwa kukupa pongezi, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Kwa heshima, ninawasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo ya Ukanda wa Maziwa Makuu wa mwaka 2006. Awali ya yote, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima kubwa, kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kamati kwa Mujibu wa Kanuni namba 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, baada ya kujadili Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo ya Ukanda wa Maziwa Makuu wa mwaka 2006 (*Pact on Security, Stability and Development in the Great Lakes Region*) wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilikaa tarehe 23 Aprili, 2008 ili kupitia na kuchambua Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa mwaka 2006. Kamati ilielezwa kuwa, Mkataba wa Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Mkuu wa Mwaka 2006, unatokana na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2004, Jijini Dar es Salaam. Katika maelezo hayo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe, alieleza Kamati kuwa, baada ya Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali za Ukanda wa Maziwa Makuu, kukutana Nairobi Kenya mwaka 2006 na kusaini Mkataba huo, nchi zilizoridhia ni Kenya, Uganda, Congo DRC, Rwanda, Burundi na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa ibara ya pili ya Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa 2006, madhumuni makuu ni matatu yafuatayo:-

(a) Kuweka utaratibu utakaotawala uhusiano mionganini mwa Nchi Wanachama kama inavyobainishwa katika ibara ya nne ya Mkataba huo.

(b) Kutekeleza Azimio la Dar es Salaam, Itifaki, Mpango wa Kazi, Utaratibu wa Ufutiliaji na Mfuko Maalumu kama inavyotaja ibara ya tatu ya Mkataba huu.

(c) Kuweka mazingira ya usalama, utulilvu na maendeleo endelevu mionganini mwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia madhumuni na faida za Mkataba huo, kwa ujumla, Kamati yetu inaunga mkono Azimio la Bunge kuridhia Mkataba huu, hasa kwa vile maudhui ya jumla ya Mkataba yana faida kubwa katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Mkataba huu, utaiwezesha Tanzania kutumia fursa ya kuwa na bandari katika kukuza biashara. Aidha, mkataba huu utasaidia sana kuimarisha usalama katika mipaka yetu, jambo ambalo ni muhimu kwa utulivu na amani ndani ya nchi. Faida nyingine muhimu ni kuweka nchi yetu mahali pazuri katika diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mkataba huu una faida kwa Tanzania, Kamati inaushauri kuwa, Serikali ijiandae vyema kwa changamoto zitokanazo na kusainiwa kwa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Aidha, ninamshukuru sana Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Balozi Ali Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wataalam wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ufanuzi nzuri sana walioutoa mbele ya Kamati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nitoe shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa michango yao mizuri wakati wa majadiliano kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2006. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Kamati, Ndugu Athumani Hussein, kwa kazi nzuri katika kuihudumia Kamati yetu. Kwa heshima kubwa, ninaomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati, kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheheshimiwa Mohamedi A. Abdulaziz, Mheshimiwa Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamedi, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda na Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na tunaunga mkono hoja. Ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati. Sasa ninaomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM – MSEMADI MKUU UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kukupongeza kwa nafasi uliyoiopata. Hizo ni dalili njema kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninatoa shukrani zangu binafsi, kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo ya Ukanda wa Maziwa Makuu wa mwaka 2006 (*Pact on Security, Stability and Development in the Great Lakes Region*). Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni makuu kama yalivyoonyeshwa katika ibara ya pili ya Mkataba ni mazuri. Kambi ya Upinzani, inatoa dondo kidogo kuhusu

kifungu kidogo cha (c), ninanukuu: “*Create the condition for security, stability and sustainable development between the member States.*” Hapa maneno *security and sustainable development*, ndiyo yametufariji. Kwa hiyo, kwa sasa nchi yetu inadhani maneno hayo yametumiwa kwa dhana moja tu ya kulinda usalama wa mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona neno hili lina maana pana sana, kama vile likimaanisha maslahi ya Taifa, yaani *national interest*. Maslahi ya Taifa yanalindwa na viongozi wetu, ambao tumewapa dhamana ya kuangalia maliasili zetu ili itumike kwa maendeleo endelevu, yaani *sustainable development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja hiyo hapo juu, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi; inakuwa vipi mkataba huu unawabana na kuwachukulia hatua wanaodhalilisha usalama, yaani *security* ya nchi kwa njia ya ufisadi, jambo ambalo linaweza kusababisha *stability* na *sustainable development* kuwa mashakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema, Mkataba huu una itifaki mbalimbali, ambazo zitazuia uvunaji haramu wa maliasili ya nchi mwanachama. Kambi ya Upinzani, inalipongeza sana hilo, kwani Tanzania imekuwa ndiyo mwathirika mkubwa katika uvunaji haramu wa maliasili yetu. Wasiwasi unakuja kwa mtandao wa mafisadi wa maliasili zetu, una nguvu na unahusisha hata wale ambao tumewakabidhi madaraka kusimamia maliasili hizo. Je, kwa namna hiyo, nini kinatakiwa kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 4(1) inahusu maeneo ambayo yanasisi mamiwa na Mkataba, kuhusiana na mahusiano ya kisheria kati ya nchi mwanachama, imeonyesha maeneo ambayo yatapewa kipaumbele. Mkataba umeonyesha tena, *democracy and good governance*. Kambi ya Upinzani, inaona kauli kama hii imekuwa ikiongelewa katika mikataba kadhaa, ambayo inaletwa hapa Bungeni kwa kuridhiwa. Suala la msingi hapa ni kuwa pale ambapo viongozi wa nchi wanachama wanavunja sheria wazi wazi au nchi mwanachama ikishindwa kutekeleza misingi ya demokrasia na utawala bora, kwa mkataba huu, kiongozi huyo anatakiwa afanye nini? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akifanya majumuisho, atupe ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 6 ya Mkataba inasisitiza kuwa na Itifaki, Demokrasia na Utawala Bora. Kifungu kidogo cha (b), kinahusu uanzishaji wa taasisi zitakazohusu kukuza na kuendeleza misingi ya demokrasia na utawala, kanuni na sheria pamoa na kuangalia katiba za nchi wanachama, ambapo bado zinatoa mwanya kwa utendaji ulio bora, kwa mihimili ya dola iliyooanishwa katika katiba hizo. Kambi ya Upinzani, inakubaliana kabisa na yote yaliyosemwa katika ibara hii, lakini Tanzania kama nchi ambayo inasifikasi kulinganisha na nchi zote mwanachama wa mkataba huu, bado inashindwa kuwa kioo cha Demokrasia na Utawala Bora. Ukweli huu umejionyesha wazi wazi, matokeo mbalimbali yaliyojitokeza na yanayoendelea kujitokeza, kuhusiana jinsi gani haki za msingi za wananchi zinavyovunjwa na vyombo

vya dola, yaani matumizi ya nguvu za dola katika kunyamazisha wananchi kwenye madai mbalimbali katika asasi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 8 ya mkataba huu, inayohusu itifaki ninanukuu: “*Protocols for prevention and the punishment of the kinds of crimes of genocide, war crimes and crimes against humanity and all forms of discrimination* katika kifungu cha (d) cha Ibara hiyo kinachosema kuwa, *to condemn and eliminate all forms of discrimination and discriminatory practices.*” Kifungu hiki ni muhimu sana, hasa kwa nchi yetu ambayo siku zote, itaendelea kuwa na msemo wa amani na utulivu. Vitendo hivi ambavyo vinaanza kujitokeza vya kuanza kubaguana kulingana na mahali pa kuzaliwa ni sumu kwa umaja wetu, jumuiya nzima na nchi wanachama.

Kambi ya Upinzani, inasema kuwa, yejote yule ambaye anashindwa kujenga nguvu ya hoja katika suala lolote na badala yake akaanza kuingiza sumu ya ukabila na udini, basi mtu huyo ni wa kumchukulia hatua kali za kisheria. Mfano, machafuko ya Kenya, Burundi na Rwanda ni mifano iliyo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nami niendelee kukupongeza kwa nafasi uliyoipata na ninaomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Sasa tuna wachangiaji wawili tu ambao watachangia hoja hii na hatimaye tutamwita Mheshimiwa Waziri ili aweze ku-*wind up*. Kwa hiyo, ninaomba sasa nimwite mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa William H. Shellukindo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe maoni kidogo kuhusu Azimio hili la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo ya Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe, kwa kuiongoza Wizara hiyo kwa ufanisi mkubwa kabisa. Jukumu hili ni zito, nasi tupo tayari kumsaidia pale ambapo msaada utahitajika. Kwa mfano, msaada mmoja ni kwenye Azimio hilo, ninadhani kwako wewe litakuwa limekupa shida, kwa sababu ya mambo mawili. Kwanza, m Kutano Mkuu wa kwanza umefanyika Dar es Salaam mwezi wa 11 tarehe 20 mwaka 2004. Kwa hili tu inaonyesha kwamba, Tanzania ndiyo ilitakiwa ikimbie wakati wengine wanatembea, kwa kuwa nchi nyingine zimesharidhia Mkataba lakini sisi bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni lile ambalo Mheshimiwa Waziri amelieleza kwamba, tumekuwa na heshima kwamba, Katibu Mkuu Mtendaji au *Executive Secretary* ni Mtanzania, kwa hiyo nguvu za nyumbani alizihitaji sana. Kwa hiyo, ninadhani kwa hili tunalolifanya leo, tutakuwa tumempa nguvu zaidi kwamba na nyumbani kule

wanamsaidia kuweza kutekeleza majukumu yake. Kwa sababu anaweza kuulizwa na wenzake kule kwamba, umekalia kiti hapa wewe *Executive Secretary*, lakini mbona nchi yako haijaridhia; mbona Bunge la Tanzania halijaridhia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili alilizungumza jumla, halihusu Mkataba huu wala Itifaki. Nimeona mikataba mingi na itifaki nyingi zinachelewa sana kufika kwenye Bunge. Hili kwetu sisi linatupa tatizo, kwa sababu ni jukumu letu la Kikatiba katika ibara ya 63(3)(e) kwamba, tuna jukumu kama Bunge la kuridhia mikataba na itifaki ile ambayo inahitajika Bunge liridhie. Sasa inapochelewa, tunalaumiwa sisi kikatiba. Kwa hiyo, tungeomba sana Serikali itusaidie, tusipate hizo lawama. Kwa mfano, ninadhani Balozi Mula Mula akisia kwamba, Bunge linazungumza hili atakuwa na furaha kubwa. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani vilevile tungeweka utaratibu, sizungumzii mkataba huu tu; ninazungumzia mikataba mingine mingi na itifaki kwamba ni vizuri Bunge linaporidhia basi baadaye tuletewe taarifa za utekelezaji zinakwenda kwendaje huko. Kwa mfano, kwenye mikataba huu, inahitajika sana kuwa na programu ya utekelezaji na imeelezwa kabisa katika mikataba wenyewe. Kwa kuwa kuna itifaki nyingi ambazo zinastahili kutekelezwa ni vizuri kukiwa na programu ili tuweze kujuu maendeleo yake na kama kuna changamoto vilevile Bunge lijue. Kwa mfano, katika Itifaki inayohusu Amani na Usalama, utaona kwamba katika nchi ambazo ni wanachama au zinahusika na mikataba huu; Burundi, Uganda, Congo DRC na Sudan, zina migogoro ya ndani. Kwa hiyo, tunaridhia, sasa ni vizuri tukajua maendeleo yake yakoje, kwa sababu inahusu sana hii. Kwa hiyo, ningeomba sana kuridhia kusiwe kuridhia halafu tukanyamaza. Kuwe kuridhia na kufuatilia utekelezaji na kuona kama zile changamoto na sisi Bunge lina nafasi ya kusaidia kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo tu. Ninapenda kutamka kwamba, ninaunga mkono kuridhiwa kwa mikataba huu. Ahsante sana. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Shellukindo. Sasa ninaomba kumwita mchangiaji wetu wa mwisho katika hoja hii, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani. (*Makofit*)

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika Azimio hili lililoko mbele yetu. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Azimio hili hapa Bungeni, pamoja na kwamba, tumechelewa kidogo. Sisi ambao tuliwahi kushiriki katika mikutano hii kama Watanzania, tulijisikia kidogo vibaya tulipoambiwa kwamba, idadi haijatimia, kwa sababu zilitakiwa nchi nane ziwe zimeridhia. Tukajikuta sisi ndiyo tulikuwa wahamasishaji wakubwa katika suala hili na tukawa hatumo katika orodha ya watu ambao tumekwishardhia.

Ninashukuru leo Mheshimiwa Waziri, umeleta hii hoja hapa Bungeni na wale watakaokwenda kuiwasilisha katika mikutano hii kwa maana ya kutoka Bunge letu la

Tanzania, tutakuwa angalau sasa tumeondoa lile tatizo ambalo tulikuwa tunalihihi sisi ambao tulikuwa tunashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhia kwa Mkataba huu, kutasaidia mambo mengi ambayo yataleta manufaa ya wananchi wetu, ambao wanaishi katika maeneo haya ya Maziwa Makuu. Kama tunavyofahamu kwamba, nchi za Maziwa Makuu bado kuna migogoro mbalimbali, ambayo imetokana na vita ya wenyewe kwa wenyewe kutokana na mambo ya kisiasa. Wanaoathirika zaidi ni akina mama na watoto kuhamahama na kuwa wakimbizi katika maeneo yao na kuhangaika na kutokuwa na maendeleo ya kudumu katika maisha yao ya kila siku.

Sasa kwa kuridhia sisi mkataba huu, tutakuwa tumeongeza nguvu katika mijadala ambayo inajulikana kwa neno la *Inter-Parliamentary Forum* ya *Great Lakes Region*, kuweza kujadili vizuri na kutoa maamuzi sahihi, ambayo pengine itabidi yawafikie Wakuu wa Nchi ili watoe maamuzi kwa ajili ya kuendeleza *peace, security, stability and development*. Vilevile itasaidia katika suala zima la kuwa na Utawala Bora katika maeneo yetu haya ya nchi za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kwamba, Utawala Bora ndiyo utakuwa ufumbuzi mzuri kwa nchi hizi ambazo zina migogoro, ziweze kutulia na kuweza kupanga mipango yao ya maendeleo na kuweza kuwanufaisha wananchi wa maeneo yale, waweze kufanya shughuli zao za maendeleo, waweze kusoma na vile vile Utawala Bora kwa maana ya kushughulikia migogoro yao kwa utaratibu wa sheria hii itasaidia kupunguza migogoro na hizi kutulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu kwamba, baada ya *Summit* ya Nairobi, tarehe 15 Desemba, 2006 kilikaa kikao kingine Kinshasa tarehe 26 – 28 Februari, 2007. Mambo muhimu ambayo Serikali inaomba izingatie ni suala zima, linaloitwa *Kinshasa Declaration*, ninaomba ninukuu sehemu tatu, ambazo ninaona ni muhimu kwa Serikali kuzingatia mambo haya: *Kwanza, nishukuru kwamba hili la kwanza limekwishatekelezwa; To work towards attaining rapid ratification of the pact in order to enter into force as soon as possible in accordance with Article 33 of the Pact.* Ninashukuru leo hilo limetimia. Lingine vilevile niikumbushe Serikali kwamba, *request our Heads of States and Governments to take necessary measures to release the contribution owned to the regular budget of the conference Secretariat for the year 2007/2008* na kadhalika. Hilo ni muhimu ili hizi shughuli ziende vizuri. Hilo ni muhimu ili hizi shughuli ziende vizuri.

La mwisho, vilevile niseme kwamba, *Pact* inakumbusha pia *our respective governments to contribute to the special fund for reconstruction and development*. Sasa tukiweza kutekeleza haya na mengine mengi kwa sababu yapo kama 11, lakini nimesema tu kwamba, haya kwa Serikali yetu msije mkasahau kama tulivyosahau kuchelewa katika kuridhia *Pact* hii hivi sasa. Hayo mengine ili kuleta ufanisi mzuri kwamba, shughuli hizi ziwe endelevu na kuleta matunda na amani katika nchi zetu za Maziwa Makuu, haya ni ya msingi katika mambo ya *contribution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba, tunao wengi ambao wanashiriki katika mijadala hii, lengo kubwa ni kuleta amani katika nchi za Maziwa Makuu. Kwa hiyo, niishukuru Serikali kwa kuweza kuleta Azimio hili hapa Bungeni. Tumechelewa lakini hatujachelewa sana, ninaamini baada sisi kuridhia Tanzania sijui na wengine, tayari sasa hivi ninaamini kama anavyosema Mheshimiwa Waziri ni nchi saba tu ambazo zilikuwa zimeridhia, ilikuwa inahitajika nchi ya nane ili *quorum* itimie. Kama itakuwa kuna nchi yoyote toka kikao cha mwisho kilichofanyika Burundi, basi ninaamini leo sisi Tanzania kuridhia *pact* hii tutakuwa tumetimiza nchi ya nane. Kwa hiyo, vikao vitakavyokuja hivi sasa, *quorum* itakuwa imetimia na yale majadiliano ambayo yanahitaji yaendelee kwa maana ya kutimia *quorum*, sasa yatakuwa yametimia ili tuweze kuleta amani na utulivu na maendeleo katika maeneo yetu ya Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani. Sasa ninaomba nimwite, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ili aweze ku-*wind up*.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nikushukuru tena wewe, pamoja na wachangiaji ambao ningependa kuwatambua sasa. Waliochangia kwa mazungumzo ni Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa William H. Shellukindo na Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah. Aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mussa A. Zungu. (*Makofi*)

Ningependa nitumie muda mfupi, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa mawazo mazuri waliyotupatia. Ningependa kwanza, nitoe shukrani zangu kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye ametupa mawazo mazuri na mengi tumeyasikia na tutayafanyia kazi. Ningependa pia nimshukuru Mheshimiwa William Shellukindo, ametukumbusha kwamba, mikataba mingi inachelewa. Tumesikia ametukumbusha kwamba, tujitahidi tuwe na *action plan* na tutoe taarifa ya utekelezaji wetu kwenye Kamati inayohusika, pamoja na Bunge tunesikia na tutajitahidi kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, nimefarijika pia na mchango wa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na tumezingatia ushauri wake wa kutekeleza kwa vitendo *Kinshasa Declaration*, kwa sababu hicho ndicho kipimo cha utekelezaji wa mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Mkataba huu unatekelezwa wakati muafaka, kwa sababu kuidhinisha kwetu na kuridhia kwetu leo, kunafanya mkataba huu uweze kutekelezwa kuanzia Jumatatu. Ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kutengeneza historia katika Bunge, kwa kutumia wakati muafaka kuridhia Azimio hili. Hatutawaangusheni, tutawapa taarifa kabambe wakati wote tutakapohitajika kufanya hivyo na ningependa pia niwatakie kila la kheri, kwa wale tunaorudi majumbani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninapenda tena nirudie kwamba, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tunalishukuru Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri mliyoifanya mchana huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. Ahsante. (*Makofī*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa ninaomba muiamue.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(Azimio la Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu wa Mwaka 2006 (*Pact on Security Stability and Development in Great Lakes Region*) limeridhiwa rasmi na Bunge. Tunaendelea na shughuli inayofuata, Katibu.

M A A Z I M I O

AZIMIO LA KUUNGA MKONO KUANZISHWA KWA BUNGE LA SADC (ESTABLISHMENT OF A SADC PARLIAMENT)

MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, NIInawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, hoja ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu azimio la Bunge kuunga mkono, kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Establishment of a SADC Parliament*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni namba 86, fasili ya 5 na nyongeza ya 8, kifungu cha 9 fasili ya 2 na fasili ndogo ya (b), ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007; ninayo heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ili niweze kutoa hoja ya kuliomba Bunge lako lipitishe Azimio la Bunge, kuhusu kuunga mkono kusudio hilo la kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Establishment of SADC Parliament*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo mafupi ya Kamati, ninaomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati yetu waliojadili Azimio hili kama ifuatavyo: Mheshimiwa Wilson W. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu -

Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makweta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah. Salim, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda na Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilipata fursa ya kujadili kwa kina, umuhimu wa kuanzishwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika katika kikao chake cha tarehe 23 Aprili, 2008. Katika kikao hicho, tulimwalika mbele ya Kamati, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ambaye ni mwakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*. Kwa niaba ya wawakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*, yaani Mheshimiwa Samuel J. Sitta - Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Anne S. Makinda - Naibu Spika, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa. Wawakilishi wetu huko, kuhusu chimbuko la Azimio hili linalohusu umuhimu wa kuanzisha Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, tunawashukuru sana wawakilishi wetu na tungeomba Bunge liwape pongezi za dhati, wawakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*, kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuliletea heshima Taifa letu. Aidha, Kamati ilipokea maoni ya Serikali, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe - Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Serikali haina pingamizi kwa Azimio hili kuitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezingatia sana faida linganishi (*Comperative Advantages*) za kuwa na Bunge hili, dhidi ya utaratibu wa kuwa na Baraza la Kibunge la Nchi za Kusini mwa Afrika. Miogoni mwa faida hizo ni pamoja na kuziwezesha nchi wanachama wa *SADC*, kurasimisha utaratibu muhimu utakaosaidia kuunganisha mawazo ya nchi hizo na kupata nguvu zaidi katika diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ni kuwezesha makubaliano ya pamoja ya kieneo, kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu uhusiano wa kimataifa. Jambo hili ni muhimu sana kwa vile linaweka chombo rasmi cha kudumu, kitakachokutanisha Nchi Wanachama wa *SADC*; kisera na kidiplomasia. Vilevile kuanzishwa kwa Bunge hili, kutarahisisha majadiliano juu ya masuala yenye maslahi ya pamoja kieneo. Suala ambalo ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi katika Nchi Wanachama wa *SADC*, Tanzania ikiwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niliyoyaeleza ni maoni ya Kamati yangu kuwa, Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, litaongeza ufanisi wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa *SADC*, katika kuchangia maendeleo na utekelezaji

wa sera na mipango muhimu, dhidi ya matatizo yanayozikabili nchi zetu. Aidha, Bunge hilo litasaidia sana katika uoanishaji wa sheria mionganini mwa nchi wanachama; jambo ambalo manufaa yake ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba kusoma Azimio la Bunge kuunga mkono Kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. Azimio la Bunge kuhusu kuunga mkono kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, *Establishment of a SADC Parliament*.

KWA KUWA Baraza la Kibunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC Parliamentary Forum*), limeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 3 ya Katiba ya Baraza hilo, pamoja na fasili ya ibara ya 9 fasili ndogo ya 2 na 10, fasili ndogo ya 6 ya Katiba ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*);

NA KWA KUWA Baraza hili lilianzishwa kwa madhumuni ya kuwa na chombo cha mashauriano cha Kibunge (*Parliamentary Consultative Assembly*) Kusini mwa Afrika;

NA KWA KUWA dhamira ya Baraza hilo ni kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Establishment of a SADC Parliament*), kama chombo cha majadiliano kuhusu masuala mbalimbali yenye maslahi kwa nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

NA KWA KUWA Bunge hilo la *SADC* likianzishwa litakuwa na manufaa mengi kwa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo ya *SADC* kama vile; Kutia nguvu na kusukuma mbele hoja ya ushirikiano na muungano wa eneo la Kusini mwa Afrika (*Regional Cooperation and Intergration*) kuelekea ushirikiano wa muungano wa Afrika; kujenga, kukuza na kuimarisha umoja, utawala bora, demokrasia, haki za binadamu, usawa wa kijinsia, maendeleo ya kiuchumi na pia kuimarisha hali ya amani na utulivu katika eneo lote la Kusini mwa Afrika; kukuza ushirikiano wa Kibunge ndani na nje ya eneo la Kusini mwa Afrika; kuwa chombo cha kikanda cha majadiliano na mashauriano (*regional forum for dialogue and consultation*), kuhusu masuala mbalimbali yenye maslahi kwa wananchi wote wa eneo la Kusini mwa Afrika; kuwezesha ulinganifu (*harmonisation*), wa sheria katika eneo la Kusini mwa Afrika; na kuwezesha kuridhia na kutekeleza (*ratiification and implementation*), kwa haraka mikataba mbalimbali ya kimataifa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya *SADC*;

NA KWA KUWA tangu lianzishwe Baraza la Kibunge la *SADC*, limetoa mchango mkubwa katika kuimarisha ushiriki wa Mabunge ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Kusini mwa Afrika katika masuala yanayohusu Ushirikiano wa Kikanda kwa eneo hilo la Afrika;

NA KWA KUWA uwezo wa Wabunge wa kutoa ushauri na mawazo yanayoshawishi kujenga na kuiimarisha hoja ya maendeleo, ushirikiano na muungano wa kikanda na hatimaye kuwa na Muungano wa Baraza zima la Afrika, utaimarika zaidi kutokana na kuanzishwa kwa Bunge la *SADC*;

NA KWA KUWA Baraza la Kibunge la SADC lilikusudiwa kugeuzwa kuwa Bunge la Kikanda lakini muda wa kufanya hivyo haukubainishwa;

NA KWA KUWA maeneo mengine ya Afrika, yameanzisha Mabunge yao ya Kikanda kama vile Bunge la Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (*Economic Community of West African States - ECOWAS Parliament*; Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Legislative Assembly*); na Bunge la Nchi za Pembe ya Afrika (*Inter-Governmental Authority and Development – IGAD*):

NA KWA KUWA Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ndiyo pekee katika Afrika ambayo haina Bunge lake la Kikanda;

NA KWA KUWA Mabunge yote ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*), yameombwa kujadili na kuitisha Azimio la kuunga mkono hoja ya Kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na kuwasilisha taarifa ya kuitishwa kwa Azimio hilo katika Mkutano wa 27 wa Kilele wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*The 27th SADC Ordinary Summit of the Heads of States and Government*);

KWA HIYO BASI, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wake wa Kumi na Moja linaazimia kwamba, linaunga mkono hoja ya Kuanzisha Bunge la Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Establishment of SADC Parliament*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. (*Makofit*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Waheshimiwa Wabunge, tuna mchangiaji mmoja tu kwa hoja hii, ninaomba niite jina lake, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kabla sijafanya hivyo, ninaomba nikupongeze kwa heshima kubwa uliyoipata ya kukaa kwenye Kiti hicho. Ninaomba niseme, umependeza kweli kweli. (*Makofit*)

Ninaomba nitoe shukrani za dhati, kwa Mwenyekiti wa Kamati, kwa kuchambua, kujadili na kuona kwa upana sana, yote yaliyomo katika Azimio hili. Ameleta mbele ya Bunge lako Tukufu, mapendekozo yote ambayo mimi nilipata nafasi ya kuchangia kwenye Kamati yake. Ninamshukuru sana yeye, pamoja na Kamati yake. Ninaomba kuishukuru pia Serikali yetu, kwa kuunga mkono Azimio hili kwa sababu sasa ni dhahiri

kabisa kwamba, Bunge letu na Serikali yetu, tumeungana katika kuunga mkono jambo hili ambalo linatia uzito katika kuunga mkono Azimio letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa niaba ya wenzangu; Mheshimiwa Anna S. Makinda, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa na Mheshimiwa Spika, ambaye yecheza anaingia kwa kofia yake katika Bunge la SADC. Mnakumbuka kwamba, mlituchagua tuwe wawakilishi wenu na ninashukuru Mwenyekiti ameshalitaja hilo, lakini na mimi kwa niaba ya wenzangu, niwashukuruni sana, kwa heshima mliyotupa tuweze kuwawakilisha katika Bunge hilo, ambalo kwa sasa linaitwa *SADC Parliamentary Forum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika hapa kwa kifupi tu ni utaratibu wa Wabunge, kwenda kwa wapiga kura wao. Sisi Wabunge wa SADC katika ujumla wetu, tulikubaliana kwamba, tunafanya Azimio kama Bunge la SADC (*Parliamentary Forum*), kufanya mpito (*transition*), kwenda kwenye Bunge la SADC. Tunapofanya Azimio hilo, sisi wenyewe ni lazima turudi pia kupata maoni ya wapiga kura wetu. Kwa hiyo, kinachopatikana leo ni maoni ya wapiga kura wetu, ambao ni Mabunge yetu na kwa maana hii; Bunge la Tanzania. Katika hatua hii, hatujafikia hatua ya *protocol*, ambayo ndiyo itaihusisha na Serikali na siku ile sasa *protocol* itakaporidhiwa, ndio Bunge rasmi litaanzishwa. Kwa leo kinachoombwa ni nia ya kuunga mkono, kwenda kuanzisha Bunge lenyewe; nia ya kuianzisha, sio kulianzisha Bunge kwa leo.

Baada ya kulisema hilo moja tu ambalo Mwenyekiti wa Kamati labda hakuliweka kwa ajili ya muda, niseme tu kwamba, kwa hivi sasa tuna wajumbe watano katika Bunge au *Parliamentary Forum* kama tunavyoliita. Katika Bunge linalotarajiwa, hatutegemei kuwa na gharama ya ziada, labda zile taratibu za kawaida tu; gharama kuongezeka kwa sababu ya wakati na kadhalika. Hatutegemei kuwa na gharama ya kawaida, kwa sababu Katiba ya Bunge hilo imebakia kama ilivyo hivi sasa; kwamba, Wabunge watatokana na Wabunge ndani ya Bunge, kwa kipindi kile ambapo Bunge linakuwepo. Kwa hiyo, hakuna gharama kwa nchi wanachama na tulilizingatia hilo ili tusiongeze mzigo kwa wapigakura wetu. Kwa hiyo, tulitaka kuondoa hiyo hofu, watu wasione kwamba, Mabunge yanakuwa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni lile ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amelisema; Ukanda wetu ni wa pekee ambao umebaki bila Bunge. Katika Katiba ya AU, tulipoanzisha PAP; moja ya mambo muhimu yaliyosemwa ni kwamba, Bunge la Afrika litakuwa na haya Mabunge ya Kikanda, kama ngazi ya kufikia Bunge la Afrika. Sasa wenzetu wote Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na hata Kanda ya East Africa, wanapokuja kwenye Bunge la Afrika, wanapata mawazo kutoka kwa wawakilishi wa Mabunge ya Kanda zao. Ukanda wa SADC ni ukanda pekee, ambao umebaki bila kuwa na Bunge. Kwa hiyo, Wabunge wetu wanakwenda kwenye PAP, kama mtu mmoja mmoja, japo tuna utaratibu wa ndani ya Bunge la SADC la sasa, kuweza kukaa pamoja nao na kuweza kuwapatia mawazo ya Kanda yetu. Itakuwa msaada mkubwa sana, Bunge hili likipatikana, linaweza likawasaidia sana Wabunge wetu katika Bunge la Afrika. Jana tulifanya uchaguzi wa Bunge la Afrika, ninadhani hii itakuwa ni njia ya kuimarisha Wabunge wetu kwenye Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamke tu mwisho kwa kumalizia, Wabunge tukifanikiwa kupata Bunge hili, tunazungumzia Wabunge watakaowakilisha Wabunge wenzao 3,000 katika Ukanda wetu katika nchi 14 za *SADC*. Kuwa na Wabunge 3,000 ni wengi na ni Ukanda mkubwa ambao unategemewa kuwa na wananchi takriban 250,000,000. Kwa hiyo ni eneo zito na kubwa. Tukiwa na Bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi hao, tunategemea tutakuwa na Ukanda ambao utakuwa na nguvu kiuchumi, kijamii na katika mambo yote ambayo yanategemewa. Kwa hiyo, tunawaomba mtusaidie tuungane sote kama Bunge, tuliunge Azimio hili ili liweze kutupatia manufaa makubwa. Sihitaji kuingia kwenye manufaa ni mengi na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, ameyataja yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge watusaidie, watuunge sisi Wajumbe walioupeleka ili tuweze kulipeleka hili suala. Ninaomba niseme Mheshimiwa Spika kwa leo ni Mjumbe kwenye Kamati ya Utendaji. Kwa kweli, tulikuwa tunafadhaika anapokaa kwenye Kamati ya Utendaji, tunafika Tanzania ndio pekee kati ya nchi tatu amabazo hazijaridhia. Mimi mwenyewe nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati, ambayo ndiyo chimbuko la Azimio hili. Unapokuwa Mwenyekiti, unakaa kwenye Kiti, nchi yako haijaridhia, unapata tatizo sana. Nimefarijika sana leo Azimio limekuja na ninashukuru kwamba, Wabunge nina hakika mtatuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Sasa ninaomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati, ili aweze *ku-wind up*. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tafadhalii.

MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMABO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kutoa shukrani na kumtambua mchangiaji mmoja tu aliyechangia hoja yetu; Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Sikupata michango ya maandishi. Kwa hiyo, nitazungumza kwa muda mfupi. Tunazipokea pongezi na shukrani za Mheshimiwa Dr. Willbroad Slaa, kwa ushirikiano tuliopatia na yeze anaoendelea kutupatia. Ninapenda tu kumhakikishia kwamba, suala la gharama, Kamati yetu haikulizungumzia kwa makusudi; kwa sababu kinachojadiliwa mbele ya Bunge hili Tukufu ni kusudio la kuanzisha Bunge. Uamuzi utafanywa na Viongozi wakuu wa Nchi na Serikali Wanachama wa *SADC*. Kwa hiyo, wakiongeza gharama, sisi Bunge tutazipokea na ni jukumu letu kuamua ziwe nydingi ziongezeke, umuhimu wa jambo lenyewe ndiyo hasa jambo la msingi la kuzingatiwa, hatimaye na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba, hii ni hoja ya Kamati, sio hoja ya wawakilishi wetu ndani ya *SADC*, kwa hiyo ni hoja ya Bunge zima. Wabunge wote tunaiunga mkono kwa sababu ni Azimio la Bunge. Kwa hiyo, tupo pamoja na wewe na hii ni sehemu ya Bunge, limeshatufikia ndio maana nikataja Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge; fasili ya 9(2)(b). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawakilishi wetu nje katika Mabunge, kama Bunge la Afrika, *Pan African Parliament, SADC Parliamentary Forum* na *East African Legislative Assembly*, wanawajibika kuleta taarifa mbele ya Kamati yetu na sisi tukiridhika, mapendekezo yanayowasilishwa kwetu kwa niaba ya Bunge hili, wajibu wa Kamati ni kuleta maoni ili Bunge hili Tukufu liweze kuyaafiki na kuazimia. Nimefurahi sana, mmeafiki bila pingamizi, tunaenda vizuri. Nisipoteze muda, saa ya ku-wind up inakaribia.

Ninashukuru tena kwa kupata fursa na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kukubali Azimio lenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Uanzishwaji wa Bunge la SADC liliridhiwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na imeungwa mkono. Ninapenda kutangaza kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano sasa limeridhia Uanzishwaji wa Bunge la *SADC*. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Spika, ili tuweze kubadilishana hiki Kiti na kumalizia shughuli zilizobaki. (*Kicheko*)

Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu, toa taarifa.

DR. THOMAS D. KASHILILAH – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge hili, sasa zimekamilika.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia kwa ajili ya kupokea hoja ya kuliahirisha Bunge ni mfupi mno. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri wa Nchi au Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atoe hoja ya kutengua Kanuni ya 28(2) na (3), ili tuweze kuendelea hadi hapo Waziri Mkuu, atapohitimisha hoja yake. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu, atatoa Hotuba ya Kuhitimisha Mkutano huu wa Bunge; na kwa kuwa muda uliobakia hauwezi kuliwezesha Bunge kuendelea kumaliza shughuli hii; hivyo basi, Bunge lako litengue Kanuni ya 28(2) na (3), ili liendelee kukutana hadi Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

SPIKA: Hoja iliyo mbele yetu ni ya kutengua Kanuni ya 28(2) na (3), ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu, anayetoa hoja ya kulahirisha Bunge, aweze kuendelea hadi tuhitimishe hilo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ili Waziri Mkuu aendelee baada
ya muda ilipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Hoja imeafikiwa, sasa ninamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kulahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, shughuli za Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu, zinakamilika leo. Ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutulinda na kutuwezesha kukamilisha shughuli zote ambazo zilipangwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, ninapenda nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto, kupitia Chama cha Mapinduzi. Vilevile, ninampongeza kwa dhati, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuwapongeza Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Katika kipindi hiki kifupi, wameonyesha uwezo mkubwa katika kuliongoza Bunge vizuri. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa George B. Simbachawene, kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Chuo cha Ufundji Arusha na Mheshimiwa Prof. Feetham Filipo Banyikwa, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge kwenye Bunge la Afrika. Ninawataenia wote hawa, kila la kheri katika majukumu yaliyoko mbele yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, liliweza kujadili na kupitisha jumla ya Miswada saba ifuatayo: Muswada wa Sheria ya Usambazaji wa Petroli wa Mwaka 2007 (*The Petroleum Supply Bill, 2007*); Muswada wa Sheria ya Mikopo ya Ukodishaji Rasilimali wa Mwaka 2007 (*The Financial Leasing Bill, 2007*); Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 (*The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008*); Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO wa Mwaka 2008 (*The UNESCO National Commission Bill, 2008*); Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2008 (*The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008*); Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali za Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008 (*The Financial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008*); na Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 (*The Electricity Bill, 2007*).

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu pia lilijadili na kupidisha Maazimio mbalimbali yafuatayo: Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba Ulionanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 (*Protocol Ammending the Agreement Establishing the Inter-Governmental Standing Committee on Shipping – ISCOS, 2006*); Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Wakala wa Uwezesaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati (*Agreement for Establishment of the Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA*) wa mwaka 2006; Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Shirika la Kimataifa Linalosimamia Usafiri wa Anga Duniani (*ICAO*) wa Mwaka 2001 Kuhusu Vifaa Vinavyohamishika (*Convention on International Interests in Mobile Equipment*); Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Mkataba Kuhusu Masuala Maalum Yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika (*Protocol to the Convention on International Interests in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment*); Azimio la Kuridhia Mkataba wa Usalama, Amani na Maendeleo wa Ukanda wa Maziwa Makuu (*Pact on Security, Stability and Development in Great Lakes Region*); na Azimio la Kuunga Mkono Kuanzishwa kwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*Establishment of a SADC Parliament*).

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao wakati wa mjadala wa Miswada na Maazimio haya. Kazi ya msingi ya Bunge ni kutunga Sheria na hivyo, kupidishwa kwa Miswada na Maazimio hayo ni mafanikio ya Bunge letu Tukufu, kutimiza wajibu wake. Aidha, katika Bunge hili, jumla ya maswali 188 ya msingi yameulizwa na kupatiwa majibu, pamoja na maswali mengine mengi ya nyongeza. Ni imani yangu kuwa, Waheshimiwa Wabunge, wamepata maelezo ya kina kutoka Serikalini. Ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa ufasaha na umahiri mkubwa. Ninaamini kwamba, hii ni kazi nzuri ambayo ilitegemewa na wapiga kura wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, lilipokea na kukubali Taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, ikiwa ni pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo kwenye Taarifa hizo. Taarifa hizo ni Taarifa ya Hesabu za Serikali ya Mwaka 2005/2006 na Taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2005/2006. Aidha, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge, waliweza kupokea na kujadili Hoja Binafsi za Wabunge kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji na bei zake, ambavyo muda wake Kisheria unaishia mwaka 2009; Uuzwaji wa Nyumba za Serikali; Uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India; na Utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Containers Terminal Services (TICTS)*. Ninapenda nitumie nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, waliowasilisha hoja hizi na wote waliochangia wakati wa kuzijadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, ninaomba nielekeze hotuba hii ya kufunga Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge, kuelezea masuala mbalimbali muhimu yanayolikabili Taifa letu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Machi, 2008, kulitokea maafa makubwa kule Mererani, Mkoani Manyara, ambapo Wachimbaji Wadogo wa madini takriban 74, walifukiwa kwenye mashimo ya machimbo ya Migodi ya madini ya *Tanzanite* na kupoteza maisha. Hadi tarehe 24 Aprili, 2008 (jana), jumla ya miili 57 ilikuwa imeopolewa kutoka kwenye machimbo hayo. Aidha, Wachimbaji Wadogo wanne kule Chunya, nao walipoteza maisha baada ya kukosa hewa safi kwenye machimbo ya Mgodi wa dhahabu wa Matundasi. Roho za macheemu hawa wote, Mungu azilaze mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, matukio haya ya maafa katika migodi hii, yamesababisha kupotea kwa nguvukazi muhimu sana kwa Taifa. Sote tunajua kwamba, Watanzania wengi wanaofanya kazi za uchimbaji ni vijana wenyе umri kati ya miaka 16 na 35. Vijana walio katika umri huu ni nguvu kazi muhimu na mhimiili wa ukuaji uchumi kwa Taifa lolote. Kupoteza vijana wengi kiasi hicho kwa mara moja ni pigo kwa familia zao, lakini pia kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kupotea kwa maisha ya vijana wetu kwenye machimbo haya ni jambo la kusikitisha sana. Kama nilivvolieleza Bunge lako Tukufu, wakati nikijibu swalı la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, Siku ya Alhamisi tarehe 10 Aprili, 2008, matatizo ya Wachimbaji Wadogo ni makubwa na hivyo, yanahitaji Mkakati Maalum. Nimeielekeza Wizara ya Nishati na Madini, kwa kushirikiana na Wadau, kuanza mchakato wa kushughulikia matatizo haya. Lazima mpango utakaoandaliwa uzingatie Sera, Sheria na Kanuni zinazohusiana na Wachimbaji Wadogo. Kwa mfano, haifai kabisa kutoa leseni kwa Wachimbaji ambao hawajachukua hatua muhimu za tahadhari za kiusalama katika migodi.

Maisha ya watu hayawezi kufanyiwa majoribio, kwa vile tu wapo wamiliki wanaotaka kuchimba madini. Lazima usalama wa maisha ya Wachimbaji kwanza, utiliwe mkazo. Maafisa Madini waliopo katika Kanda mbalimbali nchini, nao wanahimizwa watimize wajibu wao na kusimamia utekelezaji wa Sheria kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mvua zinazoendelea kunyesha nchini katika baadhi ya maeneo zimekuwa nyingi na hivyo kusababisha mafuriko, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu, pamoja na njaa na athari nyingine kwa jamii. Kwa mfano, mwezi wa Januari 2008, sehemu ya Makuyuni, Mkoani Arusha, ilipata mafuriko na kusababisha madhara kwa watu na mali zao. Mwezi Machi, 2008, mafuriko mengine yalitokea katika eneo la Mto wa Mbu, Mkoani Arusha na eneo la Uchira la Lower Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Aidha, Wilayani Kyela, mafuriko yameleta madhara makubwa ambapo zaidi ya hekta 95.5 zimeathirika. Serikali katika ngazi za Wilaya na Mikoa, tayari imechukua hatua mbalimbali za kuwasaidia Wananchi walioathirika na mafuriko hayo. Aidha, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, limechukua hatua ya kupeleka vifaa vya kujenga daraja la dharura katika Mto Lufilyo, Wilayani Kyela. Serikali katika ngazi zake zote, itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali, kurejesha hali ya kawaida katika maeneo hayo. Serikali inawapa pole wananchi waliokumbwa na mafuriko haya katika kipindi hiki mfupi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mlima Oldonyo Lengai, umeendelea kulipuka kwa muda wa takriban miezi kumi mfululizo sasa. Kulipuka kwa *Volcano* ya Mlima huu, kumewaathiri Wananchi wanaoishi kwenye Vijiji vilivyo jirani na Mlima huo. Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi milioni 19 na mahindi tani 19.6, yenye thamani ya shilingi milioni 3.3, kwa ajili ya kuwasaidia Wananchi walioathirika na mlipuko wa *Volcano* ya Mlima wa Oldonyo Lengai. Timu ya wataalam, imefanya tathmini ya athari zake na taarifa hiyo imeshawasilishwa Serikalini. Kila jitihada itafanyika, kuwasaidia Wananchi wenzetu waliopatwa na majanga haya.

Nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa maeneo yaliyopatwa na maafa mbalimbali, kwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia Wananchi walioathirika. Aidha, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa mchango wa shilingi milioni 17.5 kwa waathirika wa Mererani. (*Makofsi*)

Niyashukuru pia Majeshi yetu, kwa jinsi walivyojitolea kusaidia kukabiliana na maafa yaliyotupata hasa kule Mererani na Kyela. Kipekee kabisa, niwashukuru Wana-Apollo wote wa Mererani, kwa jitihada kubwa walizofanya, kuopoa miili ya wenzao waliofia kwenye Mgodi wa Mererani. Sote tulishuhudia jinsi vijana wetu hawa, walivyofanya kazi hiyo kwa bidii, licha ya kuwa na zana duni na mazingira magumu ya migodi yenye ya Mererani. Aidha, niyashukuru sana makampuni, watu binafsi na wananchi kwa ujumla, ambao walitoa michango yao kuwasaidia wahanga wa maafa haya. Taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara ya hadi tarehe 24 Aprili, 2008, inaonyesha kuwa, jumla ya fedha taslimu zilizopokelewa zimefikia shilingi 210,528,000, tunawashukuruni sana kwa michango hiyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kukabiliana na maafa si la mara moja. Aidha, suala hili sio la kungoja maafa yatokee, ndipo kuanza kukabili madhara yake. Kukabiliana na maafa ni mchakato unaoanzia kwenye kuzuia. Wataalam wanasesma: "Kinga ni Bora Kuliko Tiba." Kwa maana hiyo, katika kuchukua tahadhari dhidi ya maafa ni lazima wananchi wapate taarifa sahihi za tahadhari juu ya maafa yanayoweza kutokea. Tunaelewa kwamba, nchi yetu ina eneo kubwa sana kijografia, ambalo lina ugumu wa mawasiliano. Kwa maana hiyo, si rahisi sana kwa wananchi wote kupata taarifa kupitia Vyombo vya Habari. Kwa misingi hiyo ni lazima Mamlaka zilizopo kwa mfano, Mamlaka ya Hali ya Hewa, zitoe taarifa za utabiri wa Hali ya Hewa na tahadhari kuhusu kutokea kwa majanga kama mafuriko kila mara na kwa usahihi mkubwa inavyowezekana. Taarifa kama hizi, zinahitaji kuwafikia Wananchi katika maeneo yote ili wachukue tahadhari za kutosha.

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa tuwe na utaratibu wa mawasiliano kwa karibu sana, kati ya Mamlaka ya Hali ya Hewa na Kamati za Maafa, kwa ajili ya kupeana taarifa. Ninaelewa kwamba, Wilaya zote zimeshaunda Kamati za Maafa na mafunzo yameshatolewa kwa Maafisa katika Mikoa 13 na Wilaya zake. Kamati hizi zihakikishe kwamba, zinatumia njia mbalimbali kufikisha ujumbe kwa Wananchi. Vilevile ni dhahiri, Vyombo vya Habari pekee havitoshi. Kwa mfano, mikutano ya hadhara, inaweza kutumika kupashana habari na kuwaandaa wananchi kujikinga na maafa. Njia hii inaweza kusaidia sana kufikisha taarifa katika ngazi za chini. Aidha, Mamlaka ya

Utabiri wa Hali ya Hewa, iangalie uwezekano wa kutumia huduma ya ujumbe mfupi wa simu za mikononi, zinazotolewa na makampuni ya simu yaliyopo hapa nchini. Makampuni haya yana uwezo mkubwa sana wa kutoa habari kwa wateja wao wote, kwa wakati mmoja. Nina imani kwamba, kama tutayatumia Makampuni haya, watu wengi wanawenza kupata habari za tahadhari dhidi ya maafa kwa haraka sana. (*Makofii*)

Vilevile, Waheshimiwa Wabunge, mnao mchango mkubwa katika suala hili. Ninii mpo karibu na wapiga kura wenu, mnapata taarifa mbalimbali, kutoka Vyombo vya Habari na mawasiliano ya kisasa, hivyo mnawenza kuzifikisha haraka kwa wananchi mnaowawakilisha. Wito wangu kwenu, tusaidiane katika kupashana habari. Aidha, tukipata habari tusizipuuze. Wachina wanasema katika methali yao moja kwamba: "Hata mchwa anaweza kuharibu maji ya Bwawa." Wenzetu hawa wanaamini kwamba, mchwa anaweza akajenga kidogo kidogo katika kuta za bwawa na kusababisha ucharibifu mkubwa. Kwa maneno mengine, tatizo dogo la kupuuza taarifa, linawenza kugeuka na kuwa tatizo kubwa, linaloweza kusababisha janga la Kitaifa. Kwa maana hiyo, tukiweza kutumia vizuri taarifa zitakazopatikana, tunawenza kupunguza athari za maafa ambazo zinawenza kutokeea. Idara ya Kuratibu na Kudhibiti Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, itaendelea kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Mamlaka ya Hali ya Hewa na Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya, kuhakikisha kwamba, taarifa zinazopatikana zinawafikia Wananchi kwa haraka na kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maafa ya migodini na mafuriko, wapo Wananchi waliofariki katika ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri. Ajali hizo zimesababisha vifo, ucharibifu wa mali na pengine ulemavu. Kwa mfano, ajali za magari zilizotokea hivi karibuni Mkoani Tanga na Dodoma na maeneo mengine nchini. Ninachukua fursa hii, kutoa pole kwanza, kwa wafiwa wote walipoteza ndugu na jamaa zao na kuwatachia afya njema wote walijeruhiwa. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya Sekta ya Elimu, ambayo Serikali imekuwa ikifanya, yameanza kuonyesha matunda mazuri. Tumeshuhudia kiwango cha kufaulu wanafunzi katika Shule za Msingi, kikiendelea kukua mwaka hadi mwaka. Mfano, mwaka 2004 kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 48.7, mwaka 2005 asilimia 61.8 na mwaka 2006 asilimia 70.5. Vilevile, kutokana na juhudhi kubwa za Wananchi na Serikali, kumekuwepo na kasi kubwa ya ujenzi wa Shule mpya za Sekondari karibu katika kila Kata nchini. Idadi ya Shule za Sekondari, imeongezeka kutoka 1,202 mwaka 2005 hadi kufikia 2,861 mwezi Machi, 2008.

Kutokana na jitihada hizo, lipo ongezeko kubwa la Wanafunzi wanaochaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza. Mfano, mwaka 2005 Wanafunzi waliojiunga na Kidato cha Kwanza walikuwa 134,963 na imeongezeka hadi Wanafunzi 401,011 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 197. Mwaka 2008 Wanafunzi waliochaguliwa walikuwa 392,547. Mafanikio haya ni dhahiri, yameanza kuleta changamoto kubwa kwa Serikali na Wadau wa maendeleo, kutafakari upya kuhusu umuhimu wa kuongeza nafasi za Kidato cha Tano na Sita ili kuwezesha Wanafunzi wanaofaulu Kidato cha Nne kupata

nafasi. Changamoto hii imeanza kujitokeza mwaka huu wa 2008, hata kabla ya kutimia miaka mitano tangu kuanza kwa zoezi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii, kufafanua changamoto inayotokana na Matokeo ya Kidato cha Nne. Katika mwaka 2007, wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne katika Shule za Sekondari za Tanzania Bara walikuwa 115,302. Wanafunzi waliofaulu kuijunga na Kidato cha Tano walikuwa 41,168, sawa na asilimia 36 ya wanafunzi waliofanya mtihani. Hili ni ongezeko la wanafunzi 11,467, ikilinganishwa na mwaka 2006. Wanafunzi waliochaguliwa kuingia Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari za Serikali ni 24,946, sawa na asilimia 22 ya waliofanya mtihani na ni sawa na asilimia 60.6 ya Wanafunzi waliofaulu.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha kuwa, Wanafunzi 16,222, sawa na asilimia 39.40 ya wanafunzi waliofaulu, wamekosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari za Serikali. Hii ina maana kuna uhaba wa nafasi 16,222 katika Shule za Kidato cha Tano na Sita zilizopo. Ingawa baadhi ya wanafunzi wanawenza kuchukuliwa na sekondari za binafsi zenyenye nafasi 15,000 na Vyuo vya Ualimu vyenye nafasi 6,000, bado Serikali ina jukumu la kuongeza Shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita. Hivyo, ni jukumu la kila mmoja wetu, kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanaendelea na masomo ili wasiishie hapo walipo. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya, imeanza kuchukua hatua zitakazowezesha kukabiliana na tatizo hili, ikiwemo kuongeza shule zaidi za Kidato cha Tano na Sita. Serikali itaelezea kwa kina, mikakati hiyo katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, uhaba huu unatokana na ufaulu wa asilimia 36 tu. Kama ufaulu ungekuwa mkubwa zaidi, uhaba nao ungekuwa mkubwa zaidi ya hapo, kwani wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne, wanatarajiwa kuongezeka kila mwaka na kufikia 326,935 mwaka 2010. Ikiwa kiwango cha kufaulu kitabaki kile kile na nafasi zilizopo mashulenzi zikabaki kuwa 24,946, wanafunzi watakaokosa nafasi wataongezeka kutoka 16,222 mwaka 2007 hadi 92,750 mwaka 2010. Serikali imeliona hilo na sasa inachukua hatua za maandalizi ya mpango wa kukabiliana na tatizo hili, kama Bunge lako Tukufu lilivyoarifiwa katika Mkutano huu. Katika Mpango huo wa Serikali, kila Wilaya inatakiwa kutayarisha shule mbili za kitaifa, moja ya wasichana na moja ya wavulana, kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita kuanzia mwaka 2009. (*Makofi*)

Vilevile shule chache za Kata, zitaongezewa majengo na vifaa ili ziweze kukidhi vigezo vya kuwa Kidato cha Tano na Sita. Ninapenda kuchukua fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuwa kichocheo katika Wilaya zenu cha kufikia malengo yetu katika elimu. Tushirikiane kuwahamasisha Wananchi kuhakikisha shule hizo zinajengwa ili ziongezeke katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi, katika miaka ya hivi karibuni, nchi yetu imekuwa na mwelekeo wa kukosa Wanasyansi ambaao ni watu muhimu katika maendeleo ya Taifa lolote. Ushahidi wa hili, unaweza kuonyeshwa na ulinganisho wa kufaulu wa masomo ya Sayansi na Sanaa katika Shule za

Msingi na Sekondari. Kushuka kwa kiwango hiki cha kufaulu masomo ya sayansi, kunathibitishwa na takwimu za Baraza la Mitihani Tanzania, ambazo zinaonyesha kwamba, ufaulu wa masomo ya sayansi na sanaa kwa Shule za Msingi na Sekondari, kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2003 - 2007 umeshuka sana. Ningependa kutoa mifano michache na takwimu katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nikianza na Shule za Msingi; Taarifa inaonyesha kuwa, kiwango cha kufaulu kwa hisabati kimeshuka kwa asilimia 28.4 kati ya mwaka 2006 na 2007 peke yake. Tukianzia mwaka 2003, idadi ya watahiniwa ilikuwa 489,908 na kiwango cha kufaulu kwa somo la hisabati kilifikia asilimia 63.6. Mwaka 2004 kikafikia asilimia 33.4, mwaka 2005 asilimia 47.0 na mwaka 2006 asilimia 45.8. Mwaka 2007, hali ilibadilika sana. Katika watahiniwa 773,120 ni asilimia 17.4 tu ya watahiniwa ndio waliofaulu somo la hisabati. Hali hii imechangiwa na shule nyingi za msingi, kukabiliwa na upungufu wa Walimu wa somo la hisabati. Vilevile, viwango vya kufaulu masomo ya sayansi na maarifa ya jamii kwa watahiniwa vimeshuka zaidi mwaka 2007, ikilinganishwa na mwaka 2006. Kwa mfano, kwa upande wa somo la sayansi, kiwango kimeshuka kutoka ufaulu wa asilimia 80.3 mwaka 2006 kwenda asilimia 66.7 mwaka 2007. Katika somo la maarifa kiwango kimeshuka kutoka asilimia 70.9 mwaka 2006 kwenda asilimia 56.4 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika kushuka kwa ufaulu wa Masomo ya Hisabati na Sayansi, wasichana ndio wameathirika zaidi ikilinganishwa na wavulana. Kwa mfano, ufaulu wa wavulana kwa somo la hisabati mwaka 2003 ulikuwa asilimia 69.9 ikilinganishwa na asilimia 57.3 ya wasichana. Kwa mwaka 2007 ufaulu wa wavulana ulishuka na kufikia asilimia 23.4 wakati kwa wasichana ulifikia asilimia 11.1. Zipo jitihada za Serikali kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili ambazo nitazieleza hivi punde.

Mheshimiwa Spika, katika Shule za Sekondari kiwango cha kufaulu katika somo la hisabati pia ni cha chini, ukilinganisha na masomo ya sanaa na masomo mengineyo ya sayansi (Fizikia, Kemia na Biolojia). Kwa mfano, ufaulu wa mwaka 2003, somo la hisabati ulikuwa asilimia 26.9 ikilinganishwa na fizikia asilimia 56.8, kemia asilimia 65.1, biolojia asilimia 57.9 na jirografia asilimia 61.7. Mwaka 2004 ufaulu wa hisabati ulikuwa asilimia 29.9; mwaka 2005 asilimia 23.4, mwaka 2006 asilimia 23.4 na mwaka 2007 asilimia 31.3. Kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa somo hili, kunachangiwa na watahiniwa kuwa na msingi mbaya wa somo la hisabati tangu wakiwa katika Shule za Msingi. Fizikia na kemia hayafundishwi moja kwa moja katika Shule za Msingi, bali huanza kufundishwa katika Shule za Sekondari. Hivyo, inawezekana mtoto aliyepata msingi mbovu wa hisabati katika Shule za Msingi, anaanza kujenga chuki na somo hilo tangu mwanzo.

Mheshimiwa Spika, katika Kidato cha Sita, watahiniwa wanaonyesha kufaulu vizuri katika masomo yote, ijapokuwa katika somo la fizikia kiwango cha kufaulu kimeshuka kwa asilimia 20.2 kati ya 2006 na 2007. Mwaka 2006, kiwango cha kufaulu somo la fizikia kilikuwa asilimia 79.9 na mwaka 2007 kilikuwa asilimia 59.7. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa wanafunzi wa kuingia Kidato cha Tano, umezingatia ulinganishaji wa jinsia katika elimu nchini. Katika uchaguzi huo, wawulana waliochaguliwa ni asilimia 53.9 tu ya wawulana 26,590 waliofaulu wakati wasichana waliochaguliwa ni asilimia 72.7 ya wasichana 14,578 waliofaulu. Hata hivyo, bado tunahitaji kuweka uwiano huo kimasomo. Kwa mfano, wakati asilimia 46.2 ya wawulana waliochaguliwa wamejiunga na masomo ya sayansi ni asilimia 30.2 tu ya wasichana waliochaguliwa ndio waliojiunga na masomo ya sayansi. Huo ni uthibitisho kwamba, wawulana bado wanaendelea kuwa wengi zaidi katika nyanja za sayansi nchini. Hatuna budi kujenga mazingira mazuri na kutoa motisha kwa wanafunzi wa kike kupenda kusoma masomo ya sayansi. Aidha, hatuna budi kuondoa dhana kuwa, masomo ya sayansi ni masomo yanayohitaji nguvu hivyo ni ya wawulana. Kila mzazi na kila mwananchi, ashiriki katika kuwajengea wasichana msingi mzuri nyumbani na shulenii wa kusoma masomo ya sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali ya masomo ya sayansi mashulenii si nzuri hata kidogo. Nchi zilizopiga hatua kubwa sana kimaendeleo, ziliwekeza katika elimu na kipaumbele kikawekwa katika kuimarisha Taasisi za Teknolojia zinazohimiza ubunifu. Katika miaka ya hivi karibuni, Nchi ya Marekani imekuwa ikichukua hatua za kurudisha hadhi yake katika masomo ya sayansi na hisabati, baada ya kugundua kwamba, imepitwa sana na nchi nyingi. Marekani ilijikuta ikiwa nchi ya 21 duniani, kwenye ushindani wa wanafunzi wenyewe vipaji katika somo la hisabati. Hali hii iliwfanya washtuke na kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo hili. Walifanya hivyo kwa sababu wanajua umuhimu wa sayansi na kuwa na Wanasayansi ni bora. Takwimu hizi za hapa kwetu, nazo zinatupa onyo kwamba, tuchukue tahadhari kabla mambo hayajafika kwenye hali mbaya zaidi. Kwa hiyo, tunavyofanya mageuzi haya makubwa ya elimu, suala la msisitizo katika masomo ya sayansi ni la muhimu sana kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tukabiliane kwa nguvu zote na changamoto hii kubwa ya kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika masomo ya sayansi. Ninaelewa kabisa kwamba, masomo ya sayansi yanahitaji mwanafunzi aweze kujifunza na kutahiniwa kinadharia na kwa vitendo zaidi ili aweze kutafakari yeeye anayojifunza na kujenga utayari wa kujifunza zaidi. Hata hivyo, shule nyingi zina upungufu wa maabara za kufanya majoribio ya kisayansi na wataalam wenyewe taaluma ya kutosha katika kufundisha masomo haya kwa vitendo. Aidha, shule nyingi zina upungufu wa Walimu wa Hisabati hasa katika shule za msingi.

Vilevile, lipo tatizo la wanafunzi kujifunza kwa kukariri zaidi masomo ya sayansi na hisabati kwa lengo la kufaulu mtihani tu. Matokeo yake, inaathiri upatikanaji wa wataalam wenyewe kuelewa nadharia na vitendo. Hapa inanikumbusha kisa cha Mwanafunzi Mtaalam wa Kilimo, ambao tunawajua kwa majina; Mabwana Shamba Mtarajiwa, ambaye alikwenda kwa mkulima mmoja kijijini. Katika kumshauri mkulima huyu, mwanafunzi alimwambia yule mkulima: “Mbinu unazozitumia katika kilimo chako hiki ni mbinu za kizamani sana. Sitaona ajabu kama mti huu utakupatia chini ya kilo 20 za mapeasi.” Mkulima yule akamwangalia mtaalamu yule kwa mshangao, naye akamwambia: “Nami kwa kweli sitashangaa kwa vile mti huu ni wa machungwa sio wa mapeasi.” (*Kicheko*)

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, tuwe makini. Tujenge uwezo wa wataalam wetu, wapate elimu ya kutosha kuwawezesha kutoa ushauri pasipo kubahatisha. Tuweke kipaumbele katika masomo ya hisabati na sayansi ili kupanua upeo wa wataalam wetu katika kuwashauri wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kutafuta ufumbuzi wa suala hili kwa umakini kabisa. Kwa kuanzia, Taasisi ya Elimu Tanzania, imeboresha mitaala ambayo inalenga kumjengea mwanafunzi uwezo wa kufikiri na kujifunza kwa kina. Mitaala hiyo, imeanza kutumika tangu 2005. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania, limeandaa na kuendesha Programu ya Mafunzo ya Watunzi na Warekebishihi wa Maswali ya Mitihani. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa mabadiliko ya mitaala kuanzia Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu. Mitihani hiyo, itaanza kutahini wanafunzi mwaka 2008 kwa Shule za Sekondari, 2009 kwa Vyuo vya Ualimu na 2011 kwa Shule za Msingi. Baraza la Mitihani la Tanzania, linatarajia kutoa maswali ya mitihani yanayopima uwezo (*competence*), badala ya maudhui (*content*) tu; na hivyo itamlazimu mwalimu na mwanafunzi kuwa wabunifu katika kufundisha na kujifunza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo ni lazima tukabiliane na tatizo la msingi la upungufu wa walimu wa hisabati kuanzia Shule za Msingi. Sote tunaelewa kwamba, msingi mbovu hauwezi kuhimili nyumba. Tukishaacha watoto wetu wa Shule ya Msingi wakawa na msingi mbovu wa hisabati, upo uwezekano mkubwa; wakalichukia somo hilo kwa sababu wanaingia Sekondari wakiwa tayari hawalipendi somo la hisabati na mengineyo. Aidha, kuna uhaba mkubwa walimu. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa, mahitaji ya Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati katika Shule za Sekondari kwa mwaka 2007, yalikuwa 23,407. Walimu waliopo ni 6,277. Hii ni asilimia 26.8 tu. Hivyo, kuna upungufu wa Walimu 17,130, sawa na asilimia 73.2. Katika Vyuo vya Ualimu, mahitaji ya Wakufunzi wa Masomo ya Sayansi na Hisabati kwa mwaka 2007 yalikuwa 540. Wakufunzi waliokuwepo ni 153, sawa na asilimia 28.3. Kwa hiyo, kuna upungufu wa Wakufunzi 387, sawa na asilimia 71.7.

Kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba, bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kutufikisha pale tunapotaka kwenda. Katika mkakati mzima wa kuboresha elimu, suala la kuongeza idadi ya Walimu wakiwemo wa Hisabati kwa Shule za Msingi limezingatiwa. Serikali imeweka upendeleo maalum katika kuwachagua wanafunzi, wanaoomba kusomea Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati. Aidha, katika Vyuo Vikuu, nafasi za walimu wa masomo haya zitaongezwa kutoka 1,130 mwaka 2007 hadi 1,945 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, tunalo jukumu kubwa la kujenga umuhimu wa kukuza masomo ya sayansi katika shule zetu kuanzia Shule za Msingi hadi Sekondari. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliwahi kusema: "Uchumi wa kisasa ni ule unaoendeshwa kwa kutumia maarifa, yaani kwa Sayansi na Teknolojia." Tutafanikiwa vizuri, kama watoto wetu watakuwa wamesoma vizuri masomo ya Sayansi na Hisabati. Wito wangu kwa Viongozi wa Mikoa

na Wilaya ni kuhakikisha kwamba, tunahimiza elimu hiyo kwa nguvu sana na kwa wazazi tunawahimiza vilevile wasaidie kutoa msukumo mkubwa kwa watoto wao kupenda masomo haya.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kukabili ana changamoto za kupanua Elimu ya Sekondari katika ngazi ya Kidato cha Tano na Sita, yameleta changamoto kubwa katika upanuzi wa Elimu ya Juu. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, kifungu 63; Serikali imelenga kuwezesha asilimia 12.5 ya watakaomiliza Kidato cha Sita, kuendelea na masomo ya Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa misingi hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, itaongeza nafasi katika Vyuo Vikuu kutoka 49,967 mwaka 2008 hadi 79,807 ifikapo mwaka 2012. (*Makofit*)

Hata hivyo, Vyuo Vikuu vya Umma (*Public Universities*), kwa sasa vinakabiliwa na matatizo makubwa kwenye miundombinu, upungufu wa vitabu, majarida na vifaa vingine vya kujifunzia; na Wahadhiri na Wataalamu wengine. Miundombinu ikiwemo majengo na mifumo ya maji na umeme iliyopo, inahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa sababu imetumika kwa muda mrefu, bila kufanyiwa ukarafati wa kawaida. Aidha, kuna msongamano mkubwa katika mabweni, kumbi za mihadhara, vyumba vya madarasa, karakana, mактaba na hata *cafeteria*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuvinusuru Vyuo Vikuu, wakati inafanya maandalizi ya kuanza utekelezaji wa Elimu ya Juu au MEJU. Katika hatua ya kwanza, Serikali inaangalia uwezekano wa kupata shilingi bilioni 5.4 za dharura mwaka huu wa fedha 2007/2008, ambazo zimeombwa na Wizara, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Fedha hizo zinajumuisha kumlipa mkandarasi, kununua vifaa vya maabara, pamoja na vifaa vya Karakana ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Aidha, zitatumika kuweka umeme wa kujenga na kujenga *cafeteria* ndogo katika Hosteli ya Chole ya Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili; na kusaidia kulipa sehemu ya deni kubwa la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Aidha, Serikali imeunda kamati inayoangalia upya, Mfumo wa Pensheni wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Umma. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, upanuzi wa Elimu unaofanyika unaongeza pia changamoto kwenye Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Changamoto kubwa ni pamoja na ufinyu wa Bajeti na mfumo wa mchakato wa kuteua Wanafunzi wanaostahili kupata mikopo ya Elimu ya Juu. Malalamiko mbalimbali, yamekuwa yakitolewa kuhusu ucheleweshaji wa kushughulikia maombi ya wanafunzi na idadi ndogo ya wanaonufaika na huduma hiyo. Aidha, kasi ndogo ya urejeshaji wa mikopo, inapunguza uwezo wa kutoa huduma ya mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaangalia upya muundo na shughuli za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ili kuona namna ya kuboresha huduma zinazotolewa na Bodi hiyo. Aidha, Serikali pamoja na mambo mengine, itaboresha Sheria ya *The Higher Education Students Loans Board Act No. 9 of 2004*, kwa kutekeleza marekebisho ya Mwaka 2007 na Kanuni za Bodi ya Mikopo za mwaka 2008. Vilevile,

Bodi itafungua Ofisi za Kanda na Mikoa ili kurahisisha usambazaji, ukusanyaji na ufuatiliaji wa fomu za mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Wananchi wataelimishwa zaidi kuhusu upimaji wa wanaostahili mikopo, unaojulikana kama *means testing*, ambao bado utaendelea kutumika ili uwe sahihi na makini zaidi kwa lengo la kuepusha malalamiko kutoka kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingi duniani, inakabiliwa na itaathirika sana na kupanda kwa bei ya vyakula duniani. Bei ya vyakula, imekuwa ikipanda sana duniani kote kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kuongezeka kwa mahitaji ya chakula duniani, ukame na kupanda kwa gharama za uzalishaji kulikosababishwa na kuongezeka kwa bei ya mafuta. Aidha, bei zimepanda kutokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula, unaosababishwa na baadhi ya mashamba kutumika kuzalisha mazao yanayotumika kuzalisha nishati mbadala itokanayo na mimea. Inakadirwa kwamba, mahitaji ya nafaka duniani, yataongezeka na kufikia tani milioni 2,126 kwa msimu wa mwaka 2007/2008, ongezeko la asilimia tatu ikilinganishwa na ya msimu wa 2006/2007. Ongezeko hili, limesababishwa na ongezeko la watu hasa katika nchi zinazoendelea. Aidha, katika msimu huu, kumetokea ongezeko kubwa la matumizi ya nafaka kuzalisha nishati.

Kwa msimu wa 2007/2008, inakadirwa kwamba, tani milioni 100 za nafaka zikiwemo tani milioni 95 za mahindi, zitatumika kuzalisha nishati. Hali hii imezifanya bei za nafaka duniani kupanda sana. Wataalam wa Shirika la Kilimo na Chakula Duniani na Benki ya Dunia, wanasema kwamba, bei ya vyakula kwa miaka kumi ijayo, itakuwa juu kulinganisha na miaka kumi iliyopita. Aidha, bei za vyakula zinatarajiwaa kufikia kilele chake kati ya mwaka 2008 na 2010 na kuanza kushuka kwa kiwango kidogo kidogo baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa nchi yetu inajitosheleza kwa chakula kila msimu, tusingkuwa na wasiwasni sana na kupanda kwa bei hizi. Lakini historia yetu inatuonyesha kwamba, kukitokea ukame msimu mmoja tu, tunakumbwa na njaa hata kama misimu iliyotangulia tulivuna kwa wingi. Tafsiri hii ya upandaji bei ya vyakula ni kwamba, kama hatutaweza kuvuna chakula cha kutosha, kukihifadhi na kukisafirisha kwenda sehemu zenye uhaba wa chakula, tutalazimika kuagiza chakula nje. Tutalazimika kununua vyakula kwa bei kubwa nje ya nchi ili tulishe watu wetu. Aidha, kama tutachukua tahadhari mapema, tutaweza kabisa kujilinda dhidi ya upandaji huu wa bei. Tahadhari tunazoweza kuchukua ni pamoja na kuongeza uzalishaji, kuhifadhi chakula wakati wa msimu mzuri na kutengeneza barabara za vijiji ili zipitike wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa miaka kadhaa, imekuwa ikitoa ruzuku ya mbolea ili kuwaweweza wakulima kuzalisha zaidi. Mahitaji ya mwaka mzima ya mbolea ni tani 385,000. Mwaka 2006/2007, jumla ya tani 287,655 zilipatikana na kusambazwa kwa Wakulima. Kati ya hizo, tani 89,000 ziliikuwa ni mbolea ya ruzuku. Mwaka 2007/2008, mbolea ya ruzuku ilikuwa tani 91,370. Hadi Machi, 2008, jumla ya tani 62,691 ziliikuwa zimesambazwa mikoani. Pamoja na hilo, Mfuko wa Pembejeo ulioanzishwa unaendelezwa ili kusaidia wakulima kukopa pembejeo za kilimo.

Ninatambua kwamba, bado kuna uhaba mkubwa wa pembejeo, lakini bado inawezekana kuongeza ufanisi katika hali hiyo na kupunguza kwa kiasi kikubwa, athari zinazoweza kutokea kutokana na bei zinazoendela kupanda za chakula. Serikali inaangalia utaratibu unaoweza kutumika, kukiimarisha kiwanda chetu kinachozalisha mbolea cha Minjingu ili kuweza kusaidia usambazaji na upatikanaji wa mbolea hapa nchini kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, tunapotoka katika Bunge hili, tujue tunayo changamoto kubwa ya kuanza kufikiria namna ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu upandaji huu wa bei za vyakula na tafsiri yake kwa uchumi wetu. Wananchi wahimizwe kuzalisha chakula cha kutosha na kuhifadhi ziada ya kutosha katika ngazi ya kaya hadi msimu mwengine unapoanza. Aidha, itakuwa ni jambo bayo sana kuuza chakula kwa bei rahisi leo, halafu kesho tununue kwa bei ghali. Tuliangalie hili kwa mtazamo huo. Kama suala kubwa ni lile la kuhifadhi chakula kutokana na miundombinu hafifu ya uhifadhi ni lazima sasa tuanze kushirikiana na wananchi kujenga maghala ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, haitoshi tu kusikitika na kulalamikia kupanda kwa bei ya vyakula duniani; kupanda kwa bei ni changamoto kwetu. Kama nchi yenye ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, rasilimali watu, sera na miongozo ya kilimo, tunaweza kujipanga na kuzalisha kwa wingi ili tuuze nje na kupata fedha za kigeni. Ninaamini kabisa kwamba, tunaweza kuzalisha kwa wingi na kupata ziada kuuza chakula nje. Ndio maana ninasema, kupanda kwa bei ya vyakula kuwe chachu ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, mazao ya chakula ni biashara ambayo ina uhakika wa soko. Hivyo, tuwahimize wananchi watambue kuwa “Chakula ni Biashara” ya uhakika na inayolipa. Kwa mfano, Nchi ya Vietnam katika mwaka 2007, iliuza nje tani milioni nne na nusu za mchele. Kwa wastani wa bei za mwaka jana ambapo tani moja ilikuwa Dola za Marekani 300, nchi hii iliingiza zaidi ya Dola za Marekani milioni 1,350 kwa kuuza mchele tu. Watanzania tuna uhakika wa kuzalisha vyakula vya aina zote tukajitosheleza na tukauza ziada nje. Jukumu kubwa la Serikali ni kutengeneza Mkakati unaotekelzezka, utakaoonyesha kwa kina, mahitaji halisi ya kufikia hatua ya kuzalisha ziada, kuhifadhi na kuuza nje ili kupata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya chakula.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuzalisha na kuuza ziada nje ni lazima tufikirie kilimo cha kibashara. Kilimo cha biashara kinahitaji uwekezaji wa kutosha. Ili uwekezaji huu uweze kufanyika ni lazima kuwepo na ardhi ya kutosha kufanyia biashara ya kilimo. Pamoja na kwamba, tumeweza kuvutia wawekezaji katika sekta nyingi, uwekezaji katika kilimo umekuwa ukisucasua sana. Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba, Tanzania ina hekta milioni 44.0 na kati ya hizo zinazotumika ni hekta 10.8 tu, sawa na asilimia 24.5. Aidha, nchi yetu inazo hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji ; kati ya hizo zinazotumika kwa Kilimo cha Umwagiliaji ni hekta 280,000 tu, ambayo ni sawa na asilimia moja. Kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba, nchi yetu ina ardhi kubwa sana inayofaa kwa kilimo, lakini tumeweza kutumia sehemu ndogo sana. Zipo sababu za uduni wa zana za kilimo, ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji, barabara zinazopitika wakati wote, uhaba wa masoko ya uhakika na miundombinu ya barabara. Njia mojawapo itakayosaidia kuanza kwa kilimo kikubwa ni

kutenga ardhi na kuruhusu watu wenye mitaji, waweze kuwekeza kwenye kilimo cha biashara (*Large Scale Farming*). Sijui kama tunaweza kukwepa hili? Imani yangu ni kwamba, kama tutakuwa na mikataba mizuri ya biashara kama hii ya kilimo, itatusaidia kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa wananchi wetu walio wengi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna wale wanaodhani kwamba, kukaribisha wawekezaji kwenye kilimo ni kuuza ardhi. Hapana! Suala la msingi hapa ni mikataba ya ukodishaji ardhi kwa kilimo cha biashara, kitakachomwezesha Mwekezaji kurudisha gharama zake na Serikali kupata mapato yake. Sidhani kama kuna mmoja wetu hapa, asiyetambua umuhimu wa ardhi kwa wananchi wetu, lakini ardhi kukaa bila kutumika nayo ni gharama nyingine. Mimi ninaamini kabisa kwamba, tukiwekeza vyâ kutosha kwenye kilimo, tunaweza kujipatia mamilioni ya fedha za kigeni. Tukijitahidi na ninaamini tutafanikiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Februari, 2008 wakati nilipotoa hotuba yangu ya kuahirisha Mkutano wa Kumi wa Bunge lako Tukufu, niliahidi kuwa, Serikali itaunda Timu Ndogo ya Wataalam ili kuisadia Serikali kuchambua kwa makini na kupendekeza namna ya kutekeleza Maazimio 23 yaliyopitishwa na Bunge, wakati wa kuhitimisha mjadala wa Taarifa ya Kamati Teule iliyochunguza mchakato wa Zabuni ulioipa *Richmond Development Company LLC* ushindi wa kuzalisha umeme wa dharura nchini mwaka 2006. Pia, niliahidi kuwa, Kamati hiyo itazingatia yaliyomo kwenye Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge na Taarifa za majadiliano zilizomo katika kumbukumbu za Bunge, yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wataalam iliyoundwa na Serikali, imekamilisha kazi yake ya uchambuzi na kutoa mapendekezo ambayo tayari yamewasilishwa Serikalini. Kama nilivyosema awali, baada ya Serikali kupitia na kuchambua kila Azimio, imebainika kuwa, yapo Maazimio ambayo utekelezaji wake ni wa muda mfupi, lakini pia yapo Maazimio ambayo yatahitaji muda zaidi kidogo wa utekelezaji; hasa yale yanayohusu kurekebisha Sheria, Taratibu na mifumo mbalimbali ndani ya Serikali, pamoja na kujenga uwezo wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, maeneo ambayo yanaonekana yatahitaji muda mrefu wa utekelezaji ni yafuatayo: Kupitia upya baadhi ya Sheria na Taratibu, hususan zile zinazohusu masuala ya mikataba kwa ujumla, Sheria za Manunuzi na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Kuweka mifumo ya uwajibikaji wa Viongozi wa Umma na Watumishi wa Umma, pamoja na kuimarisha maadili; Kuimarisha uwezo wa Serikali katika majadiliano ya mikataba mbalimbali; Kujenga uwezo wa Watendaji wa Sekta ya Manunuzi; na Kuhuisha Muundo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (*PPRA*).

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, muda uliotolewa na Bunge kukamilisha zoezi hili ni miezi mitatu, kuanzia tarehe 15 Februari, 2008. Hivyo, ninapenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa, hivi sasa kazi ya uchambuzi wa Maazimio hayo imeshakamilika. Aidha, kila Wizara na Taasisi zinazohusika, tayari zimepewa maelekezo ya kuanza utekelezaji mara moja.

Nia ni kukamilisha utekelezaji wa Maazimio mengi katika kipindi kilichokusudiwa. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali itajitahidi kuharakisha utekelezaji wa Maazimio yote na Taarifa rasmi itawasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, mwezi Juni, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuzungumzia kwa ufupi sana suala la Umoja wa Afrika, kupeleka Majeshi Visiwi Comoro, kwa ajili ya kukikomboa Kisiwa cha Anjouan. Itakumbukwa kwamba, Visiwa vya Comoro vimekumbwa na machafuko ya mara kwa mara ya Mapinduzi ya Kijeshi. Hata hivyo, mwaka 2002, ulifanyika uchaguzi ambapo Kanali Azali Asouman, alichaguliwa kuwa Rais wa Comoro na Kanali Mohamed Bakari, kuwa Rais wa Anjouan.

Mwezi Mei, 2007, ulifanyika uchaguzi mwingine ambapo Bwana Ahmad Abdallah Sambi kutoka Anjouan, alichaguliwa kuwa Rais wa Muungano wa Visiwa vya Comoro, Bwana Mohamed Ally Said kuwa Rais wa Kisiwa cha Mwali na Bwana Mohamed Abdoulehabi kuwa Rais wa Kisiwa cha Ngazidja. Hata hivyo, kwa upande wa Anjouan, Kanali Mohamed Bakari, alikaidi kuondoka madarakani baada ya muda wake kumalizika. Kanali Bakari, alikataa kata kata kuruhusu Tume ya Umoja wa Afrika, kusimamia uchaguzi Kisiwani humo. Baada ya Kanali Bakari kugoma kuondoka madarakani, jitihada za Kidiplomasia na majadiliano ndani na nje ya Bara la Afrika, zilianza kumshawishi ili aweze kuachia madaraka baada ya muda wake kumalizika. Umoja wa Afrika, ulifanya jumla ya vikao tisa Cape Town – Afrika Kusini, Addis Ababa, Ethiopia na Motsamudu na Anjouan (Comoro), kujaribu kumshawishi Kanali Bakari kuachia madaraka, lakini alikataa.

Mheshimiwa Spika, baada ya jitihada zote za Kidiplomasia kuonekana zinashindwa, Rais wa Visiwa vya Comoro, Bwana Ahmed Abdallah Sambi, alipeleka ombi kwenye Mkutano wa Kumi wa Wakuu wa Nchi za Afrika, ulifanyika Addis Ababa, Februari, 2008 la kumwondoa kwa nguvu Kanali Bakari, Kisiwani Anjouan. Mkutano huo wa Wakuu wa Nchi za Afrika, ulikubali ombi hilo. Nchi nne za Libya, Senegal, Sudani na Tanzania, zilitaaliwa kuunda Kikosi cha Jeshi la Umoja wa Afrika, ambalo lingeendesha operesheni ya kumng'oa Kanali Bakari. Kuanzia tarehe 11 hadi 16 Machi, 2008, Tanzania na Sudan zilianza kusafirisha Majeshi kupeleka Comoro.

Mheshimiwa Spika, Operesheni ya Majeshi iliyojulikana kama “Operesheni Demokrasia Comoro” ilianza rasmi tarehe 24 Machi, 2008 na kukamilika kwa ufanisi mkubwa kesho yake tarehe 25 Machi, 2008. Kisiwa cha Anjouan, kikawa kimekombolewa na Kanali Bakari na wafuasi wake 22 kukimbilia kwenye Kisiwa cha Mayotte, kilichopo huko Ufaransa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, “Operesheni Demokrasi Comoro” ilikuwa ya mafanikio makubwa sana, ambapo kulikuwa hakuna uharibifu mkubwa wa mali wala vifo. Hata hivyo, tulimpoteza Askari mmoja, Koplo Raphael Sarakikya, aliyeefariki kwa bahati mbaya kwa kutumbukia baharini wakati wa maandalizi ya kupakia vifaa ndani ya meli.

Ninatoa pole nyingi sana kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa kumpoteza shujaa huyo ambaye bado Taifa lilimuhitaji sana. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, aipokee na kuiweka roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Baada ya Operesheni hiyo kumalizika, majeshi yameanza kurejea nyumbani na mapokezi rasmi ya majeshi yetu yalifanyika tarehe 24 Aprili, 2008 (jana), Mjini Dar es Salaam. Hata hivyo, Tanzania imeombwa kubakiza Wanajeshi 145 na Sudani Wanajeshi 130 ili kusaidia kuangalia usalama katika maandalizi ya uchaguzi unaotarajiwa kufanyika tarehe 31 Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kuvipongeza Vikosi vya Umoja wa Afrika, vilivyoshiriki katika “Operesheni Demokrasia Comoro” kwa kufanya kazi kwa uaminifu, umakini, umahiri na ujuzi wa hali ya juu, ulioepusha mauaji na uharibifu wa mali. Aidha, ninawapongeza kwa namna ya pekee, Wanajeshi wetu walioshiriki katika “Operesheni Demokrasia Comoro” walioongozwa kwenye Uwanja wa Mapigano na Luteni Kanali Anthony Msindai, kwa kazi nzuri na nidhamu ya hali ya juu, waliyoionyesha. Wapiganaji hawa wameliletea sifa Taifa letu ndani na nje ya nchi. Ninawapongeza sana na hongereni kwa ushindi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kwa kirefu masuala muhimu yanayolikabili Taifa letu hivi sasa; ni busara tuyaalangie maeneo haya kwa makini. Hii ni changamoto kwetu sisi sote. Kwa maana hiyo, ninapenda nimalizie kwa kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Tuwahimize Wananchi kuzingatia taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu kujikinga na Maafa. Vilevile tukubali kutumia tahadhari zinazotolewa, kwani “Kinga ni Bora Kuliko Tiba.”

(b) Maendeleo ya ulmwengu wa sasa yanaendeshwa na Sayansi na Teknolojia. Tuanze sasa kwa nguvu zote, kuhimiza umuhimu wa watoto wetu kupenda masomo ya hisabati pamoja na sayansi.

(c) Tuendelee kuhimiza wananchi kujitolea kujenga Shule za Sekondari kwa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na Kidato cha Tano hadi cha Sita.

(d) Mwisho, tunalo tatizo la kupanda kwa bei ya vyakula; tuwahimize wananchi kutumia nafasi hii, kuzalisha chakula cha kutosha na kukihifadhi ili ziada iwasaidie katika msimu unaofuata. Aidha, kwa kuzalisha zaidi kutasaidia kupunguza makali ya kupanda kwa bei ya vyakula hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwashukuru wote waliofanikisha Mkutano huu wa Bunge. Shukrani za pekee ni kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kudhihirisha kwamba, wewe ni mtu wa viwango na kasi inayohitajika. Ninamshukuru vilevile Naibu Spika, kwa kutuongoza vizuri pale ambapo Mheshimiwa Spika, alipata

dharura. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, kwa ufanisi mkubwa waliouonyesha wakati walipohitajika kutuongoza hapa Bungeni. (*Makofi*)

Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yenu mbalimbali wakati wa kujadili na kupitisha Miswada na Maazimio yote yaliyowasilishwa kwenye Mkutano huu. Ninamshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah na Wasaidizi wake, pamoja na Wataalam wote wa Serikali, kwa huduma mbalimbali ambazo zilifanikisha Mkutano huu. Ninawashukuru kwa namna ya kipekee, kwa michango yenu mikubwa na mizuri wakati wa kujadili hoja binafsi zilizowasilishwa na Wabunge wenzetu katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Ninawashukuru Waandishi wa Vyombo mbalimbali vya Habari, kwa kutoa taarifa za mambo yote yaliyojadiliwa katika Mkutano huu kwa wakati. Wote kwa ujumla wao ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninawatachia wote safari njema na naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi Siku ya Jumanne tarehe 10 Juni, 2008, Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana katika Mkutano wa Kumi na Mbili maalum kwa ajili ya Bajeti hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yako nzuri, pana na imechukua sekta nyingi; ina kina cha mambo mengi sana na nimekwishapata rai hapa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kadhaa kwamba, ichapishwe kwa haraka ili tuweze kugawiwa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Mambo ya Bunge, amenihakikisha kwamba, wiki ikayo tutakuwa nayo pale Dar es Salaam na tutahakikisha kwamba, hotuba zinawafikia Waheshimiwa Wabunge, kwa haraka kadri inavyowezekana. (*Makofi*)

Matangazo kidogo kabla sijawahoji. Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mweka Hazina wa Umoja wa Wabunge Wanawake wa Bunge letu (*TWPG*), anawakumbusha Wajumbe wote, yaani Wabunge Wanawake kwamba, kesho Jumamosi kutakuwa na semina saa tatu asubuhi, Ukumbi wa Pius Msekwa, itifaki zote za semina hiyo zimeandaliwa.

La pili, kwa mara ya kwanza, ninafurahi kutangaza kwamba, Kamati nzima ya Uongozi, pamoja na Makamu Wenyeviti, yaani *Steering Committee* ya Bunge, tutakuwa na semina ambayo nayo kwa mara ya kwanza, itafanyika Zanzibar Kiwengwa, tarehe 28 – 30 Mei, 2008.

Kabla ya zile Kamati, tutajifungia huko ili kuweza kujipanga vizuri namna ya kuliendesha Bunge hili. Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu na Makamu wao,

pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Masuala ya Bunge) na Mwanasheria Mkuu. Basi muiweke katika kalenda yenu ili mziweke tarehe hizo vizuri. (*Makofi*)

Ninapenda kutanganza kwamba, jana nilifahamishwa na Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, ameteuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwa Kamishna katika TACAIDS; ni jambo zuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tangazao la nne, mmeniona ninatumia kitaulo hiki na wengine mmeniandika kwamba, nina tatizo kubwa la afya, kwa sababu hapa siyo mahali ambapo unaweza kutokwa jasho au nimepigwa kipapai, yote si kweli.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 21 Desemba, 2007, nilifanyiwa *operation kule Bungalow*, India na nilipewa dawa ambazo ni za kutumia kwa miezi sita, kila siku asubuhi vidonge viwili na Daktari amenambia kwamba, moja ya *side effects* ni kwamba, *from time to time utatoka flashes* kidogo; Mheshimiwa Idd Simba anasema ni *menopause*, haihusu wanaume. Kwa kuwa Mzaramo mtani wangu basi! (*Kicheko*)

Kwa hiyo, nitarejea tena India tarehe 20 Mei kumalizia, maana yake ilitanguliwa na sindano na itamaliziwa na sindano; kuna sindano ya miezi sita ambayo unachomwa tumboni, ndiyo mambo hayo. Lakini nipo imara, sina *pressure*, wachawi hawaniwezi! (*Kicheko/Makofi*)

Tangazao la tano, niliwaarifu mapema kwamba, ninaandaa taarifa ya kujibu tuhuma dhidi yangu, lakini nimeshauriwa na Katibu na Wanasheria wa Bunge kwamba, kwa kuwa *CAG* sasa hivi anapitia Taarifa za Ukaguzi, haitakuwa na maana mimi niwe na taarifa ambayo wale wasionipenda kwanza, wataicheka tu watasema ninajikosha.

Kwa hiyo ni jambo zuri kwamba, *CAG* atapitia yote hayo; mambo ya matumizi na taarifa mtaiona; ni sehemu ya ukaguzi wa kawaida wa *Vote 42*, kama kweli kumeliwa shilingi milioni 60 au milioni mbili kwa matibabu au mambo mengine ya ovyo ovyo yale, basi *CAG* atatusaidia.

Kwa hiyo, sina wajibu tena wa kutoa taarifa, kwani ile ya *CAG* ni *professional* na itaonyesha matumizi yalivyo katika miaka miwili ya fedha za Ofisi ya Bunge.

Sasa nimalizie kwa shukrani; Waheshimiwa Wabunge, niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwashukuru kwanza Naibu Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, kwa jinsi alivyonisaidia, Wenyevit; Mheshimiwa Jenista J. Mhagana, Mheshimiwa Job Y. Ndugai na leo hii mmemwona Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, ametosha kabisa. Kwa hiyo, ninadhani *Budget Session* nitakuwa na kazi nyepesi kwa wasaidizi hawa. (*Makofi*)

Ninaomba kipekee, nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kazi ya Bunge inahitaji ushirikiano na Serikali, umewaongoza wenzako vizuri na tumeweza kufanya kazi zetu vizuri. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mwanzo huo mwema ambao tunakuombea uuendeleze. (*Makofi*)

Ninapenda niwashukuru Mawaziri wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, pamoja na Naibu Mawaziri. Vilevile ninapenda nimshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzanim Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamedm pamoja na Makamu wakem Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, tumekuwa na mashauriano mengi, ambayo yamesaidia kuyaweka vizuri masuala ya kitaifa na hivi ndivyo inavyotakiwa twende. (*Makofi*)

Ninawashukuru Wenyejiti na Makamu Wenyejiti wa Kamati zote, kwa kazi kubwa sana walifanya, kusimamia kazi za Kamati za Kisekta. Ninapenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ujumla wenu, mmefanya mengi na mmewezesha Mkutano huu wa Kumi na Moja kuwa mzuri na wa kihistoria. (*Makofi*)

Kipekee, nimshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, pamoja na wenzake wote, yaani Watumishi wote hususan Wakuu wa Idara mbalimbali; Kamati za Bunge, Shughuli za Bunge, vijana wangu wa *Hansard* na nisisahau Madereva, Wahudumu mbalimbali na niseme tu kwamba, Wahudumu *uniform* zao zimeanza kufifia; ukiacha hizi za rangi hii, zile nyingine zinazovaliwa kila siku, ndiyo! Kwa hiyo, Katibu ninaomba uchukue hatua ili Mkutano ujao wa Bunge, vijana wetu wawe wameng'ara zaidi kwa sababu wanafanya kazi kubwa sana.

Mtaalamu mmoja alitoa tathmini akasema, mhudumu mmoja anayehudumia Bunge kuanzia saa tatu hadi saa saba na saa kumi na moja hadi saa mbili kasorobo, anatembea kilomita 30. Kwa hiyo, siyo kazi ndogo hata kidogo.

Ninapenda kwa niaba yenu, niwashukuru Wakazi wa Dodoma, wenyeji wetu, wakiongozwa na *RC*, Mheshimiwa William V. Lukuvi. Ninadhani mtakubaliana nami, wametutunza vizuri sana. (*Makofi*)

Pale kwenye *Speaker's Gallery*, ninapenda kutambua kuwepo kwa Mama yetu, Mheshimiwa Tunu Pinda, tunakushukuru Mama kwa sababu ni vizuri katika mambo haya, kuonekana kwamba, upo kwa sababu tunaelewa mafanikio ya Mzee yanatokana sana kwa kiasi kikubwa na malezi mema ambayo unampa. Tunaomba uendelee kumlea, tunamhitaji sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba kuwahoji kuhusu hoja aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, Bunge liahirishwe hadi Siku ya Jumanne tarehe 10 Juni, 2008 saa tatu asubuhi hapa Dodoma.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Ninamwomba Mheshimiwa William Lukuvi kwamba, wale wasioafiki wabaki hapahaha Dodoma na wasipewe ukarimu wowote. (*Kicheko/Makofi*)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

*(Saa 8.00 mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 10 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*